Vodacom Tanzania Public Limited Company

# Taarifa ya mwaka

kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021



Pamoja tunaweza

# Maelezo ya Jumla

## Taarifa ya Mwaka 2021 ya Vodacom Tanzania

Hii ni taarifa ya tano ya mwaka ya Vodacom Tanzania, na ya nne tangu kampuni iorodheshwe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam tarehe 15 Agosti 2017.

Taarifa hii inatoa maelezo ya jumla ya biashara yetu, muundo wa biashara, mazingira ya uendeshaji, kupitia mikakati yetu, mafanikio ya mfumo wa uendeshaji na utawala kwa mwaka wa fedha ulioanzia tarehe 1 Aprili 2020 hadi 31 Machi 2021. Utaratibu wetu wa kutoa taarifa ya mwaka umekuwa ukiongozwa na kanuni na masharti yaliyo katika Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha (IFRS), Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam za mwaka 2016 na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Mkaguzi huru, Ernst & Young ('EY') amethibitisha taarifa zetu za fedha za mwaka na kutoa hati safi. (ukurasa wa 76 hadi 79 kwenye nakala ya kingereza).

Bodi imeshiriki kikamilifu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa hii. Bodi inaamini kuwa ripoti hii inaelezea masuala yote muhimu na inawasilisha maelezo yenye ulinganifu kuhusu utendaji wa kundi la Makampuni kwa kipindi husika na vilevile inatoa taswira halisi ya mikakati yetu ya utekelezaji.

Wakurugenzi wanaamini kuwa kuchapisha mipango mkakati ya Vodacom Tanzania, hakutaleta athari yoyote ile katika medani za ushindani wa kibiashara. Bodi ilipitisha taarifa hii ya mwaka tarehe 19 Agosti 2021.

Imesainiwa kwa niaba ya Bodi na:

| | |
|---|---|
| **Thomas B. Mihayo** | **Hisham Hendi** |
| Mwenyekiti | Mkurugenzi Mtendaji |
| 19 Agosti 2021 | 19 Agosti 2021 |

## Azma yetu kuu ya kuongeza thamani katika jamii

Azma kuu ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'. Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (UN SDGs) yanatoa taswira ya muonekano wa kesho iliyo bora, kwa kuweka malengo ya muda mrefu ya kuondoa umaskini, kulinda mazingira na kuleta mafanikio kwa wote ifikapo mwaka 2030. Vodacom Tanzania ina nia ya kutimiza wajibu kama taasisi ya sekta binafsi katika kufikia malengo haya, kuunga mkono serikali, jamii, biashara na watu binafsi katika kujenga kesho iliyo bora. Tunachangia kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya maendeleo kupitia biashara yetu kwa kuwezesha mawasiliano ya data, ujumbe, sauti na huduma za fedha na hivyo kutoa mchango muhimu katika kutimiza malengo ya maendeleo duniani.
Malengo ya Maendeleo Endelevu:




Vodacom Tanzania imeainisha na kuweka kipaumbele katika malengo nane ya maendeleo endelevu ambayo tunaamini tunaweza kuwa na mchango chanya.




## Yaliyomo

**Utangulizi**
Sisi ni nani 01
Thamani tuliyoijenga 02
Mapambano dhidi ya UVIKO-19: Kutekeleza mkataba wetu wa kijamii 04

**Biashara yetu**
Vodacom Tanzania kwa ufupi 06
Bidhaa na huduma zetu 07
Taarifa ya Mwenyekiti 08
Taarifa ya Mkurugenzi mtendaji 10

**Utendaji wetu**
Kutekeleza azma na wajibu wetu kwa jamii 14
Ufanisi wetu kifedha 18
Taarifa ya Vodacom Tanzania foundation 24

**Mfumo wa kiutawala**
Viongozi wetu 26
Taarifa ya uongozi wa kampuni 28
Shughuli za uongozi wa kampuni 30
Taarifa ya masuala ya ujira 32

**Maelezo ya hesabu za fedha za mwaka**
Taarifa ya wakurugenzi 36
Tamko la majukumu ya wakurugenzi 43
Tamko la mkuu wa kitengo cha fedha 43

**Taarifa za ziada**
Taarifa ya Mkutano Mkuu wa wanahisa 44
Fomu ya mwakilishi 48
Taarifa kuhusu umiliki 51
Taarifa kuhusu kampuni 52
Dai la Haki 53

### Maelezo ya msingi

Tafadhali zingatia kuwa hii ni tafsiri ya taarifa ya mwaka kwa ufupi. Taarifa kamili ya mwaka imetolewa kwa lugha ya kiingereza. Iwapo kutatokea mkanganyiko wa tafsiri, taarifa ya kiingereza itatumika.

# Sisi ni nani

Vodacom Tanzania ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania kwa kutoa huduma za mawasiliano kwa wateja wa matumizi binafsi na biashara ikiwa ni pamoja na huduma za simu sauti, data, ujumbe mfupi wa maneno na huduma za fedha kwa wateja zaidi ya milioni 14.9.

Vodacom Tanzania iliorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam mnamo Agosti 15, 2017. Mmiliki mkubwa wa Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu (yaani 'Kundi la Kampuni za Vodacom') ni Vodacom Group Limited, kampuni iliyosajiliwa Afrika Kusini ambayo nayo inamilikiwa na Vodafone Group PLC ya Uingereza.

## Azma yetu

### Kwanini tupo

Kutoa huduma nafuu ya intaneti.

Tunakuunganisha kwa kesho iliyo bora



**Jamii ya Kidigitali**
Kuwaunganisha watu na vitu kwenye intaneti



**Kuwashirikisha watu wote**
Kuhakikisha mawasiliano ya kidigitali yanapatikana kwa watu wote



**Sayari yetu**
Kupunguza athari kwa mazingira yetu

## Kwa namna gani

### Namna ya utekelezaji

1. Kuweza kuaminiwa na wateja
2. Kujenga mustakabali
3. Kufanya majaribio – kujifunza haraka
4. Kukamilisha mambo yote pamoja

## Mkakati wetu

### Tunachotakiwa kufanya

- Kuthaminisha huduma ya data na fursa za kidigitali
- Kuchochea ongezeko la wateja kupitia huduma ya M-Pesa
- Kuendelea kuimarisha huduma kwa wateja wa matumizi ya biashara kupitia bidhaa zetu mbalimbali
- Kuwa chapa inayoongoza. Kushikilia na kuongeza umiliki wa soko
- Kudhibiti gharama na kuwa na michakato yenye ufanisi
- Watu. Vipaji bora, kuzingatia taratibu bora

## Dira yetu

### Tunakoelekea na tunataka kuwa nani

- Kuwa kampuni ya kidigitali inayoongoza ambayo inawezesha jamii iliyounganishwa katika mtandao
- Kuiunganisha jamii kwa kesho iliyo bora
- Kuwa mwajiri bora (mahali bora pa kufanyia kazi)

# Thamani tuliyojenga

## Ufanisi wetu

| Wateja | Wateja katika soko | Wateja wa M-Pesa |
|---|---|---|
| milioni **14.9** (wamepungua kwa 4.2%) | **30.2%**[1] (nafasi ya kwanza) | milioni **7.4** (ongezeko la 10.6%) |

| Mapato ya huduma shilingi | Mapato ya data shilingi |
|---|---|
| bilioni **966.0** (yamepungua kwa 5.7% - robo ya nne ya mwaka yameongezeka 6.3%) | bilioni **186.9** (ongezeko la 3.3%) |

| Mapato ya M-Pesa shilingi | Gharama za uwekezaji shilingi |
|---|---|
| bilioni **356.8** (yamepungua kwa 0.4%) | bilioni **122.4** (sawa na 12.6% ya mapato) |

## Kwa wanahisa wetu

Shilingi bilioni 427.5

zimelipwa kama gawio la mwaka na gawio maalum kwa wanahisa wetu (2020: shilingi bilioni 54.5).

**Jumla**

Shilingi bilioni 549.3

zimelipwa kama gawio tangu Kampuni iorodeshwe kwenye soko la hisa miaka minne iliyopita.



## Kwa wateja wetu

**Tumewezesha mawasiliano kwa wateja zaidi ya**
milioni 14.9.

Tumepanua wigo kwa wanaofikiwa na huduma zetu.




**Tumepanua mtandao wetu kwa kuongeza**
**Minara 499** – ya 4G
**Minara 143** – ya 3G
**Minara 131** – ya 2G

**Tumeongeza huduma jumuishi za fedha kwa wateja wa M-Pesa zaidi ya**
milioni 7.4

- Tumetoa mikopo ya Songesha kwa takriban nusu ya wateja wetu wa M-Pesa.

**Kampuni ya**
kwanza
katika 'Net Promoter Score ('NPS')' tukiwa tunaongoza kwa alama 17.

## Kwa wafanyakazi wetu

Shilingi bilioni 61.6
zimetumika kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya kuendeleza ujuzi.

**Tumetoa mafunzo ya kujiendeleza kwa njia ya mtandao kwa kwa zaidi ya**
wafanyakazi 400.

- **Tumeendesha awamu sita za mafunzo ya afya**, tatu kuhusu UVIKO-19 na tatu kuhusu ustawi wa jumla kwa wafanyakazi wote pamoja na kuwapatia vifurushi vya usafi binafsi dhidi ya UVIKO-19.
- **Tumewaruhusu wafanyakazi ambao hawalazimiki kukutana moja kwa moja na wateja** kufanya kazi wakiwa nyumbani ikiwa ni hatua ya kujikinga dhidi ya UVIKO-19.
- **Tumewawezesha wafanyakazi kupata huduma ya ushauri wa afya** inayolipwa na kampuni.

## Katika jamii yetu

**Tumechangia jumla ya**
Shilingi bilioni 429.7
kwenye fedha za umma kwa njia ya kodi na tozo, masafa na tozo za mamlaka za udhibiti wa sekta.

Tumeunga mkono programu za Serikali za kufikisha mawasiliano vijijini kwa kujenga
minara 260
**katika kipindi cha miaka tisa iliyopita.**

Shilingi bilioni 425.6
zimetumika kwa ajili ya malipo ya bidhaa na huduma za wasambazaji wa ndani na makampuni washirika zaidi ya 400 nchini Tanzania.

**Zaidi ya**
Shilingi bilioni 0.5
zimetumika katika uwekezaji katika jamii, na kunufaisha zaidi ya watu milioni 1.4[1] nchini kote.

**Zaidi ya ajira**
149 000[2]
zisizo za moja kwa moja zimetolewa kwa watanzania.

1. Pamoja na shughuli za kijamii zilizofanyika moja kwa moja kwa wateja wetu.
2. Pamoja na wafanyabiashara huria (freelancers) na mawakala wa M-Pesa.

# Hatua dhidi ya UVIKO-19

## Kutekeleza wajibu wetu kwa Jamii


Kwa kuzingatia dira ya kundi la makampuni ya Vodacom, lengo la Vodacom Tanzania ni "Kuiunganisha jamii kwa kesho iliyo bora". Tukiwa ni kampuni ya kiteknolojia, tunatumia huduma zetu za teknolojia na mawasiliano kuwaunganisha watu na kuziwezesha biashara kufanyika kwa ufanisi na mafanikio katika ulimwengu unaokua wa kidigitali. Mawasiliano bora huongeza ubora wa maisha, huongeza ufanisi na kuwezesha kuishirikisha zaidi jamii kupashana habari baina ya watu, jamii na biashara mbalimbali.

**Katika kutekeleza lengo hili, Vodacom Tanzania imedhamiria kutekeleza wajibu huu kwa jamii, kwa kuzingatia kanuni tatu:**

- Kuhamasisha **tabia ya kuwajali** wateja wetu kupitia bidhaa za bei nafuu na rahisi kutumia zinazotolewa zenye ubora wa hali ya juu.
- Kuhakikisha **usawa** na kuhamasisha ushirikishaji kidigitali, kwa kuongeza upatikanaji wa bidhaa, huduma na miundombinu ya kidigitali.
- Kuonesha na **kuongoza** ubunifu katika kusukuma mabadiliko kuelekea jamii ya kidigitali.



Lengo la kutimiza wajibu wetu kwa jamii linaakisiwa na jitihada zetu za kupambana na UVIKO-19. Baada ya tukio la kwanza la UVIKO-19 kuripotiwa mnamo Machi 2020, tumetekeleza na kuendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha usalama wa wafanyakazi na makandarasi wetu, na kuendelea kuwaunganisha watu, biashara na serikali katika mawasiliano.





Tumewekeza ili kudumisha ubora wa mtandao wetu na kuwezesha mawasiliano.

Tumeendelea kuimarisha mfumo wa M-Pesa na huduma za kifedha kuwezesha malipo ya kielekroniki.

Tuliondoa tozo kwenye kurasa mtandao za serikali zenye taarifa za UVIKO-19 na kushiriki kwenye kampeni ya wizara ya afya kuelimisha jamii.

Tumeunga mkono serikali kwa kutoa msaada kwa vitengo muhimu vya serikali, ikiwa ni pamoja na:

- Kutoa mawasiliano ya intaneti bure kwa vikosi maalum vya serikali, upatikanaji wa data bure kwa Taasisi ya Utafiti wa Tiba (NIMR), na data isiyo na ukomo kwa wafanyakazi wote katika vituo maalum vya kupambana na UVIKO-19.
- Kuipatia wizara ya afya visambaza data na laini za simu kwa ajili ya data ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya intaneti bure na kuharakisha mawasiliano na shughuli mbalimbali.
- Kuchangia vifaa vyenye thamani ya Dola milioni 1 za Marekani (sawa na Shilingi bilioni 2.3) kupitia kitengo chetu cha huduma kwa jamii ili kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya kuenea kwa ugonjwa huu.

Tumewezesha wateja kufanya kazi wakiwa nyumbani, na kusaidia biashara ndogondogo kupitia upatikanaji wa vifurushi maalum vya data, vifaa vya kuunganishia data (modem), na kutoa mafunzo jinsi ya kutumia vifaa vya kufanyia kazi nyumbani.

Tumetoa fursa ya upatikanaji wa huduma ya elimu bure kwa wanafunzi wakati shule zilipokuwa zimefungwa, ikiwa ni pamoja na huduma kupitia mtandao kama vile 'Instant Schools' na 'Shule Direct'. Pia tuliondoa tozo kwenye kurasa mtandao za kielimu kuwezesha mafunzo nje ya shule.


Tumewaelimisha wananchi kuhusu UVIKO-19, tumetuma SMS kwa wateja milioni 14.9 kuhusu hatua za kiafya za kujikinga. Sambamba na hayo, tumetoa bure viunganishi vya kurasa za tovuti zenye maudhui ya UVIKO-19 pamoja na huduma ya kupiga simu namba 199 bila makato kwenda kwenye kituo cha ushauri wa afya.




Juhudi hizi zimewezeshwa kwa kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kunakuwa na usalama wa wafanyakazi na makandarasi, kuhakikisha kuwa sote tunatumia teknolojia ya kidigitali kupunguza maambukizi ya UVIKO-19 na kuwaunganisha watu kwa ajili ya kesho iliyo bora.


1. Pamoja na shughuli za kijamii zilizofanyika moja kwa moja kwa wateja wetu

# Vodacom Tanzania
## kwa ufupi





**Uwekezaji kwa miaka 4** (Shi bilioni)





**Idadi ya ya minara**




**Wateja wa siku 90** (Shi milioni)





**Idadi ya minara ya 4G**




**Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu**





**Idadi ya watu wanaofikiwa na mtandao wetu wa 4G**



# Bidhaa na huduma zetu

Tuna wateja zaidi ya **milioni 14.9** wanaotumia bidhaa na huduma zetu.




**Huduma kwa matumizi ya wateja binafsi na kidigitali**

Sauti
- Simu za kiganjani

Data
- Modemu za broadband
- Intaneti kwa simu
- Mkongo
- Simu za kutumia waya

Ujumbe mfupi
- Ujumbe mfupi wa maneno na programu za mitandao ya kijamii

Huduma zilizoongezwa thamani
- Video kadiri ya mahitaji
- Kusikiliza muziki
- Video mbashara
- Michezo, bahati nasibu
- Habari, huduma za mikopo ya muda wa hewani

Huduma kwa wateja
- Kituo cha mawasiliano, dawati la huduma kwa wateja
- Maduka ya Vodacom, huduma binafsi (My Vodacom app, USSD code)
- Huduma za kidigitali (kupitia mitandao ya kijamii
- Tovuti, WhatsApp na Live Chat app) na viashiria kwa wateja (ujumbe ibukizi)

**Matumizi ya wateja wa Biashara**

Simu za kiganjani
- Sauti
- Intaneti
- Ujumbe mfupi wa maneno
- Video

Uunganishaji
- Pasi waya
- kwa waya
- VPN
- Mkongo, intaneti maalumu na ya kushirikiana

Kusimamia shughuli kwa mtandao
- Intaneti ya Vitu ('IoT')
- APN kwa ajili ya makampuni

Usalama, 'cloud' na Kuunganisha ('hosting')

Bidhaa na huduma maalum
- Huduma kwa wakulima 'Connected Farmer' au 'M-Kulima'
- Huduma kwa mashule 'VodaShule', 'Connected education'

**M-Pesa**

Kuweka na kutoa fedha
Kwa mawakala zaidi ya 123 000

Kuhamisha fedha toka kwa mtu kwenda kwa mtu mwingine
Kutuma pesa ndani ya nchi na kimataifa (IMT)

Mifumo ya malipo ya kielektroniki
- Kadi za kieletroniki "M-Pesa Mastercard"
- Mfumo wa malipo wa kulipa kwa Simu
- Mteja kwenda kwenye Biashara ('C2B')
- Biashara kwenda kwa Mteja ('B2C') na
- Biashara kwenda kwenye Biashara ('B2B')

Huduma za Malipo na Mikopo
- Huduma ya mikopo ya Songesha
- Akaunti ya akiba ya M-Pawa
- M-Koba kwa ajili ya mikopo na kuweka fedha za vikundi
- Akaunti ya akiba ya Halal Pesa ambayo inafuata miongozo ya Sharia



# Taarifa ya Mwenyekiti

**Huu ni mwaka wangu ya kwanza nikiwa mjumbe na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom Tanzania PLC (Kampuni). Hivyo nina furaha na heshima kuiwasilisha ripoti ya nne ya pamoja ya Kampuni tangu iorodheshwe katika Soko la Hisa la Dar es Salaam mnamo Agosti 2017. Kampuni hii inabaki kuwa ya kwanza na pekee ya simu iliyoorodheshwa nchini Tanzania.**

Ingawa nimekuwa kwenye Bodi ya Vodacom Tanzania PLC tangu tarehe 1 Novemba 2020, lakini nimekuwa nikishiriki katika Kampuni kama mmoja kati ya wateja wa Vodacom tangu ilipoanzishwa zaidi ya miaka 20 iliyopita. Kama mteja, nimepata uzoefu wa moja kwa moja wa ubora wa huduma zake, mtandao wake, na bidhaa na huduma zake mbalimbali za kidigitali.

Tangu nilipojiunga katika Bodi, nimevutiwa na namna Kampuni ilivyoweka utaratibu makini wa kuwapokea wajumbe wapya wa bodi na kuwapa uelewa kuhusu shughuli na utendaji wa Kampuni. Kupitia utaratibu huu, nimepata ujuzi kuhusu utendaji wa Kampuni na mihimili yake kimkakati, ubora wa taratibu zake za kiutawala na mifumo ya usimamizi, pamoja na uimara wa muundo wa utamaduni wa kitaasisi.

Hatua zilizochukuliwa na Kampuni katika mapambando dhidi ya janga la UVIKO-19, zimedhihirisha ubora wa utamaduni na uongozi wa Kampuni, na zimethibitisha kuwepo uimara wa mfumo wa kibiashara katika wakati huu mgumu. Janga hili limevuruga taratibu za kijamii na kiuchumi, limeleta ugumu mkubwa kwa familia na jamii, na kuleta changamoto kwa namna mbalimbali ambazo makampuni yamekuwa yakizitumia kufanya biashara.



Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo

Kwa nafasi yangu nyingine niliyonayo kama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Utalii Tanzania, nimeshuhudia athari za janga hili kwenye sekta ya utalii, ambayo ni sekta muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi. Kwa kuzingatia muktadha wa kijamii na kiuchumi nchini Tanzania, ambapo sehemu kubwa ya watu wanaendesha maisha yao kwa kipato cha kutwa, athari za kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii zingesababisha madhara makubwa yasiyovumilika. Ili kupambana na changamoto hii ipasavyo, kulihitajika jitihada kubwa zinazoratibiwa kati ya serikali, wafanyabiashara na jamii. Hivyo serikali yetu inastahili pongezi ilipoamua kuchagua kuacha kuzuia shughuli za kiuchumi nchini.

Uthabiti na utekelezaji mzuri wa mikakati ya uendeshaji imewezesha Kampuni kupata matokeo chanya kifedha ukizingatia changamoto za kuenea kwa janga la UVIKO-19, mazingira ya kiudhibti na shinikizo la bei. Katika kutekeleza mkakati wake, Kampuni imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha usalama na ustawi wa wafanyakazi na makandarasi wake, na kuwaunganisha watu, jamii, biashara na serikali kwa kudumisha mtandao ulio bora na imara.

Kulingana na madhumuni yake, imeendelea kuiunga mkono serikali na jamii kwa kutoa huduma muhimu za kujenga uwezo na huduma saidizi, kuchochea jitihada zake katika huduma za fedha jumuishi, kilimo cha kujikimu na elimu kwa mtandao, na kuchukua hatua kupunguza baadhi ya athari za janga la UVIKO-19 kwa biashara zilizoathiriwa zaidi.

Ili mchango wa biashara uweze kudhihirika katika jamii , ni muhimu kushirikiana na serikali na wadhibiti kwa kujenga mahusiano chanya. Ili kuchochea upatikanaji wa matokeo haya, yatupasa kuimarisha majadiliano na kushughulikia tofauti kati ya serikali, wadhibiti na biashara. Changamoto katika mahusiano haya, imekuwa dhahiri katika majadiliano yanayohusu bei ya data ambayo ni ya chini sana hapa nchini. Bei hii ya chini na isiyohimilika, inakwamisha uwekezaji unaohitajika sana katika miundombinu ya mtandao na kukwamisha ubunifu muhimu kwa ukuaji na maendeleo ya kiuchumi.

Tumeona maendeleo yanayoridhisha mwaka huu katika majadiliano kuhusu sera ya bei na sera nyinginezo baina ya Kampuni na serikali na wadhibiti – TCRA kwa huduma za GSM na Benki Kuu ya Tanzania kwa huduma za fedha – tukitafuta suluhisho la muda mrefu kwa manufaa ya pande zote. Kuendelea kuijumuisha jamii kidigitali na kuhakikisha kuenea kwa huduma za unganishi za mitandao, ni mifano muhimu ya matokeo ya mikakati ya makusudi, ambayo iwapo itaendelezwa itakuwa na faida kwa wadau wote. Upatikanaji wa faida ya maendeleo ya huduma za kidigitali unategemea kuwepo kwa mfumo wa udhibiti na fedha ambao unatengeneza mazingira ya uhakika, vivutio, usalama wa uwekezaji wa muda mrefu, unaochochea ubunifu, na kukabili changamoto za kijamii na kimazingira. Ili kudhihirisha uwajibikaji wetu kwa taifa, tumedumisha utamaduni wetu wa kutimiza azma yetu kwa usahihi, wakati pia tukiendeleza uwazi na uwajibikaji.

Hatuna budi kama Kampuni tutambue wajibu mpana wa kijamii kuliko kulenga faida ya muda mfupi, na kuwa tunatambua kuwa uwezo wetu kujenga thamani ya muda mrefu unategemea, uwezo wa jamii kiuchumi katika mazingira tunayotoa huduma, uhusiano bora na wadau wetu na usimamizi madhubuti wa rasilimali tunazozitegemea.

Namna yetu ya kutimiza wajibu huu imeelezwa kwa kina katika taarifa hii. Ninahimiza kila mmoja wenu, kama mdau wa Vodacom Tanzania PLC, kupitia taarifa yetu ya utekelezaji na mkakati, na kutupatia mrejesho bayana kuhusu matokeo ya uendeshaji.

Nafasi yangu kama Mwenyekiti ni kuhakikisha kuwa Bodi inafanya kazi ya kuongoza kwa makini, kusimamia utekelezaji na mwelekeo wa kimkakati wa Kampuni, na kuhakikisha kuwa uongozi unawajibika kwa uaminifu, kuzingatia maadili na jamii. Katika kutekeleza kazi hii, tuna bahati ya kuwa na Bodi ambayo ina watu wenye utaalamu, uzoefu na mitazamo mbalimbali. Ninapenda kuwashukuru wajumbe wenzangu katika Bodi kwa kuniunga mkono kikamilifu tangu nilipochukua nafasi ya uenyekiti. Kwa niaba ya Bodi, ninapenda kumshukuru Hisham Hendi ambaye chini ya uongozi wake, Vodacom imekuwa kinara katika kutekeleza mkakati wa maendeleo ya kidigitali ambao umechochea ukuaji wa huduma jumuishi ya kifedha nchini kupitia huduma za kibunifu za fedha kwa simu, na amekuwa mstari wa mbele katika kufanikisha uwekezaji wa mawasiliano na kuunganisha mamilioni ya Watanzania. Ninamtakia Hisham na familia yake kila la heri katika shughuli zake mpya.

Tunasubiri kwa hamu ujio wa Mkurugenzi mtendaji wetu mpya, Sitholizwe Mdlalose. Anakuja na uzoefu na ufahamu katika nafasi hii muhimu na ya juu ya uongozi, lakini pia ana rekodi nzuri ya kukuza biashara kupitia mikakati ya kimageuzi. Uteuzi wake unaakisi jitihada za Bodi ya Vodacom Tanzania kuimarisha nafasi yetu katika sekta hii muhimu na kuendeleza dhima ya Vodacom, ya kuunganisha wateja wake kwa kesho iliyo bora.



**Jaji (mstaafu) Thomas B. Mihayo**
Mwenyekiti

19 Agosti 2021

# Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji

**Athari mbaya kwa jamii kutokana na janga la UVIKO-19, zilidhihirisha umuhimu wa utayari wa Vodacom Tanzania, ilipochukua hatua za haraka kusaidia jamii kwa namna mbalimbali.**

**Mbali na kuweka kipaumbele cha kuimarisha mtandao wetu na kuwezesha kutoa huduma za malipo kwa mtandao, tuliunga mkono jitihada za serikali kwa kuchangia jumla ya shilingi bilioni 2.3 kuwezesha ununuzi wa vifaa tiba na madawa na kuondoa tozo kwenye huduma muhimu za mawasiliano pamoja na kurasa mtandao za elimu.**

Katika masuala ya kifedha, mapato na faida vilipungua kutokana na athari ya kufungia huduma za simu kwa wateja milioni 2.9, mwishoni mwa mwaka uliopita wa fedha pamoja na ongezeko la ushindani. Vilevile, athari za janga la UVIKO-19 kwenye shughuli za kiuchumi, ziliathiri matumizi ya wateja.

Ijapokuwa sababu hizi zilichangia katika kushuka kwa mapato ya huduma kwa 5.7%, kulikuwa na mafanikio mazuri ya ongezeko la mapato ya huduma katika nusu ya pili ya mwaka, yakichagizwa na ongezeko la mapato ya data na M-Pesa. Muhimu zaidi, tumeendelea kuongoza kwa kuwa na 30.2% ya wateja wote katika soko, na kuendelea kushikilia nafasi yetu ya kwanza katika 'net promoter score' tukiongoza kwa pointi 17 kati yetu na mshindani anayefuata, licha ya watoa huduma wengine kutumia mbinu zisizo na mwelekeo wa muda mrefu za kuongeza wateja.

Kuanzia tarehe 1 Aprili 2020, biashara ya M-Pesa ilianza kuendeshwa kama kampuni inayojitegemea ikitumia jina la M-Pesa Limited, na kumilikiwa kikamilifu na Vodacom Tanzania PLC, kwa kufuata sheria ya Mfumo wa Malipo ('the National Payment System Act'). Wakati biashara ya M-Pesa ilipata faida, biashara ya 'GSM' iliingiza hasara. Hii iliathiri vigezo vya kukokotoa kodi mwaka huu, na kusababisha ongezeko la malipo ya kodi ukilinganisha na mwaka uliopita.

Tulifurahi kuweza kulipa gawio maalum la shilingi 178.57 kwa kila hisa ambapo jumla ya shilingi bilioni 400 zililipwa kwa wanahisa tarehe 13 Novemba 2020. Tukiangalia mbele, tunapata matumaini kutokana na dalili za awali za mageuzi ya sekta ambayo yanaweza kurejesha ukuaji na kuchochea uwekezaji katika sekta. Wakati tunapita katika kipindi hiki cha mageuzi, tunaendelea kujikita katika kutoa huduma bora na za kipekee kwa wateja wetu. Tunatarajia mikakati yetu ya kupunguza gharama na hatua madhubuti za kuchochea ongezeko la huduma za kidigitali na fedha zitaongeza uwezo wa kutengeza faida ya kundi la makampuni katika mwaka ujao wa fedha. Wakati tunaendelea kuwa na mafanikio mazuri katika usajili wa laini za simu, tunamashaka na athari za UVIKO-19 na kasi ya hali ya uchumi kuimarika, ambavyo vinaweza kuathiri kipato cha mtu mmoja mmoja kutokana na kudhoofika kwa shughuli za kiuchumi

## Utekelezaji wa malengo yetu kimkakati

Ufanisi wetu mwaka huu unaakisi utekelezaji madhubuti wa mkakati wetu, katika maeneo yetu muhimu ya kimkakati, licha ya kuwepo changamoto za kuenea kwa janga la UVIKO-19.

### Kuthaminisha huduma ya data na fursa za kidigitali

Tumefanikiwa kuwa na matokeo chanya katika msukumo wetu wa kuchochea huduma jumuishi za kidigitali na kuogeza thamani ya huduma zetu kwa wateja. Matumizi ya data yameongezeka kwa 47.2% ongezeko kubwa likichochewa na



Hisham Hendi

Shilingi
**178.57**
kwa kila hisa
**Gawio maalum**

Shilingi bilioni
**186.9**
**Mapato ya data za simu**
ongezeko la 3.3%

matumizi ya 4G, ikiakisi uwekezaji wetu endelevu katika mtandao, mkakati wa kusambaza simu janja, kuongeza ubora wa huduma kwa wateja kwa kutoa ofa mbalimbali na kuimarisha ubora wa huduma za data. Watumiaji wetu wa simu janja wamefika milioni 3.7 ikiwa ni ongezeko la 7.0%. Ongezeko hili kubwa limetokana na kampeni za kuongeza matumizi ya simu janja, kwa kusambaza simu janja za bei nafuu kwa wateja, ikihusisha masharti nafuu ya malipo.

Mapato ya data za simu yaliongezeka kwa 3.3% hadi shilingi bilioni 186.9 licha ya wateja 600 000 wa data kufungiwa huduma katika robo ya mwisho wa mwaka jana. Ingawa tuliripoti ongezeko kubwa la matumizi ya data, wastani wa bei kwa megabaiti uliakisi ushindani mkubwa wa soko na hii inasababisha hatari ya kupungua kwa mapato ya sekta ya mawasiliano.

Tumewekeza shilingi bilioni 122.4 (12.6% ya mapato) katika kupanua wigo wa mtandao wetu, kuongeza uwezo wa mtandao, na kuboresha miundombinu yetu ya TEHAMA. Tumeongeza minara 499 ya 4G na 143 ya 3G nchini, na kupanua wigo wa 4G kufikia 42%  ya watu kutoka 33% mwaka uliopita; na kuongoza katika sekta.

Tumeongeza minara mipya 131 ya 2G, na kufanya wigo wetu wa 2G kufikia 93% ya watu ambayo inaakisi lengo letu la kuongeza matumizi jumuishi ya kidigitali, na kuunga mkono program ya serikali ya kuongeza wigo wa huduma za mawasiliano vijijini.

Tangu tulipomteua mkurugenzi wa huduma za kidigitali na kuanzisha idara mpya ya huduma za kidigitali, tumeendelea vizuri katika kuongeza huduma zetu za kidigitali. Mapato ya huduma za kidigitali yaliongezeka maradufu, yakichochewa na ongezeko la bidhaa na kuimarisha huduma kwa wateja. Tumepiga hatua nzuri katika program yetu ya kuendeleza vipaji vya ubunifu katika bidhaa za kidigitali, tuliyoandaa kwa ubia na Smart Lab kuwasaidia wabunifu chipukizi kuendesha biashara zao kwa faida. Tumewekeza shilingi milioni 350 kwenye programu hii, kwa kutumia rasilimali zetu kusaidia na kutoa ushauri kwa kampuni 15 zilizoteuliwa – katika maeneo ya teknolojia ya fedha, elimu, afya, biashara mtandao na mazingira ili kubadili maono yao kuwa biashara zenye thamani. Juhudi hizi zinawawezesha vijana wabunifu wa Kitanzania kuzalisha nafasi za ajira na kutatua matatizo ya jamii, na pia kuongeza hadhi ya chapa ya Vodacom katika jamii ya wafanyabiashara wanaochipukia katika huduma za kidigitali



**Kuongeza kasi ya ongezeko la wateja kupitia M-Pesa**
M-Pesa imeendelea kuwa huduma muhimu inayowezesha huduma jumuishi kifedha kwa kuwezesha wateja kufanya miamala ya kielektroniki kwa urahisi. Ongezeko la bidhaa zilizotolewa zimechochea ukuaji wa mfumo huu na ongezeko la watumiaji wa huduma hizi za kidigitali. Kufikia tarehe 31 Machi 2021, tumehudumia wateja milioni 7.4 wa M-Pesa, ambao ni sawa na 49.8% ya wateja wote.

Kupitia M-Pesa tumetoa huduma za miamala ya thamani ya shilingi trilioni 69 katika mwaka, ikiwa ni ongezeko la 18%. Huduma yetu ya mkopo ya Songesha, imeendelea kufanya vizuri ikiwa na ongezeko zuri mwaka huu. Biashara yetu ya kuhamisha fedha kimataifa pia inaendelea kuchukua nafasi muhimu katika kuunga mkono huduma jumuishi ya kifedha ikiwa ni ongezeko la zaidi ya mara mbili katika fedha zilizopokelewa kutoka nje  hadi kufikia miamala ya zaidi ya shilingi bilioni 500 na fedha zilizotumwa nje zaidi ya shilingi bilioni 70, ongezeko la zaidi ya 35%.

Ubia wetu na zaidi ya makampuni 900 umeendelea kuwezesha huduma za malipo kwa haraka, urahisi na salama kupitia mfumo wa M-Pesa, kukiwa na miamala ya zaidi ya shilingi trilioni 4.0 iliyofanyika kati ya biashara na wateja wao.

**Kuendelea kuimarisha huduma kwa wateja wa Kibiashara**
Kupitia kitengo cha wateja wa biashara, tuliimarisha mkakati wetu wa kuongeza huduma za mfumo wa IoT, bidhaa za kidigitali za kilimo na elimu hivyo kuongeza wigo wa huduma zetu. Tumejenga ubia ambao utachochea na kuongeza kiwango cha huduma hizi na tumeshirikiana kikamilifu na kampuni ya Mezzanine katika kuzindua bidhaa zetu za kidigitali za kilimo na elimu. Kufika tarehe 31 Machi 2021, tulikuwa na zaidi ya wakulima wadogo 100 000 waliosajiliwa katika bidhaa yetu ya 'M-Kulima' na vilevile tumeona ukuaji unaoridhisha katika usajili wa shule mpya na wanafunzi katika majukwaa ya 'connected education' na 'VodaShule'.



**Watu: Vipaji bora, utekelezaji bora**

Ili kuwezesha mpito wetu kuwa kampuni ya teknolojia inayokidhi mahitaji ya siku zijazo, mwaka huu tumelenga kikamilifu katika kujenga utamaduni wa Vodacom, kwa kuwashirikisha wafanyakazi katika matukio yanayolenga kuimarisha lengo letu na kudumisha utamaduni unaojenga ubunifu, ushirikiano na kujifunza kwa wepesi, na hivyo kujenga uwezo wa kujisimamia kwa mtu mmoja mmoja na ki-idara. Ni jambo linalotia moyo kuona kuwa Vodacom Tanzania PLC imepata alama za juu kabisa katika Kundi la makampuni ya Vodacom, katika kipengele cha umoja na ushirikishwaji katika kazi , ikionesha mabadiliko chanya ya utamaduni wa utendaji na mahusiano kazini. Kuhamasisha ushirikishwaji wa wazawa na uwakilishi wa makundi mbalimbali wa wafanyakazi, ni muhimu katika kutimiza azma yetu. Mwaka huu, tumeteua wakurugenzi watatu wapya, wote wakiwa ni Watanzania, na hivyo kuongeza uwakilishi wa wazawa katika kamati yetu ya uongozi kufika 72.7% kutoka 30.8% miaka minne iliyopita. Tumeendelea kupiga hatua zaidi mwaka huu kuelekea lengo letu la mwaka 2023 kuhusu uwakilishi wa jinsia na ujumuishi: mwishoni mwa mwaka, 36.4% ya wajumbe wa timu ya menejimenti walikuwa wanawake, kutoka 30.8% mwaka uliopita.

## Mtazamo wetu kimkakati na azma yetu kutimiza malengo

Kuenea kwa janga la UVIKO-19 kumedhihirisha umuhimu wa huduma za mawasiliano ya simu na fedha, kwa namna ambavyo wateja wetu waliongeza kasi ya matumizi ya huduma za kidigitali. Azma yetu ya kuiunganisha jamii kwa ajili ya kesho iliyo bora pamoja na uwekezaji wetu kwenye rasilimali watu, mtandao na mifumo ya kidigitali vinapaswa kuwezesha mabadiliko kuelekea ulimwengu wa kidigitali. Hata hivyo, mageuzi katika sekta yanabaki kuwa kipengele muhimu kitakachosaidia uwekezaji kwa siku zijazo. Mahitaji ya huduma za data na M-Pesa ni makubwa, sambamba na mkakati wetu wa huduma jumuishi za kifedha na kidigitali. Tunaendelea kuwekeza na kupanua mfumo wa majukwaa haya tukitegemea hii itakuwa ni kichocheo cha ukuaji siku zijazo. Pia tumepiga hatua kubwa kuhakikisha kuwa tunaongeza wigo wa vyanzo vya mapato kupitia huduma zetu za kidigitali. Program zetu za 'fit for growth' zimejikita vyema katika biashara yetu na kwa kiwango kikubwa zimejielekeza katika muundo na mageuzi ya kidigitali ambayo inatupata fursa ya kuchukua hatua za muda mfupi za kudhibiti gharama ili kuzidi kuimarisha biashara yetu pale inapohitajika. Biashara ya huduma kwa makampuni inabaki kuwa lengo muhimu katika mwaka ujao. Kupitia kitengo cha huduma kwa makampuni, ('Vodacom Business'), mkakati wetu ni kubadilika kutoka utaratibu wa kutoa huduma zilizozoeleka na kwenda kwenye utaratibu wa kisasa na bora wa huduma za kidigitali. Tutalinda na kukuza umiliki wa soko katika kitengo chetu cha huduma kwa makampuni, kupanua mtandao wetu wa simu za waya, na kuchochea huduma za intaneti, M-Pesa na mfumo wa IoT, na kutumia fursa za kusisimua kupitia ofa za huduma za kidigitali katika kilimo, elimu na uzalishaji viwandani.

Jitihada hizi za ukuaji zitawezeshwa na shughuli zinazohusiana na kudumisha chapa yetu madhubuti, kuimarisha mahusiano na wadau wetu, kuwa na ufanisi kiuendeshaji, na kujenga utamaduni unaoendana na azma ya Kampuni.

Tutakuwa na mwelekeo maalum katika kuimarisha majadiliano yetu na wasimamizi wa sekta yetu, ili kuhakikisha muundo wa soko na viwango vya bei vinachochea uwekezaji wa muda mrefu katika miundombinu inayohitajika ili kuwezesha utoaji wa huduma bora na kuleta manufaa yanayotokana na kuboreshwa kwa huduma za kidigitali.

Mwelekeo wa kiuchumi usiotabirika duniani na kikanda ni tatizo ambalo linaendelea kuwepo. Hali hii isiyotabirika inadhihirisha wajibu wetu kama biashara, na nafasi muhimu biashara yetu inavyoweza kuunga mkono juhudi za serikali na jamii katika kukuza maendeleo jumuishi ya kiuchumi kwa kunufaika na uwezo wa teknolojia za kidigitali, kuwezesha jamii iliyounganishwa kimtandao. Tunaamini jukumu hili, na uwekezaji wetu katika ukuaji wa kiuchumi unaweza kuchochewa kupitia mageuzi katika sekta, hususan kuwa na bei sahihi za data.

Jinsi athari za kuenea kwa janga la UVIKO-19 zinavyoendelea kujidhihirisha, sambamba na mwelekeo wa uchumi usiotabirika, tunatarajia hali ya uchumi kuimarika kwa mwaka wa fedha ujao. Mtazamo huu umetolewa na watafiti wa masuala ya kiuchumi wa kimataifa na taasisi za fedha kama vile Benki ya Dunia. Sambamba na matokeo ya awali ya jumla ya fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 yaliyotolewa tarehe 17 Mei 2021, tulitoa mwongozo kuwa kuimarika kwa hali ya uchumi pamoja na kuhitajika wa huduma zetu, vinatupa msingi wa malengo yetu ya muda wa kati kama ifuatavyo:

- Ongezeko la mapato ya huduma kuanzia kiwango cha kati hadi juu kwa tarakimu moja
- 13.0% – 14.5% ya matumizi ya mtaji kama asimilia ya mapato


Mara baada ya kutoa taarifa ya awali ya hesabu za jumla, tarehe 30 Juni 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ali idhinisha mabadiliko ya Sheria ya Fedha iliyobadilisha Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa – iliyoanzisha tozo kwenye miamala ya fedha kupitia simu za mkononi. Tozo hizi zilizoanzishwa na serikali Julai 2021, zimeathiri utendaji na mapato ya biashara. Tozo hizo ni sawa 4.4% ya thamani ya muamala, na hivyo kuongeza mzigo mkubwa wa gharama kwa mtumiaji wa mwisho. Mapato yetu na faida ya M-Pesa yameathiriwa kwa kiwango kikubwa na kuanzishwa kwa tozo hizi. Athari hii ya ukuaji inategemewa kuendelea, japo kwa kiasi cha kati kutokana na punguzo la 30% la tozo hizi linalotarwajiwa kuanzia mwezi Septemba kwani pamoja na punguzo hilo la tozo hizo bado ongezeko la gharama kwa mtumiaji wa mwisho ni kubwa. Tunaendelea kushirikiana na serikali kutathmini athari za tozo hizo kwenye sekta na kiuchumi.

Vilevile, tunaendelea kutathmini athari ya tozo hii katika malengo yetu ya muda wa kati na tutawajulisha viwango vipya vya matarajio ya utendaji na ufanisi wetu tutakapotoa taarifa ya nusu mwaka unaoishia tarehe 30 Septemba 2021 hapo tarehe 12 Novemba 2021.

## Shukrani

Katika kuhitimisha, ningependa kuwashukuru viongozi wenzangu kwenye Bodi, watendaji, na wafanyakazi wote wa Kampuni kwa kuniunga mkono, kutoa ushauri na moyo wa kujitoa katika kipindi chote cha mwaka uliokuwa na changamoto kwetu sote. Wakati nafurahia fursa ya kazi huko Hispania, fursa hiyo isingewezekana bila kuwa na uzoefu wa miaka mitano nilioupata hapa Tanzania. Ninaondoka nikiwa balozi mzuri wa Tanzania.

Mwisho, ninamtakia mrithi wangu, Sitholizwe Mdlalose, kila la heri anapochukua nafasi hii yenye changamoto nyingi lakini na fursa pia. Nina uhakika kuwa, chini ya uongozi na maelekezo yake, Vodacom Tanzania ipo kwenye mikono salama kutimiza azma yake kwa jamii, kuiingiza Tanzania katika zama za kidigitali na kumuunganisha kila mmoja kwa kesho iliyo bora.



**Hisham Hendi**
Mkurugenzi Mkuu

19 Agosti 2021

# Kutekeleza azma yetu
# na wajibu kwa jamii

**Azma kuu ya Vodacom Tanzania ni 'kuunganisha jamii kwa kesho iliyo bora'. Tunapambana kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuunganisha watu na vitu kwenye intaneti, kusukuma mbele jitihada za maisha jumuishi kwa wote na kupunguza athari za mazingira.**

Tunaamini kuwa kuboresha huduma za mawasiliano ya sauti na data, na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kidigitali kwa wote, ni zana muhimu katika kuchochea mageuzi ya kiuchumi na kijamii na hivyo kutoa mchango mzuri kuelekea kufikiwa kwa malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa.

Tukiwa sehemu ya kampuni ya Vodafone na Kundi la makampuni la Vodacom, tumedhamiria kujikita katika maeneo matatu yanayolenga kuhamasisha mabadiliko chanya ya kijamii na kuchangia katika kufikiwa kwa malengo ya Umoja wa Mataifa ya Mandeleo Endelevu ('UN SDGs'):



Kuunda **Jamii ya kidigitali**


Kuchochea **maisha jumuishi kwa watu wote**

Kulinda **Sayari** yetu kwa kupunguza athari za mazingira

Kupitia shughuli zetu katika maeneo haya matatu, tunaleta athari chanya katika kufikiwa malengo nane yafuatayo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu ('UN SDGs')





# Jamii iliyounganishwa kidigitali

Ni muhimu kuongeza matumizi ya TEHAMA hapa Tanzania, ili kuleta mageuzi kutoka uchumi wa kilimo asilia kwenda uchumi wa kipato cha kati unaoendeshwa kwa uimara wa ujuzi na maendeleo ya viwanda vya kati. Sekta ya mawasiliano ya simu za kiganjani imechangia katika malengo ya maendeleo ya taifa kwa kuwezesha upatikanaji wa huduma jumuishi za kidigitali. Na pia sekta hii, bado ina nafasi ya kuchangia zaidi kwa kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu, kuongeza uzalishaji katika sekta mbalimbali za kibiashara, na kufungua fursa jumuishi za kiuchumi. Tunapunguza ombwe la kidigitali kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za kigiditali kupitia uwekezaji wetu katika kupanua miundombinu ya mawasiliano hasa katika maeneo ya vijijini, kuwezesha upatikanaji wa simu janja za bei nafuu, kuwezesha upatikanaji wa vifurushi vya gharama nafuu na vilevile upatikanaji wa mifumo ya kidigitali inayotatua changamoto za kijamii na kiuchumi.

## Kuwaunganisha watu wote

Licha ya changamoto za mazingira ya kibiashara kuathiri ufanisi wetu, hasa kutokana na athari za kuenea kwa UVIKO – 19, bado tumeendelea kuwekeza katika mtandao wetu na mifumo yake, kwa kutumia shilingi bilioni 122.4 ili kuongeza wigo wa upatikanaji na ubora wa mtandao wetu, pamoja na kuboresha mifumo ya TEHAMA. Uwekezaji wetu haukulenga katika maeneo ya mijini tu, bali pia katika viunga vyake, kwa lengo la kuwezesha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuhakikisha upatikanaji wa mawasiliano bora na nafuu. Katika mwaka huu, tumeongeza minara mipya 90 katika maeneo ya vijijini na kuboresha zaidi ya minara 330 kuwa ya teknolojia ya 3G na 4G. Miongoni mwa minara mipya vijijini , minara 43 imejengwa kwa ubia na serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, 'Universal Communication Service Access Fund –UCSAF'. Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka, tulikuwa na jumla ya minara 1 660 iliyopo katika maeneo ya vijijini, ikiwa ni pamoja na minara 260 iliyojengwa kwa ushirikiano na UCSAF katika kipindi cha miaka tisa iliyopita ya ushirikiano wetu imara. Ni azma yetu kuendelea kuwekeza katika mtandao wetu na kuchangia ongezeko la ubora wa maisha miongoni mwa Watanzania, kwa kupitia upatikanaji wa huduma bora ya mawasiliano kwa makundi yote ya kijamii hapa nchini.

Tumeendelea kuchochea matumizi ya simu janja, ili kuwezesha watu wengi zaidi kupata huduma za data na kidigitali, na mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka, 24.7% ya wateja wetu walikuwa ni watumiaji wa simu janja, ikiwa ni ongezeko la alama 2.6 za asilimia ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hata hivyo, kiwango hiki tulichofikia katika kuchochea ongezeko la watumiaji wa simu janja miongoni mwa wateja wetu, kiliathiriwa na athari za kuenea kwa janga la UVIKO – 19, ambalo linagusa katika mapato binafsi ya watu kutokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi, pia kutokana na athari za kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji duniani, uliosababisha kuchelewa kuwasili nchini kwa baadhi ya simu tulizozinunua.

Tumeendelea kutoa huduma nafuu za mawasiliano kwa kundi la wateja vijana, hususan wale walio katika taasisi za elimu ya juu kwa kutoa vifurushi maarufu vijulikanavyo kama "Bando za Chuo", ambavyo vinatumiwa na wateja zaidi ya 200 000 kila mwezi. Bando hizi zimeandaliwa maalum kutoa huduma kwa bei nafuu kwa ajili ya jumuiya ya wanafunzi.

Pia tumeendelea kuwezesha matumizi jumuishi ya kidigitali kwa wateja wote kupitia vifurushi vya gharama nafuu chini ya mwavuli wa 'Ya kwako tu', vikiwezeshwa na uwekezaji katika mifumo ya 'CVM' na 'machine learning'. Katika kipindi cha mwaka ulioisha, tuliendelea kuboresha vifurushi hivi kwa bando za ki-mkoa. Zaidi ya wateja milioni nne wenye viwango tofauti vya matumizi, wanatumia vifurushi vya 'Ya kwako tu' kila mwezi. Pia, katika lengo la kuwezesha wateja wengi zaidi kutumia data, tumeendelea kuwakopesha muda wa hewani na vifurushi kupitia huduma yetu ya 'Nipige Tafu', ambavyo huvilipia wanapopata uwezo wa kuongeza muda wa hewani.

## Majukwaa ya Kidigitali


Jukwaa letu la kilimo la M-Kulima linaloendeshwa kwa ushirikiano na kampuni ya Mezzanine, sasa limesajili wanachama ambao ni wakulima wadogo zaidi ya 100 000 na kuwaunganisha na huduma mbalimbali katika mnyororo wa thamani, unaowezesha upatikanaji wa taarifa, huduma na masoko kupitia SMS na 'App'. Wakulima hawa wamepatikana kupitia zaidi ya vyama 350 vya ushirika wa masoko ya kilimo ('AMCOS'). Kusajiliwa katika jukwaa hili kumewezesha malipo ya haraka na salama kwa wakulima kupitia M-Pesa, na zaidi ya shilingi bilioni 3.5 zimelipwa kwa wakulima hao kwa kipindi cha mwaka huu ulioisha. Wakulima walio katika orodha yetu hivi sasa, wanajishughulisha na mazao ya pamba, mahindi, maharage, alizeti, tumbaku, dengu, kahawa, choroko, zabibu na mazao ya wanyama, na wapo katika mikoa 15 hapa nchini Tanzania. Tutaendelea na juhudi za kuongeza idadi ya wakulima waliojisajiliwa katika makundi ya mazao yote yaliyopitishwa.

Kupitia jukwaa letu la elimu kwa mtandao,'Connected Education', karibu wanafunzi 700 wa shule za sekondari wameunganishwa kutumia 'maktaba' iliyothibitishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, wanahudhiria madarasa mtandao, wanafanya na kusahihishiwa mitihani na masuala mengine yanayohusiana na masomo. Kwa shule zinazoshiriki, hupatiwa 'simu kibao' (tablet) kama sehemu ya kifurushi. Tunaendelea kupanua wigo wa huduma hii.

Katika huduma za kunganisha 'vitu na internet, 'IoT', tunatoa huduma za kidigitali ambazo zinaongeza ufanisi wa biashara na kurahisisha matumizi. Tunatoa huduma nyingi ikiwa ni pamoja na huduma za 'mita janja' za umeme na za maji zilizounganishwa na mtandao, ambazo hazihitaji uwepo wa msomaji wa mita kuchukua rekodi hivyo kwa kiasi kikubwa zinaongeza ufanisi wa utoaji wa bili na kiwango cha ukusanyaji wa malipo. Pia tunatoa huduma zinazosaidia usimamizi na uangalizi wa mitambo na mashine ili kuboresha ufanisi katika matumizi, kutoa taarifa za kukumbusha uhitaji wa matengenezo na taarifa za kiusalama ikiwa ni pamoja na kubainisha eneo la kijiografia mashine ilipo wakati wowote. Katika eneo hili tunatoa huduma za mfumo wa kufuatilia vyombo vya moto na majokofu.

## Huduma jumuishi ya kifedha

Huduma yetu ya kifedha ya M-Pesa imeendelea kukua na kuwafikia watu wengi zaidi kuliko mtandao wa kampuni zote zinazotoa huduma za fedha kwa simu nchini Tanzania, tukiwa na wateja milioni 7.4 wanaofanya miamala kwa mwezi, ikichakata miamala zaidi ya bilioni moja, yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 60 kwa mwaka, na hivyo kuchangia kusukuma mbele ajenda ya kujumuisha watu wote kwenye mifumo rasmi ya kifedha. Kupitia pochi ya huduma za M-Pesa, M-Pawa na Halal Pesa, tunawapatia wateja wetu huduma ya 'akaunti ya akiba mkononi' . Huduma yetu ya akiba ya M-Koba inayoendeshwa kwa ushirikiano na benki ya Posta Tanzania, imelenga mahitaji ya vyama vya akiba na mikopo katika jamii. Tunawawezesha wateja wa M-Pesa kupata mikopo kupitia huduma ya M-Pawa, na vilevile kupitia huduma yetu ya Songesha iliyoanza hivi karibuni ambayo inakuwa kwa kasi kubwa. Katika mwaka wa fedha ulioisha, zaidi ya wateja milioni 3.5, karibu nusu ya wateja wote wa M-Pesa, walinufaika kwa mikopo ya Songesha.



# Huduma jumuishi kwa wote

Tumetekeleza mambo mbalimbali ambayo yanasaidia kuondoa umaskini na kuongeza usawa nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa huduma za elimu na afya kwa watu wengi zaidi, na kuunga mkono biashara mpya za kibunifu za ki-teknolojia. Mchango wa maeneo haya katika kuchochea huduma jumuishi kwa wote, ni mbali na mchango mkubwa wa huduma ya M-Pesa katika kufanikisha huduma jumuishi ya kifedha kama ilivyoelezwa kwa undani katika ukurasa uliopita.

## Upatikanaji wa huduma ya elimu kwa wote

Tunawawezesha wateja wetu kuweza kufikia vyanzo mbalimbali vya elimu bora kupitia intaneti ikiwa ni pamoja na maktaba mtandao, kwa kuhakikisha kuwa mtandao wetu wa data unapatikana wakati wote na katika kiwango cha juu cha ubora. Umuhimu wa huduma hii umethibitika hasa katika kipindi cha janga la UVIKO-19. Kupitia idara yetu ya huduma kwa jamii, 'Vodacom Foundation', tumewezesha wateja wetu kupata huduma za ki-elimu bure, ikiwa ni pamoja na kupitia jukwaa letu la 'Instant Schools' ambalo mwaka huu, lilihudumia zaidi ya wanufaika 101 000, nasi tukigharimia zaidi ya shilingi milioni 443 tangu tulipoanza huduma hii mwaka 2020.

Huduma ya M-Pesa ya 'VodaShule' inachangia katika lengo la kufikisha elimu kwa wote kwa kurahisisha uendeshaji wa taasisi za elimu, malipo pamoja na mawasiliano kati ya wazazi, walimu na wadau wengine wa shule husika. Huduma hii inasaidia kushughulikia changamoto zinazohusu uendeshaji wa shughuli za shule, usimamizi wa kumbukumbu, utunzaji wa historia za wanafunzi na namna bora ya ukusanyaji wa ada na hivyo kuongeza ufanisi wa kitaaluma. Jumla ya shule 14 zimejiandikisha katika huduma hii, zikiwa zimesajili wanafunzi zaidi ya 1800.

## Upatikanaji wa huduma ya afya kwa wote

Katika kupambana na janga la UVIKO-19, tumeunga mkono juhudi za serikali moja kwa moja na kwa njia mbadala, ikiwa ni pamoja na:

- Kuchangia jumla ya dola za Marekani milioni moja kwa ajili ya kununua na kusambaza vifaa vya kujikinga kwa ajili ya wafanyakazi wanaohudumia wagonjwa moja kwa moja.
- Kutoa huduma ya intaneti bure kwa vikosi maalum vya serikali, huduma ya bure ya data kwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Tiba, na huduma ya data isiyo na kikomo kwa wafanyakazi walio katika vituo maalum vya kupambana na UVIKO-19.
- Kuipatia Wizara ya Afya visambaza data na laini za simu kwa ajili ya data ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya intaneti bure kuharakisha mawasiliano na shughuli mbalimbali.
- Tumeondoa tozo kwenye tovuti rasmi za Serikali zenye taarifa za COVID-19.
- Kwa kushikiriana na Wizaya ya Afya tumewaelimisha wananchi kuhusu UVIKO-19 kupitia ujumbe mfupi wa maneno (SMS) kuhusu hatua za kiafya za kujikinga. Sambamba na hayo, tumetoa huduma ya kupiga simu namba 199 bila makato kwenda kwenye kituo cha ushauri wa afya kinachoendeshwa na wizara ya afya.

Mbali na kuwawezesha wateja wetu wanaohusika na sekta ya afya kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuwa na huduma bora na za uhakika kutoka mtandao wetu wa data, kupitia kitengo chetu cha huduma za kijamii, 'Vodacom Foundation', tumeshiriki katika programu mbalimbali za kuboresha sekta ya afya. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, tumetumia zaidi ya shilingi milioni 126 na kuwanufaisha walengwa zaidi ya milioni 1.3 katika eneo la huduma za afya. Taarifa zaidi za miradi ya afya tuliyoshiriki zinapatikana katika ripoti ya kitengo chetu cha huduma za kijamii, 'Vodacom Foundation' katika ukurasa wa 24.

## Kusaidia biashara zinazochipukia za kiteknlojia

Kupitia programu ya kuendeleza digitali , 'Digital Accelerator' iliyozinduliwa mwaka uliopita, tumeweza kusaidia na kutoa ushauri kwa makampuni 15 yaliyoteuliwa katika nyanja za teknolojia ya fedha, elimu, afya, mazingira na biashara mtandao. Lengo ni kuwasaidia vijana wa Kitanzania kubadili maono yao kuwa biashara zenye thamani ambazo zitatoa nafasi za ajira na kutatua changamoto za kijamii. Mawazo bora matatu yaliyopatikana katika mchakato huu, yapo katika hatua ya kuboreshwa na wakati huo huo maandalizi ya msimu wa pili unaoanzia Septemba 2021 yanaendelea.

## Kuchochea ujuzi wa kiteknolojia kwa wasichana

Tumeendelea na programu yetu ya '#codelikeagirl' inayowalenga wasichana wenye umri kati ya miaka 15 – 18 ikiwa na kusudio la kuwajenga na kuwaongezea wasichana ujuzi wa kiteknolojia katika kutengeneza programu za kidigitali zitakazochangia kutatua matatizo na kuleta maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Mwaka huu jumla ya wasichana 348 waliobainishwa kupitia shule za sekondari, walihudhuria mafunzo ya wiki moja kupata maarifa ya lugha ya kompyuta na utengenezaji wa programu ikiwa ni pamoja na 'HTML' na 'CSS', lugha ya kompyuta kwa ajili ya kuunda kurasa za tovuti. Washiriki wa program hii, wanakuwa ni sehemu ya kundi la vijana wenye vipaji vya teknolojia na wanaendelea kushirikishwa hata baada ya warsha kupita.





# Sayari

Tumedhamiria kuendelea kupunguza athari za mazingira zinazotokana na shughuli zetu za kibiashara kwa kuwekeza katika masuala ya tabianchi ikiwamo mitandao na mifumo inayotumia nishati kidogo, kupunguza taka katika mnyororo wetu wa thamani, kuongeza unyumbufu wa tabianchi kwa kupanda miti na kuhakikisha kuwa tunafuata kikamilifu masharti yote ya utunzaji wa mazingira.

## Ufanisi katika matumizi ya nishati na maji

Mwaka ulioisha, tuliendelea kuhakikisha tunaongeza ufanisi katika matumizi ya nishati na maji. Tunaendelea kuboresha vituo vyetu vya mifumo ya data, kubadili mifumo iliyopo kuwa mifumo ya 'cloud' ambayo ina ufanisi zaidi. Hata hivyo katika kipindi cha mpito ambacho bado kinaendelea, tunatumia pamoja baadhi ya mifumo ya zamani na mipya. Mwaka huu, matumizi ya nishati yaliongezeka 5.6% kufikia 16.9GWh, matumizi ya mafuta yaliongezeka 44.6% hadi lita milioni 1.6, na matumizi ya maji yalipungua 43% hadi kilolita 25.3. Ongezeko katika matumizi ya nishati linatokana na uwekezaji ulioongezeka katika mtandao, wakati ongezeko la matumizi ya mafuta kimsingi, linachochewa na matumizi ya jenereta kutegemea upatikanaji wa kutosha wa umeme wa gridi. Mwaka huu, matumizi ya maji yalipungua kutokana na wafanyakazi wetu kufanya kazi wakiwa nyumbani kama hatua ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UVIKO – 19.

## Kupunguza uzalishaji taka

Kampuni yetu ina historia ya muda mrefu ya kuwahamasisha wateja kubadili matumizi ya vocha za karatasi na kutumia vocha za kielektroniki kama vile M-Pesa, mashine za kutolea fedha (ATM) na Vodafasta, wanapokuwa wanaongeza salio la muda wa hewani. Msukumo huu umechangia kuzuia matumizi ya karatasi yanayokadiriwa kufikia tani 140 katika mwaka wa fedha ulioisha na hivyo kupunguza taka za karatasi na kulinda misitu ambayo ni chanzo kikuu cha malighafi za kutengenezea karatasi. Kwa utaratibu huu, tunakadiria kuwa tumeepuka matumizi ya takribani tani 602 za karatasi katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

Vilevile, tangu mwaka 2016, Vodacom imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha matumizi ya laini ndogo za simu zilizotengenezwa kwa malighafi ambazo ni rafiki kwa mazingira. Jitihada hizi zimepunguza matumizi ya plastiki na hivyo kuepusha taka za plastiki zenye uzito wa takribani tani 22 katika mwaka ulioisha. Kiasi hiki ni sawa na punguzo la tani 107 katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

## Utunzaji wa baioanuwai na tabianchi

Tumeendelea na miradi yetu ya kupanda miti katika juhudi za kuchangia ulinzi na utunzaji wa mazingira. Mwaka huu, kwa kushirikiana na washirika wetu, tuliendelea na utunzaji wa miti iliyopandwa mwaka uliopita katika programu yetu iliyojulikana kama 'Kijainisha Dodoma' iliyokusudia kuongeza ufahamu na kuhamasisha jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na baioanuwai. Pia tuliendesha miradi iliyolenga kulinda baioanuwai ya msitu wa Pugu Kazimzumbwi na hifadhi ya maliasili ya Vikindu katika mkoa wa Pwani. Maelezo zaidi kuhusu miradi hii yanapatikana katika ripoti ya 'Vodacom Foundation' katika ukurasa wa 25.

Jamii zimenufaika sio tu kutokana na ulinzi wa mazingira kupitia upandaji wa miti na elimu ya mazingira kupitia warsha zilizotolewa na maafisa ugani, bali pia kupitia ajira zilizotolewa kwa watu zaidi ya 100 wakati wa utekelezaji wa miradi, matunda yaliyovunwa katika miti mashuleni, na mafunzo kuhusu teknolojia rafiki kwa mazingira katika kukamua maji ya matunda ya zabibu na uvunaji bora wa mazao ya misitu.

| Viashiria vya uendelevu wa biashara | Kipimo | Mar-21 | Mar-20 | Mar-19 | Mar-18 | Mar-17 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya wafanyakazi | Idadi | **569** | 551 | 548 | 537 | 525 |
| Idadi ya wafanyakazi wanawake | Idadi | **203** | 204 | 200 | 212 | 209 |
| Wanawake kwenye kamati ya uongozi (EXCO) | % | **36** | 31 | 36 | 31 | 31 |
| Wanawake kwenye menejimenti (wakuu wa vitengo na EXCO) | % | **41** | 41 | 41 | 43 | 39 |
| Wafanyakazi wanawake | % | **36** | 37 | 36 | 39 | 40 |
| Jumla ya gharama zilizotumika kugharimia wafanyakazi | (Shi bilioni) | **61.6** | 57.7 | 59.4 | 55.3 | 55.5 |
| Jumla ya matumizi katika mafunzo | (Shi bilioni) | **0.7** | 1.0 | 0.7 | 0.8 | 0.4 |
| Vifo wakati wa kazi | Idadi | **Hakuna** | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna |
| 'Net Promoter Score' | Nafasi ya | **Kwanza** | Kwanza | Kwanza | Kwanza | Kwanza |
| Kiwango cha kuridhika cha ushirikishwaji wafanyakazi ('engagement index') | % | **86** | 86 | 85 | 85 | 82 |
| Wateja wote (siku 90) | Idadi (000) | **14,861** | 15,513 | 14,133 | 12,899 | 12,653 |
| Wateja wa M-Pesa (kwa mwezi) | Idadi (000) | **7,395** | 6,685 | 6,989 | 6,369 | 6,198 |
| Wateja wa data (kwa mwezi) | Idadi (000) | **7,695** | 7,687 | 7,892 | 7,345 | 6,463 |
| Gharama ya uwekezaji | (Shi bilioni) | **122.4** | 154.6 | 171.4 | 159.7 | 149.9 |
| Jumla ya kodi na makato yaliyolipwa serikalini | (Shi bilioni) | **429.7** | 434.8 | 391.5 | 379.1 | 352.3 |
| Jumla ya mikopo ya muda wa hewani kwa wateja | (Shi bilioni) | **43.3** | 38.2 | 34.6 | 53.1 | 113.4 |
| Jumla ya thamani ya miamala iliyopita kwenye M-Pesa | (Shi trilioni) | **69.2** | 58.9 | 50.0 | 43.1 | 31.5 |
| Wanufaika wa mikopo ya songesha | Idadi (000) | **3,541** | 2,001 | | | |
| Minara vijijini (UCSAF) | Idadi | **260** | 217 | 199 | 188 | 173 |
| Wateja wetu walioko vijijini[1] | % | **56** | 53 | 53 | 47 | 51 |
| Matumizi ya karatasi yaliyoepukwa kwa kutumia vocha za kielektroniki | Tani | **140** | 175 | 155 | 132 | 107 |
| Matumizi ya plastiki yaliyoepukwa kwa kutumia laini ndogo za simu | Tani | **22** | 30 | 31 | 25 | 29 |

1. Kwa kadiri ya taratibu za ndani za mipaka za Vodacom.

# Ufanisi wetu kifedha

| Taarifa za Jumla | 2021 | 2020 | % ya mabadiliko mwaka hadi mwaka |
|---|---|---|---|
| **Mapato ya huduma (Sh milioni)** | **966 014** | 1 024 916 | (5.7) |
| Ambapo | | | |
| Mapato ya huduma za simu kwa sauti | **311 506** | 373 005 | (16.5) |
| Mapato ya M-Pesa | **356 801** | 358 243 | (0.4) |
| Mapato ya data za simu | **186 865** | 180 840 | 3.3 |
| Mapato ya simu zinazoingia | **58 141** | 53 204 | 9.3 |
| Mapato ya ujumbe mfupi wa maneno | **31 877** | 42 413 | (24.8) |
| Jumla ya mapato | **974 391** | 1 032 667 | (5.6) |
| Mapato kabla ya riba, kodi na uchakavu (EBITDA) (Sh milioni) | **316 134** | 364 763 | (13.3) |
| Kiwango cha EBITDA (%) | **32.4** | 35.3 | (2.9)pp |
| Gharama za uwekezaji | **(122 447)** | (154 586) | 20.8 |
| Asilimia ya gharama ya uwekezaji[1] | **12.6** | 15.0 | (2.4)pp |
| Nafasi yetu kwa idadi ya wateja wa soko[2] | **Kwanza** | Kwanza | |
| Idadi ya wateja hai/amilifu[3] (maelfu) | **14 861** | 15 513 | (4.2) |
| Idadi ya wateja hai/amilifu wa M-Pesa kwa siku 30[4] | **7 395** | 6 685 | 10.6 |
| Wateja hai/amilifu wa data[5] (maelfu) | **7 695** | 7 687 | 0.1 |
| Dakika zilizotumika kwa mwezi[6] | **194** | 155 | 25.2 |
| Wastani wa kipato kutoka kwa mteja – ARPU (Shilingi kwa mwezi)[7] | **5 259** | 5 616 | (6.4) |
| Idadi ya wafanyakazi | **569** | 551 | 3.3 |
| Idadi ya minara | | | |
| 4G | **1 820** | 1 321 | 37.8 |
| 3G | **2 825** | 2 682 | 5.3 |
| 2G | **3 356** | 3 225 | 4.1 |
| Ulinganishi wa NPS[8] (nafasi kulingana na washindani) | **Kwanza** | Kwanza | |

1. Matumizi ya gharama za uwekezaji kama asilimia ya mapato.
2. Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 2021.
3. Walaji wanaotumia huduma wanatokana na jumla ya idadi ya watumiaji simu waliotumia huduma yoyote katika miezi mitatu iliyopita. Hii ni pamoja na wateja wanaolipa ada ya kila mwezi ambayo inawapa haki ya kutumia huduma husika hata kama kiuhalisia hawaitumii huduma hiyo na wale wateja ambao wanawasiliana nje ya mtandao
4. Wateja hai wa M-Pesa wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee waliotumia M-Pesa na kufanya miamala inayotozwa katika kipindi cha mwezi.
5. Wateja hai wa data wanatokana na idadi ya watumiaji wa kipekee wanaozalisha data inayotolewa bili katika mwezi. Pia ni pamoja na watumiaji katika mpango wa pamoja wa watumiaji au ambao wanatumia APN ya shirika na watumiaji ambao wametengewa bando ya data inayozalisha mapato katika mwezi. Mtumiaji anachukuliwa kuwa hai kama analipa ada ya mwezi kulingana na mkataba kwa huduma hii au ametumia huduma hii katika mwezi huo.
6. Dakika za matumizi kwa mwezi hukokotolewa kwa kugawanya jumla ya dakika zilizotumika kwa mwezi kwa wastani wa watumiaji wa dakika hizo katika kipindi hichoJ. Jumla dakika zilizotumika kwa mwaka wa fedha 2020 zilirekebishwa, hivyo kuna mabadiliko ikilinganishwa na dakika zilizoripitiwa katika ripoti ya mwaka uliotangulia.
7. ARPU inakokotolewa kwa kugawa wastani wa mapato ya huduma kwa mwezi kwa wastani wa jumla ya wateja kwa mwezi katika kipindi hicho.
8. Net promoter score ('NPS') ni kipimo kuanzia -100 hadi 100 ambacho kinaonesha utayari wa wateja kupendekeza bidhaa au huduma za mtoa huduma kwa watu wengine. Inatumika kama kigezo cha kupima hali ya kuridhika kwa wateja na bidhaa au huduma za mtoa huduma imani ya wateja kwa chapa hiyo. Kwa kila mtoa huduma, majibu yanakusanywa kutoka kwa wateja ambao wanatumia bidhaa au huduma zake kama njia kuu au mbadala ya mawasiliano ya simu ('mtumiaji mkuu' au 'mtumiaji mbadala'). Majibu kutoka kwa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala yanalinganishwa/pimwa kwa uwiano asilia wa watumiaji wakuu na watumiaji mbadala wa mtoa huduma huyo ili kukokotoa NPS.

## Mapato

### Mapato

**Mapato ya huduma** yalipungua kwa 5.7% hadi shilingi bilioni 966.0 kutokana na athari za shinikizo la ushindani wa bei, kudorora kwa shughuli za kiuchumi kutokana na janga la UVIKO-19 na kufungiwa huduma kwa wateja milioni 2.9 katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha uliopita kutoka na laini zao za simu kutokamilisha usajili kwa alama za vidole. Utekelezaji mzuri wa mikakati yetu ya kibiashara ulisababisha mabadiliko chanya katika nusu ya pili ya mwaka, ambapo katika robo ya nne ya mwaka, mapato ya huduma yaliongezeka kwa 6.3%, ukuaji huo ukichagizwa hasa na mapato ya M-Pesa na data.

**Mapato ya huduma za simu kwa sauti** yalipungua kwa 16.5% hadi shilingi bilioni 311.5, kutokana hasa na shinikizo la ushindani wa bei, likichochewa na kushushwa kwa gharama inayotozwa kwa dakika kwa simu zinazotoka katika mitandao mingine ya ndani, likisababisha mporomoko wa 21% katika wastani wa bei kwa dakika. Mapato ya huduma ya simu kwa sauti pia yaliathiriwa na kudorora kwa shughuli za kiuchumi kutokana na janga la UVIKO-19 na kufungiwa huduma kwa wateja milioni 2.9 katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha uliopita. Jitihada zetu za kuwawezesha wateja kupata bidhaa zinazokidhi mahitaji maalum ya makundi mbalimbali (segmented offers) kwa kutumia

teknolojia ya 'CVM', na vilevile jitihada za kuhamasisha ongezeko la idadi ya siku ambazo wateja wanatumia mtandao wetu, zilisaidia kudhibiti kupungua kwa mapato ya huduma za simu kwa sauti katika nusu ya pili ya mwaka hadi 13.2% kutoka 19.4% ilivyokuwa katika nusu ya kwanza ya mwaka.

**Mapato ya M-Pesa** yalipungua kwa 0.4% hadi shilingi bilioni 356.8, kimsingi kutokana na wateja kupunguza matumizi kulikosababishwa na athari za UVIKO – 19, kufungiwa huduma kwa laini 800 000 katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha uliopita na vilevile kusitishwa kwa utozaji wa ada ya utunzaji wa akaunti zisizotumika, kwa mujibu wa matakwa ya kanuni za kumlinda mteja wa huduma za fedha[1].

Pasingekuwapo na usitishwaji wa kutoza ada hiyo, mapato ya M-Pesa yangeongezeka kwa 1.3% mwaka huu na 11.3% katika robo ya nne ya mwaka, ukuaji huo ukichochewa na ongezeko la uwanda wa huduma zetu na mapokeo chanya ya huduma zetu. Katika mwaka huu, idadi ya wateja iliongezeka kwa jumla ya wateja 710 000 hadi kufikia wateja milioni 7.4, sawa na 49.8% ya wateja wote. Tunaendelea kuongoza soko kwa kuwa na 40.7%[2] ya idadi ya wateja wote, ongezeko la pointi 1.4 za asilimia ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Bidhaa yetu ya mkopo - 'Songesha' imeendelea kututofautisha na washindani, na imeendelea vizuri kuwawezesha wateja na mawakala kukamilisha miamala. Pamekuwa na ukuaji unaoridhisha wa utumiaji na mapato ya Songesha katika kipindi cha mwaka, huku huduma hii ikichochea ujumuishi wa huduma ya fedha. Huduma yetu inayopanuka ya kutuma na kupokea fedha kutoka nje ya nchi imeendelea kuchukua nafasi muhimu katika kuunga mkono ujumuishi wa huduma ya fedha, huku fedha zilizopokelwa kutoka nje zikiongezeka kwa kiasi kikubwa kufikia zaidi ya shilingi bilioni 500 na zile zilizotumwa kwenda nje ya nchi zikifikia zaidi ya shilingi bilioni 70, ambalo ni ongezeko la zaidi ya 35%. Ushirikiano wetu na kampuni zaidi ya 900 zinazotumia huduma ya M-Pesa kutuma na kupokea miamala kwenda na kutoka kwa wateja, umeendelea kuwezesha ufanyaji wa miamala kwa haraka, urahisi na usalama, kukiwa na miamala yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 4.0 iliyofanyika mwaka huu.

**Mapato ya data za simu** yaliongezeka kwa 3.3% hadi shilingi bilioni 186.9, licha ya shinikizo kubwa la ushindani wa bei lililosababisha bei ya wastani kwa megabaiti kushuka kwa 30%, wakati matumizi ya data kwa mteja yaliongezeka kwa 47.0 % kufikia 1.4GB kwa mwezi. Mapato ya data yaliathiriwa pia na kufungiwa huduma kwa wateja 600 000 katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha uliopita. Katika robo ya nne ya mwaka, mapato ya data yaliongezeka kwa 18.7%. Huduma za data zinabaki kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa biashara na mhimili wa azma yetu ya kuunganisha kwa kesho iliyo bora. Ongezeko la wastani wa matumizi kwa mteja (ARPU) katika data tulilolipata kwenye nusu ya pili ya mwaka, linaakisi utekelezaji mzuri wa mikakati ya kibiashara katika kuchochea matumizi ya data. Tunaendelea kuchochea matumizi ya simu janja za gharama nafuu kupitia ubia wetu na makampuni ya teknolojia duniani, pamoja na kuwapa wateja namna bora zinazo rahisisha mikopo ya simu. Juhudi hizi zimewezesha ongezeko la watumiaji wetu wa simu janja kwa 7.0% hadi milioni 3.7, sawa na 24.7% ya wateja wote, ongezeko la pointi 2.6 za asilimia ukilinganisha na mwaka uliotangulia.

**Mapato ya simu zinazoingia** yaliongezeka kwa 9.3% hadi shilingi bilioni 58.1, kutokana na ongezeko kubwa la dakika za simu zinazoingia kutokana na watoa huduma kuendela kutoa vifurushi vyenye dakika nyingi zaidi hasa baada ya kushushwa kwa gharama inayotozwa kwa dakika, kwa simu zinazotoka katika mitandao mingine ya ndani. Ongezeko hili limesawazishwa kwa kiasi na punguzo la 50% ya gharama kwa dakika inayotozwa kwa simu zinazotoka katika mitandao mingine ya ndani lililofanyika mwezi Januari 2020 na punguzo lingine la 50% mnamo Januari 2021, kulingana na utaratibu uliowekwa na msimamizi wa sekta ya mawasiliano.

**Mapato ya ujumbe mfupi** yalipungua kwa 24.8% hadi shilingi bilioni 31.9, kimsingi kutokana na athari za shinikizo kubwa la ushindani wa bei, pamoja na wateja kupunguza matumizi kutokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi kutokana na janga la UVIKO-19 na kufungiwa huduma kwa wateja milioni 2.9 katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha uliopita.

## Gharama[3]

Licha ya gharama za moja kwa moja za uzalishaji kupungua kwa 6.3%, kutokana na kupungua kwa mapato, mashinikizo ya kiushindani yaliathiri gharama zinalizolipwa kwa huduma ya uwakala na gharama za simu zilizopigwa kwenda mitandao mingine. Mafanikio ya programu yetu ya kupunguza matumizi, 'Fit for growth' yalififishwa na ongezeko la 17.0% la gharama za utangazaji zilizotokana na ongezeko la zaidi ya 100% katika tozo za manispaa kwenye mabango ya nje kwa mujibu wa sheria ya fedha ya serikali za mitaa ya mwaka 2020 ; ongezeko la 6.8% katika gharama za mishahara kutokana na gharama ya mara moja ya kupunguza wafanyakazi, na pia ongezeko la 4.9% la gharama za uendeshaji mtandao kutokana na ongezeko la ukubwa wa mtandao kufuatia uwekezaji unaoendelea na pia marekebisho ya mfumuko wa bei katika mikataba iliyopo ya huduma. Gharama zetu kwa ujumla, zilipungua 1.1% hadi shilingi bilioni 660.8.

## EBITDA

Mapato kabla ya riba, kodi na gharama za uchakavu, yalipungua 13.3% hadi shilingi bilioni 316.1 kutokana na kupungua kwa mapato ya huduma yakisawazishwa kwa kiasi na kupungua kwa gharama.

## Gharama za uwekezaji

Katika mwaka ulioisha wa fedha, tuliwekeza kiasi cha shilingi bilioni 122.5 ikiwa ni sawa na asilimia 12.6% ya mapato yetu.  Uwekezaji ulielekezwa katika kuimarisha mtandao wetu wa data kwa kupanua mtandao wa 4G ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za data; na pia katika kuimarisha miundombinu ya TEHAMA. Tulijenga minara mipya 499 ya 4G ikiunganishwa kwa mkongo wa mawasiliano ili kuhakikisha kwamba wateja wetu wanapata huduma nzuri. Kiwango cha uwiano cha gharama za uwekezaji kwa mapato, kimepungua kwa pointi 2.4 za asilimia hadi 12.6% kutokana na changamoto za mazingira ya kibiashara. Malengo yetu ni kuendelea kuboresha mtandao wetu ili kuchochea ongezeko la matumizi ya data na kutoa huduma zenye ubora wa kipekee kwa wateja wetu. Tunatarajia kiwango cha gharama za uwekezaji kurejea katika uwiano kwa mapato uliokuwepo kabla ya janga la UVIKO –19, iwapo mageuzi katika sekta ya mawasiliano yataonesha mwekeleo wa ongezeko la mapato.

1. Tanzania (Financial Consumer Protection) Regulations, 2019.
2. Kwa mujibu wa takwimu za mawasiliano za robo mwaka za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania za Machi 2021.
3. Gharama mbali na gharama za uchakavu.

# Muhtasari wa taarifa za pamoja za faida na hasara na mapato mengine

| Shilingi (milioni) | **Zimekaguliwa 2021** | Zimekaguliwa 2020 |
|---|---|---|
| Mapato | **974 391** | 1 032 667 |
| Gharama za moja kwa moja | **(301 533)** | (321 693) |
| Gharama za wafanyakazi | **(61 579)** | (57 671) |
| Gharama za kujitangaza | **(35 775)** | (30 571) |
| Gharama nyingine za uendeshaji | **(260 064)** | (247 885) |
| Gharama za Uchakavu | **(264 039)** | (268 762) |
| Gharama za madeni chechefu | **(1 887)** | (10 086) |
| **Faida ya uendeshaji** | **49 514** | 95 999 |
| Mapato ya fedha | **38,418** | 50 465 |
| Gharama za kifedha | **(85 232)** | (86 470) |
| Mapato kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha za kigeni | **3 627** | 356 |
| **Faida kabla ya kodi** | **6 327** | 60 350 |
| Gharama za kodi ya mapato | **(36 433)** | (14 588) |
| **Faida kwa mwaka** | **(30 106)** | 45 762 |
| Mapato mengine | **–** | – |
| **Jumla ya mapato halisi kwa mwaka wa mapato, baada ya kutoa kodi[1]** | **(30 106)** | 45 762 |
| Mapato ya msingi na mchanganyiko kwa kwa kila hisa (TZS) | **(13.44)** | 20.43 |

1. Mapato yote yanawahusu wamiliki wa Kampuni mama kwa kuwa hakuna wamiliki walio na umiliki mdogo (non-controlling interest) kwenye kampuni tanzu.

Mapato yamepungua kwa 5.6% hadi shilingi bilioni 974.4, ikichochewa na kupungua kwa mapato ya matumizi ya wateja kutokana na wateja kupungua kwa 4.2% ikichangiwa na kufungiwa huduma kwa laini milioni 2.9 zisizokamilisha usajili wa alama za vidole, na vilevile kupungua 6.4% kwa wastani wa matumizi kwa mteja (ARPU) kutokana na shinikizo kubwa la ushindani wa bei na athari za janga la UVIKO-19.

Gharama ziliongezeka kwa kiasi cha 0.2% hadi shilingi bilioni 659.0 kutokana na ongezeko la gharama za kamisheni na gharama za simu zilizopigwa kwenda mitandao mingine kutokana na shinikizo la ushindani wa bei, ongezeko la gharama za utangazaji zilizotokana na ongezeko la zaidi ya 100% katika tozo za manispaa kwenye mabango ya nje kwa mujibu wa sheria ya fedha ya serikali za mitaa ya mwaka 2020, ongezeko la gharama za mishahara kutokana na gharama ya mara moja ya kupunguza wafanyakazi, na pia gharama za uendeshaji mtandao kutokana na ongezeko la ukubwa wa mtandao kufuatia uwekezaji unaoendelea na pia marekebisho ya mfumuko wa bei katika mikataba iliyopo ya huduma. Ongezeko la gharama lilisawazishwa kwa kiasi na mafanikio ya programu yetu ya kupunguza matumizi, 'Fit for growth'.

Gharama za uchakavu zilipungua kwa 1.8%, ikiwa ni matokeo ya mapitio ya umri na muda ambapo mali (assets) zinaweza kuendelea kutumika kwa ufanisi, upungufu ukifidiwa kwa kiasi na ongezeko kutokana na uwekezaji mpya katika mali. Mapitio haya ya mali yalifanyika kulingana na taratibu za kampuni.

Gharama za madeni chechefu katika mwaka huu zinahusisha kiasi kilichotengwa kwa ajili ya hasara tarajiwa za madeni chechefu tunayowadai wateja na washirika wetu kibiashara. Madeni ya biashara yanaripotiwa kiasi halisi kikipunguzwa na kiasi cha hasara tarajiwa cha madeni hayo kwa mujibu wa tathmini ya menejimenti juu ya uwezo wa wadeni kurejesha mikopo hiyo. Madeni yote hupimwa ili kutathmini uwezekano wake wa kutokulipwa. Gharama kutokana na madeni chechefu zimepungua kutokana na kuimarika kwa makusanyo katika huduma ya mikopo ya muda wa maongezi (Nipige tafu).

Mapato ya fedha yamepungua kwa 23.9% kutokana na viwango vidogo vya riba katika fedha taslimu na uwekezaji katika hawala za serikali, na vilevile kupungua kwa uwekezaji katika hawala za serikali kufuatia kulipwa kwa gawio maalum la shilingi bilioni 400.

Ongezeko la mapato ni matokeo ya faida tuliyoipata kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha za kigeni katika akiba ya fedha hizo.

Gharama ya kodi ya shilingi bilioni 36.4 imeongezeka kwa 149.7% ukilinganisha na kodi ya mwaka uliotangulia (2020: shilingi bilioni 14.6) hasa kutokana na gharama za kodi za kampuni ya M-Pesa ambayo ni kampuni inayojitegemea katika taratibu za ulipaji kodi, na pia kutotambuliwa kwa malimbikizo ya unafuu wa kodi (Deferred tax asset) kutokana na hasara kwenye biashara ya mawasiliano ('GSM'). Kuanzia tarehe 1 Aprili 2020, biashara ya M-Pesa ilianza kuendeshwa kama kampuni inayojitegemea kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya taifa ya mfumo wa malipo . Gharama ya kodi pia imeongezeka kutokana na kulipa kodi zinazohusiana na kipindi cha kati ya mwaka 2006 hadi 2009 kufuatia maamuzi ya mahakama ya rufaa juu ya kesi tulizozifungua kupinga kodi hizo.

# Muhtasari wa taarifa za pamoja za hali ya kifedha

| Shilingi (milioni) | Zimekaguliwa 2021 | Zimekaguliwa 2020 |
|---|---|---|
| **Mali** | | |
| **Mali za kudumu** | **1 219 874** | 1 298 663 |
| Mali na mitambo | **1 041 226** | 1 123 945 |
| Mali zisizoshikika | **70 593** | 78 510 |
| Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia | **46 559** | 54 888 |
| Thamani isiyoshikika ya uwekezaji | **1 639** | 1 639 |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa | **39 772** | 23 755 |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine | **18 696** | 15 926 |
| Kodi iliyoahirishwa | **1 389** | – |
| **Mali za muda mfupi** | **836 067** | 1 097 226 |
| Malipo ya 'Haki ya matumizi' kabla ya kutumia | **13 188** | 13 657 |
| Mali ghalani | **4 179** | 2 004 |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipwa | **125 534** | 100 815 |
| Kodi ya mapato inayotarajiwa kurejeshwa | **4 726** | 4 723 |
| Rasilimali za kifedha | **444 183** | 337 556 |
| Uwekezaji wa muda mfupi | **–** | 164 643 |
| Fedha taslimu na mbadala wa fedha | **244 257** | 473 828 |
| **Jumla ya mali** | **2 055 941** | 2 395 889 |
| **Mtaji na Madeni** | | |
| **Mtaji na Madeni** | **797 587** | 1 255 152 |
| Mtaji wa hisa | **112 000** | 112 000 |
| Malipo ziada kwenye hisa | **442 435** | 442 435 |
| Mchango wa mtaji | **27 698** | 27 698 |
| Ziada ya faida iliyotunzwa | **215 454** | 673 019 |
| **Madeni ya muda mrefu** | **466 184** | 513 575 |
| Madeni ya pango | **461 627** | 494 354 |
| Ruzuku za serikali | **235** | 1 616 |
| Kodi iliyoahirishwa | **–** | 13 800 |
| Madeni ya kibiashara na madeni mengine ya kulipa | **163** | 186 |
| Tahadhari ya madeni | **4 159** | 3 619 |
| **Madeni ya muda mfupi** | **792 170** | 627 162 |
| Madeni ya pango | **73 052** | 50 869 |
| Madeni ya biashara na mengine ya kulipa | **688 743** | 552 167 |
| Riba inayodaiwa na wateja wa M-Pesa | **8 593** | 11 992 |
| Ruzuku za serikali | **1 383** | 2 310 |
| Tahadhari ya madeni | **20 399** | 9 824 |
| **Jumla ya madeni** | **1 258 354** | 1 140 737 |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **2 055 941** | 2 395 889 |

Kupungua kwa mali na mitambo kumetokana na gharama za uchakavu zikifidiwa kwa kiasi na uwekezaji uliofanyika mwaka huu.

Ongezeko limechochewa na malipo ya kodi ya utangulizi yaliyolipwa dhidi ya hati za madai ya kodi zilizopokelewa mwaka huu.

Hii ni kodi iliyoahirishwa ya kampuni ya M-Pesa.

Ongezeko linatokana na amana za wateja binafsi wa M-Pesa pamoja na wateja wengine wa kibiashara.

Uwekezaji umepungua baada ya kukomaa kwa hawala za serikali ambapo fedha iliyopatikana haikuwekezwa tena mpaka kufikia tarehe ya kutoa taarifa.

Akiba ya fedha taslimu imepungua kutokana na kulipa wanahisa jumla ya shilingi bilioni 427 kupitia gawio la mwaka na gawio maalum.

Ziada ya faida imepungua kutokana na kulipa wanahisa jumla ya shilingi bilioni 427 kupitia gawio la mwaka na gawio maalum.

Madeni yamepungua kutokana na kulipa madeni ya pango yaliyoiva kwenye mikataba ya 'haki ya matumizi'.

Kodi iliyoahirishwa imepungua kutokana na kutorekodiwa kwa 'kodi ahirishwa' kufuatia kupata hasara kulingana na taratibu za kikodi.

Ongezeko linatokana na kuhamishwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 28.9 kutoka kundi la 'madeni ya pango' ya muda mrefu kwenda madeni ya muda mfupi, ongezeko likipunguzwa kwa kiasi na malipo ya shilingi bilioni 6.0 kwa madeni yaliyoiva.

Ongezeko limechangiwa na ongezeko la amana za M-Pesa la shilingi bilioni 110 kutoka kwa wateja, mawakala na biashara likiakisi kukua kwa biashara ya M-Pesa, na vilevile ongezeko la gharama za masoko na ya kukodisha mifumo ya mawasiliano.

# Muhtasari wa taarifa za pamoja za mzunguko wa fedha

| Shilingi (milioni) | Zimekaguliwa 2021 | Zimekaguliwa 2020 |
|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji** | | |
| Fedha zilizozalishwa kutokana na uendeshaji | **427 135** | 344 244 |
| Malipo ya kodi ya mapato | **(67 642)** | (53 181) |
| Mzunguko ghafi wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji | **359 493** | 291 063 |
| **Mzunguko wa fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji** | | |
| Nyongeza katika mali na mitambo, na mali zisizoshikika | **(112 850)** | (159 350) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali na mitambo | **17** | 719 |
| Ruzuku za serikali zilizopokelewa | **400** | 2 838 |
| Marejesho ya uwekezaji wa muda mfupi | **164 643** | 54 933 |
| Mapato ya fedha yaliyopokelewa | **17 625** | 31 118 |
| (Kuongezeka) / Kupungua kwa fedha zilizowekwa kwenye akiba za matumizi maalum | **(106 627)** | 40 463 |
| Riba kutoka amana za M-Pesa | **20 793** | 19 347 |
| Mzunguko halisi wa fedha katika shughuli za uwekezaji | **(15 999)** | (9 932) |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na shughuli za ugharimiaji** | | |
| Gawio tulilolipa | **(427 093)** | (54 459) |
| Riba ya madeni ya pango iliyolipwa | **(64 040)** | (67 034) |
| Malipo ya madeni ya pango – mtaji | **(61 395)** | (43 455) |
| Riba iliyolipwa kwa wateja wa M-Pesa | **(24 165)** | (39 013) |
| **Mzunguko halisi wa fedha zilizotumiwa katika shughuli za ugharimiaji** | **(576 693)** | (203 961) |
| Ongezeko/(punguzo) ghafi katika fedha na fedha mbadala | **(233 199)** | 77 170 |
| Fedha taslimu na fedha mbadala tarehe 1 Aprili | **473 828** | 396 622 |
| Athari za mabadiliko ya viwango vya kubadili fedha katika fedha taslimu na fedha mbadala zilizo katika fedha za kigeni | **3 628** | 36 |
| **Fedha taslimu na fedha mbadala kufika tarehe 31 Machi** | **244 257** | 473 828 |

Ongezeko la kodi ya mapato limetokana na malipo zaidi ya kodi ya utangulizi, yaliyofanyika kupinga makadirio ya kodi kwenye mashauri yanayoendelea, na pia ongezeko la kodi iliyolipwa na kampuni ya M-Pesa.

Ongezeko limetokana na hawala za serikali zilizoiva katika kipindi cha mwaka huu.

Ongezeko limechangiwa hasa na ongezeko la amana za M-Pesa la shilingi bilioni 110 kutoka kwa wateja, mawakala na biashara likiakisi kukua kwa biashara ya M-Pesa.

Ongezeko la gawio lililolipwa limetokana na malipo ya gawio ghafi ya jumla ya shilingi bilioni 27.5 kulingana na sera ya Kampuni, na vilevile gawio maalum la jumla ya shilingi bilioni 400 katika mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2020 zilizolipwa kutoka katika ziada ya faida iliyotunzwa.



# Vodacom Tanzania Foundation



**Vodacom Tanzania Foundation ni kitengo kinachosimamia uwekezaji katika jamii kwa niaba ya Kundi la makampuni. Ikiongozwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa 2030, Dira ya Tanzania 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka 5, dira ya Vodacom Foundation ni kutumia fursa za kiteknolojia ilizonazo Vodacom na wabia wake kwa kutekeleza miradi katika elimu, afya na ulinzi wa mazingira ili kuboresha maisha ya Watanzania ambao hawajafikiwa na huduma hizo. Utoaji wa huduma hizi ni nguzo za uwekezaji wa muda mrefu kuleta mabadiliko ya kijamii kwa kutoa mchango wake kwenye elimu ya afya, vifo vya watoto wachanga na namna ya kuvizuia na mchango katika kukabili majanga ili kuwezesha ustawi endelevu wa miji.**

Tangu mwaka 2004, Foundation kwa kushirikiana na Kampuni mama 'Vodafone Foundation', imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 16.2 na kusaidia maisha ya mamilioni ya watu nchini Tanzania. Mchango wa Vodafone Foundation kwa kiasi kikubwa umelenga katika afya ya kina mama.



## Ufanisi wetu 2021

**Afya – Lengo la 3 la Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu**
(Afya Njema na Ustawi)

Katika miaka miwili iliyopita, **Vodacom Foundation** imetumia zaidi ya

**Shilingi milioni 126**

katika programu zinazohusiana na afya na kuwanufaisha zaidi ya watu milioni 1.3.

Programu hizo ni pamoja na:

- Programu zinazohusu kupunguza vifo vya watoto wachanga na kuhimili majanga, na kutengeneza vitengo vya kulea watoto wachanga pamoja na kuzipatia hospitali na vituo vya afya vifaa tiba. Zaidi ya watu 607 wamenufaika na miradi iliyoendeshwa katika kituo cha afya cha Muriet, hospitali ya St. Mary's Kibara na kituo cha afya Inyonga B. Programu hii ilianza mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2020 katika kituo cha afya cha Muriet, na kuendelezwa katika mwaka huu huku ikijumuisha vituo vingine viwili vya afya.
- Programu ya usafiri wa dharura ya "M-Mama" kwa wanawake wajawazito huko Shinyanga na Sengerema, imetoa huduma kwa watu 11 239. Programu hii iliendeshwa kwa kushirikiana na Vodafone Foundation, ambapo huduma ya M-Pesa ilitumika kulipia huduma za teksi zilizotumika kama magari ya wagonjwa katika juhudi za kuzuia na kupunguza vifo vya kina mama na watoto.
- Tumeendelea na programu ya afya ya 'Mimba yenye afya, Mtoto mwenye afya' (Wazazi Nipendeni) kwa kutoa huduma ya bure ya ujumbe mfupi wa maneno kuhusu tiba, kwa kuwawezesha wanawake wajawazito kujisajili na kupokea kupitia simu zao za kiganjani ujumbe mfupi unaosambaza taarifa za afya kuhusu huduma kwa watoto wachanga, kukumbusha mahudhurio ya kliniki, kuzuia malaria, kifua kikuu na VVU/UKIMWI, uzazi wa mpango na lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Zaidi ya wateja wa Vodacom milioni 1.3 wamejisajili katika huduma hii.

## Elimu – Lengo la 4 la Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (Elimu bora)

4 ELIMU YA KIWANGO CHA JUU

Zaidi ya

**Shilingi milioni 443**

zimetumika katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Tumeendelea kuunga mkono jitihada mbalimbali za kutoa elimu kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya kiserikali na asasi zisizo za kiserikali. Kupitia mradi wetu wa 'Instant Schools', uliolenga jamii za vijijini zilizo katika mazingira magumu, tumetoa huduma za kupata elimu bure kupitia mtandao na kuwanufaisha zaidi ya walengwa 101 800 kwa mwaka huu, tukiwa tumetumia jumla ya shilingi milioni 443 katika miaka miwili iliyopita. Hii ni huduma ya kimtandao inayopatikana kupitia simu janja au kompyuta, ambapo wateja wa Vodacom wanajisajili na kupata maarifa bure katika masomo mbalimbali. Huduma zetu za elimu zimechukua nafasi muhimu katika kuhakikisha wanafunzi wanaendelea kujifunza licha ya mlipuko wa janga la UVIKO-19 mwaka 2020.

## Ulinzi wa mazingira – Lengo la 13 la Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (Kudhibiti mabadiliko ya tabianchi)

13 KUSHUGHULIKIA MAZINGIRA

Jumla ya zaidi ya

**Shilingi milioni 306**

zimetumika katika mradi huu tangu ulivyoanza mwaka uliopita.

Kwa ubia na shirika la World Wide Fund for Nature (WWF), na kwa kushirikiana na ofisi ya Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha wa 2020 Foundation ilianza utekelezaji wa pamoja wa programu ya kulifanya jiji la Dodoma kuwa la kijani, kwa kupanda miti zaidi ya 70,000 kwa kuwashirikisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwenye mradi huu. Mwaka huu, tumepanda miti zaidi ya 500 ili kurudishia miti iliyokufa kama sehemu ya kuendeleza mradi huu. Jumla ya zaidi ya shilingi milioni 306 zimetumika katika mradi huu tangu ulipoanzishwa mwaka jana.

Katika mwaka huu wa fedha, tumeshirikiana World Wide Fund for Nature (WWF) kuzindua programu inayolenga kuhuisha mabaki ya misitu ya pwani ya Vikindu na Pugu-Kazimzumbwi kupitia uhifadhi na uhamasishaji wa utalii endelevu. Katika kipindi hiki, tumeshiriki katika jitihada mbalimbali za kuwaelimisha wananchi wa maeneo ya jirani kuhusu uhifadhi wa mazingira. Jitihada hizi zilijumuisha ushiriki katika matamasha ya vijana ambapo wastani wa vijana 20 000 walifikiwa, na kuendesha warsha kuhusu matumizi ya teknolojia endelevu za nishati kwa ajili ya kuzalisha kipato na kwa matumizi ya majumbani, na kusambaza nakala za ujumbe mfupi zaidi ya milioni 2 za maarifa kuhusu hifadhi ya mazingira kwa wateja wa Vodacom.

Pia tumeandaa maudhui ya kimtandao kuhusu hifadhi ya mazingira ambayo yanatangazwa katika jukwaa la mafunzo kimtandao linalojulikana kama e-Fahamu. Mradi huu unaendeshwa kwa ushirikiano wa karibu na serikali kupitia ofisi za wakuu wa wilaya za Kisarawe na Mkuranga pamoja na vikundi vya kijamii ikiwa ni pamoja na mama lishe, vijana na waongoza watalii.

Programu zetu zinazohusiana na mazingira kwa pamoja zimewanufaisha zaidi ya watu 712, zimejenga fursa za ajira zaidi ya 115, na kuwafikia watu zaidi ya 20 000 zikiwa na ajenda ya ulinzi wa mazingira.

## Mtazamo wetu kimkakati


**Katika miaka miwili ijayo, Foundation italenga katika maeneo yafuatayo:**

- Elimu kwa wote: Tutahamasisha utoaji elimu kwa wote na kwa usawa kwa kuongeza upatikanaji wa teknolojia na intaneti katika shule za serikali nchini kote, kwa lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata huduma ya kujifunza kwa TEHAMA katika jamii za wenye kipato kidogo katika maeneo ya vijijini na mijini.
- Mabadiliko ya tabianchi na baioanuwai: Tutafanya jitihada za kuzungumzia mabadiliko ya tabianchi na kupotea kwa baioanuwai nchini Tanzania, tukilenga kuelimisha jamii kuhusu kutunza mazingira, kuhimiza mbinu bora za kilimo na kupanda miti, kuwezesha upatikanaji wa nishati salama na kusaidia katika uendeshaji wa warsha kuhusu ajenda za mabadiliko ya tabianchi.
- Kupunguza vifo vya watoto wachanga: Tutasaidia utoaji wa vifaatiba ili kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati(njiti), kujenga uwezo na ufahamu kwa wafanyakazi wa sekta ya afya wasio na ujuzi wa kutosha na kuchochea ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kuhusu kupunguza kiwango cha vifo vya watoto wachanga.
- Usimamizi wa misaada katika majanga: Tutahamasisha matumizi ya teknolojia ya simu na TEHAMA kama zana saidizi wakati wa majanga, kutoa visambaza data (routers) na laini za simu kwa watumiaji waliondaliwa kuwezesha mawasiliano ili kukabiliana na majanga, na kugharamia warsha na semina kuhusu usimamizi wa majanga.

# Viongozi wetu

**Tuna Bodi yenye wakurugenzi 12, wengi wao ni wakurugenzi wasio watendaji. Mwenyekiti wetu ni mkurugenzi huru.**

## Muundo wa Bodi







**1 Thomas B Mihayo** (74)
**Aliteuliwa mwezi Novemba 2020**
- Utaalamu wa Sheria
- Msuluhishi
- Mahusiano na serikali

**2 Hisham Hendi** (41)
**Aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji tarehe 19 Machi 2019**
- Kiongozi mwerevu wa biashara
- Uzoefu katika masoko yanayoibukia
- Utekelezaji madhubuti wa bidhaa za kibunifu na huduma mpya

**3 Jacques Marais** (55)
**Aliteuliwa Mkurugenzi wa fedha mwezi Julai 2016**
- Ujuzi mkubwa wa masuala ya fedha
- Uzoefu mpana katika masoko yanayoibukia
- Ujuzi mkubwa katika sekta ya mawasiliano ya simu

**4 Winifred Ouko** (51)
**Aliteuliwa mwezi Novemba 2017**
- Utaalamu wa fedha na mipango
- Uzoefu mpana wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati kimataifa

**5 Thembeka Semane** (45)
**Aliteuliwa mwezi Novemba 2017**
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika
- Uzoefu katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na mikakati
- Utaalamu wa fedha

**6 Margaret Ikongo** (64)
**Aliteuliwa mwezi Novemba 2017**
- Utaalamu wa fedha
- Mahusiano na serikali
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika

**7 Diego Gutierrez** (45)
**Aliteuliwa mwezi Machi 2018**
- Mpanga mikakati ya kibiashara
- Maarifa mapana kuhusu teknolojia ya simu na uzoefu wa masoko yanayoibukia
- Utaalamu wa uongozi wa kimkakati

**8 Kenneth Gomado** (43)
**Aliteuliwa mwezi Machi 2018**
- Uzoefu wa masuala ya kifedha katika masoko yanayoibukia
- Ujuzi mkubwa wa sekta za mawasiliano ya simu na FMCG
- Uzoefu wa masuala ya ushauri na ukaguzi

**9 Matimba Mbungela** (49)
**Aliteuliwa mwezi Agosti 2017**
- Maarifa na uzoefu mpana wa usimamizi wa vipaji
- Utaalamu katika taratibu bora za kusimamia rasilimali watu
- Uzoefu katika uendeshaji wa shughuli za kimataifa

**10 Nkateko Nyoka** (58)
**Aliteuliwa mwezi Aprili 2020**
- Uzoefu katika sheria na sera za umma.
- Utaalamu katika usimamizi wa mashirika
- Uongozi na mahusiano na wadau

**11 Dejan Kastelic** (43)
**Aliteuliwa mwezi Agosti 2020**
- Uzoefu mpana wa sekta ya mawasiliano na TEHAMA
- Uzoefu wa masoko mbalimbali ya kimataifa na yanayoibukia
- Utaalamu wa uendeshaji na utekelezaji wa mikakati

**12 Raisibe Morathi** (51)
**Aliteuliwa mwezi Novemba 2020**
- Uzoefu wa masuala ya fedha kimataifa
- Utaalamu wa uongozi kimkakati
- Utaalamu katika kung'amua fursa za kuunganisha au kununua biashara

A Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji  R Kamati ya Ujira  N Kamati ya Uteuzi

# Kamati ya Uongozi




























1 **Hisham Hendi** (41)
**Mkurugenzi Mkuu**
Alijiunga Vodacom mwaka 2014,
Alijiunga Vodafone mwaka 2003.

2 **Jacques Marais** (55)
**Mkurugenzi wa Fedha**
Alijiunga Vodacom mwaka 2001.

3 **Linda Riwa** (34)
**Mkurugenzi wa Biashara - Wateja Binafsi**
Alijiunga Vodacom mwaka 2017.

4 **Epimack Mbeteni** (43)
**Mkurugenzi wa Biashara - M-Pesa**
Alijiunga Vodacom mwaka 2014.

5 **Arjun Dhillon** (41)
**Mkurugenzi wa Biashara - Wateja wa Kibiashara**
Alijiunga Vodacom mwaka 2017,
Safaricom mwaka 2015.

6 **Andrew Lupembe** (48)
**Mkurugenzi Masuala ya Mtandao**
Alijiunga Vodacom mwaka 2007.

7 **Olaf Mumburi** (45)
**Mkurugenzi wa Sheria na Udhibiti**
Alijiunga Vodacom mwaka 2008.

8 **Rosalynn Mworia** (41)
**Mkurugenzi Masuala ya Mahusiano**
Alijiunga Vodacom mwaka 2008.

9 **Harriet Lwakatare** (43)
**Mkurugenzi Huduma kwa Wateja**
Alijiunga Vodacom mwaka 2012.

10 **Vivienne Penessis** (46)
**Mkurugenzi Rasilimali Watu**
Alijiunga Vodacom mwaka 2018.

11 **Nguvu Kamando** (46)
**Mkurugenzi wa Huduma za Kidigitali**
Alijiunga Vodacom mwaka 2002.

12 **Tax Agapinus** (56)
**Mkurugenzi Dharura na Utekelezaji**
Alijiunga Vodacom mwaka 2020.

13 **Athumani Mlinga** (53)
**Mkurugenzi TEHAMA**
Alijiunga Vodacom mwaka 2003.

# Taarifa ya uongozi wa Kampuni


## Taarifa ya utekelezaji

**Vodacom Tanzania Public Limited Company ('Vodacom Tanzania') inajizatiti kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa uaminifu, maadili na utaalamu katika biashara.**

Kanuni za uongozi wa Kampuni zinajumuisha nidhamu, uhuru wa maamuzi, uwajibikaji, usawa, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau. Kanuni hizi zinazingatiwa katika taratibu za udhibiti wa ndani na sera za Vodacom Tanzania zinazoongoza utendaji wa Kampuni na zinawiana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamizi unaofanywa na kampuni za umma zilizoorodheshwa nchini Tanzania.

### Muundo wa usimamizi wa Kampuni

Muundo ufuatao unaonesha safu ya viongozi wa Vodacom Tanzania tarehe 31 Machi 2021:



## Maadili ya viongozi

Bodi inakubali uwajibikaji wa pamoja katika kueleza namna ambavyo maadili na tabia za kimaadili zinapaswa kutekelezwa katika Kampuni. Hii ni pamoja na kupanga taratibu za utendaji wa wajumbe wa bodi ili kuhakikisha kuwa wanatenda kwa uadilifu, uzoefu, uwajibikaji, haki na uwazi. Sifa hizi ni kipimo cha maadili kinachozingatiwa katika tamaduni za uendeshaji wa Kampuni.

## Uongozi na Kamati za Bodi

### Bodi

Vodacom Tanzania ina bodi yenye wakurugenzi 12, ambapo kati yao wanne (pamoja na Mwenyekiti) ni wakurugenzi huru wasio watendaji, sita kati yao si watendaji (lakini si huru kwa kuwa wanawakilisha wadau wakuu), na wawili ni wakurugenzi watendaji.

Bodi imeridhika kuwa uwiano wa wataalamu wenye maarifa, ujuzi na uzoefu wa aina mbalimbali ni wa kutosha.

Bodi inaweza kukutana kwa ajili ya kufanya shughuli, kuahirisha na vinginevyo kudhibiti mikutano yake itakavyoona inafaa. Mikutano ya bodi inafanyika mara kwa mara kupitia mkakati, ufanisi wa kiuendeshaji na kifedha, na vilevile usimamizi. Mikutano maalum ya bodi inaweza kufanyika wakati itakapohitajika.

Kamati ya Uteuzi hufanya mapitio ya utaratibu wa mwendelezo wa majukumu ya bodi na kamati zake ili kuhakikisha kuwa zina watu sahihi wenye ujuzi na uzoefu kwa siku zijazo. Mkurugenzi Mtendaji ana wajibu wa kuhakikisha kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi wana ujuzi, mamlaka na rasilimali za kutosha kutekeleza mkakati wa Kampuni.

### Uwajibikaji

Bodi ina wajibu wa kuhakikisha Kampuni inakuwa na mafanikio. Kazi yake ni kuongoza na kutoa maamuzi ya busara katika kuielekeza kufanikisha ukuaji endelevu na kufanya kazi kwa maslahi ya wanahisa.

Kwa mujibu wa utendaji bora, Mwenyekiti na Mkurugenzi mtendaji wana majukumu tofauti. Mwenyekiti anawajibu wa kuongoza Bodi, wakati Mkurugenzi Mtendaji anawajibika kusimamia uendeshaji wa Kampuni.

**Katiba ya Bodi inaeleza wajibu wa Bodi, ambao ni pamoja na:**

- Kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji na Mkurugenzi wa Fedha;
- Kusimamia kwa karibu mwelekeo wa kimkakati wa Vodacom Tanzania;
- Kupitisha miradi mikubwa, ununuzi au mauzo ya vitu;
- Kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala ya biashara ya Kampuni, mbali na menejimenti;
- Kuhakikisha kuwa miundo, sera na taratibu stahiki zinakuwepo;
- Kuhakikisha udhibiti wa ndani wa Kampuni unakuwa na mafanikio;
- Kupitia na kutathmini dharura za Kampuni;
- Kupitisha bajeti ya mwaka na mpango wa utekelezaji;
- Kupitisha matokeo ya pamoja ya fedha ya mwaka na ya muda na vilevile mawasiliano kwenda kwa wadau;
- Kupitisha muundo wa uongozi na mpango wa mwendelezo wa uwepo wa viongozi; na
- Usimamizi wa teknolojia ya habari.

### Wakurugenzi

Katiba ya Kampuni inaeleza kuwa wakurugenzi wanapaswa kustaafu kwa zamu na wanaweza kuchaguliwa tena baada ya kila miaka mitatu.

### Mwenyekiti

Katiba inaitaka Bodi kumchagua Mwenyekiti kila mwaka. Bodi inaridhika kuwa Mwenyekiti anaweza kutimiza majukumu yake ipasavyo. Jaji (mstaafu) Thomas B. Mihayo aliteuliwa kuwa Mwenyekiti kuanzia tarehe 1 Novemba 2020. Uteuzi wa kushika nafasi hiyo ya uenyekiti utajadiliwa na Bodi baada ya muda wake wa sasa kuisha.

### Kupata ushauri huru

Bodi inatambua kuwa inawezekana kukawa na wakati ambapo wakurugenzi wakaona kuwa ni muhimu kupata ushauri huru wa kitaalamu. Kampuni itagharamia huduma hii kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

# Shughuli za uongozi wa Kampuni

## Vodacom Tanzania PLC

### Mikutano ya Bodi

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi kwa mwaka huu.

| Jina la Mkurugenzi | 30 Aprili 2020 Maalum | 21 Mei 2020 | 14 Julai 2020 Maalum | 20 Agosti 2020 | 29 Oktoba 2020 Maalum | 12 Novemba 2020 | 21 Januari 2021 Maalum | 18 Machi 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo (Mwenyekiti) | – | – | – | – | – | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Margaret Ikongo | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Thembeka Semane | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Dejan Kastelic | – | – | – | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Diego Gutierrez | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Hisham Hendi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Kenneth Gomado | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Nkateko Nyoka | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | – | ✓ |
| Bi Raisibe Morathi | – | – | – | – | – | ✓ | – | ✓ |
| Bw Andries Delport | ✓ | R | R | R | R | R | R | R |
| Bw Till Streichert | ✓ | ✓ | R | R | R | R | R | R |
| Bw Sithilizwe Mdlalose | – | – | – | ✓ | ✓ | R | R | R |

**Zingatia:**
1. Andries Delport alistaafu tarehe 14 Mei 2020.
2. Till Streichert alistaafu tarehe 30 Juni 2020.
3. Sitholizwe Mdlalose aliteuliwa tarehe 14 Julai 2020 na kustaafu tarehe 31 Oktoba 2020.
4. Nkateko Nyoka aliteuliwa tarehe 1 Aprili 2020.
5. Dejan Kastelic aliteuliwa tarehe 17 Agosti 2020.
6. Raisibe Morathi aliteuliwa tarehe 1 Novemba 2020.
7. Thomas B. Mihayo aliteuliwa tarehe 1 Novemba 2020.
8. Margaret Ikongo alishika wadhifa wa Mwenyekiti wa muda wa bodi kuanzia tarehe 1 Desemba 2019 hadi 31 Oktoba 2020.

### Mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Jedwali hapo chini linaonesha mahudhurio ya wajumbe katika mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji kwa mwaka huo.

| Jina la Mjumbe | 30 Aprili 2020 Maalum | 31 Mei 2020 | 14 Julai 2020 Maalum | 20 Agosti 2020 | 29 Oktoba 2020 Maaluml | 12 Novemba 2020 | 21 Januari 2021 Maalum | 18 Machi 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bi Margaret Ikongo (Mwenyekiti) | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Thembeka Semane | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

**Note:**
Winifred Ouko alishika wadhifa wa Mwenyekiti wa muda wa Kamati tangu tarehe 1 Januari 2020 hadi Oktoba 2020.

### Mikutano ya Kamati ya Ujira

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe katika mikutano ya Kamati ya Ujira mwaka huu.

| Jina la Mjumbe | 21 Mei 2020 | 20 Agosti 2020 | 12 Novemba 2020 | 17 Machi 2021 |
|---|---|---|---|---|
| Bi Winifred Ouko (Mwenyekiti) | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Diego Gutierrez | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Matimba Mbungela | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

## Mikutano ya Kamati ya Uteuzi

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe kwenye mikutano ya Kamati ya Uteuzi mwaka huu.

| Jina la Mjumbe | 18 Agosti 2020 | 17 Machi 2021 |
|---|---|---|
| Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo (Mwenyekiti) | – | ✓ |
| Bi Margaret Ikongo | ✓ | x |
| Bi Winifred Ouko | ✓ | ✓ |
| Bw Matimba Mbungela | ✓ | ✓ |

**Zingatia:**
1. Margaret Ikongo alishika wadhifa wa Mwenyekiti wa muda wa Kamati tangu tarehe 1 Desemba 2019 hadi 31 Oktoba 2020.
2. Jaji (mstaafu) Thomas B Mihayo aliteuliwa kuwa Mwenyekiti tarehe 1 Novemba 2020.

# Kampuni Tanzu

## Mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya M-Pesa Limited mwaka huu.

| Jina la Mkurugenzi | 20 Mei 2020 | 12 Juni 2020 Maalum | 19 Agosti 2020 | 11 Novemba 2020 | 17 Machi 2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| Bw Sitoyo Lopokoiyit (Mwenyekiti) | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Christopher Williamson | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Olaf Mumburi | ✓ | x | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Epimack Mbeteni | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe kwenye mikutano ya Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji ya M-Pesa Limited mwaka huu.

| Jina la Mjumbe | 20 Mei 2020 | 19 Agosti 2020 | 11 Novemba 2020 | 17 Machi 2021 |
|---|---|---|---|---|
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Christopher Williamson | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Olaf Mumburi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

## Mikutano ya Bodi ya Shared Networks Tanzania Limited

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi katika mikutano ya Bodi ya Shared Networks Tanzania Limited mwaka huu.

| Jina la Mkurugenzi | 19 Mei 2020 | 18 Agosti 2020 |
|---|---|---|
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ |
| Bi Rosalynn Mworia | ✓ | ✓ |

**Zingatia:** Shared Networks Tanzania Limited iko kwenye mchakato wa kufungwa kwa hiari

## Mikutano ya Bodi ya Vodacom Trust Limited

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wakurugenzi kwenye mikutano ya Bodi ya Vodacom Trust Limited mwaka huu.

| Jina la Mkurugenzi | 20 Mei 2020 | 19 Agosti 2020 |
|---|---|---|
| Bw Jacques Marais | ✓ | ✓ |
| Bi Rosalynn Mworia | ✓ | ✓ |

**Zingatia:** Vodacom Trust Limited iko kwenye mchakato wa kufungwa kwa hiari

## Mikutano ya Vodacom Tanzania Foundation (NGO)

Jedwali lifuatalo linaonesha mahudhurio ya wajumbe kwenye mikutano ya Bodi ya Vodacom Tanzania Foundation mwaka huu

| Jina la Mkurugenzi | 20 Mei 2020 | 19 Agosti 2020 | 10 Novemba 2020 | 16 Machi 2021 |
|---|---|---|---|---|
| Bi Rosalynn Mworia | ✓ | ✓ | ✓ | x |
| Bw Olaf Mumburi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bw Evans Lyimo | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Harrieth Lwakatare | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bi Vivienne Penessis | x | ✓ | ✓ | x |

**Zingatia:** Vodacom Tanzania Foundation (NGO) ipo kwenye mchakato wa kufungwa kwa hiari. Shughuli za Foundation ni sehemu ya shughuli za masuala ya kijamii za VTPLC.

# Taarifa ya Masuala ya Ujira 2021

## Barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira

**Wapendwa Wanahisa**

Ninayo furaha, kwa niaba ya Bodi kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Ujira ya Kampuni.

Taarifa hii inatoa muhtasari wa falsafa na sera yetu inayohusu wakurugenzi watendaji na wasio watendaji, na kwa kifupi inaeleza namna sera ilivyotekelezwa katika kipindi cha mwaka. Kazi yetu kama wajumbe wa Kamati ya Ujira ni kusaidia na kuishauri Bodi kuhusu masuala yanayohusiana na ujira wa wakurugenzi watendaji. Tunawajibika kuhakikisha kuwa falsafa na sera ya ujira inaunga mkono azma ya Kampuni ya kutoa ujira ulio sawa na stahiki ambao utavutia, kubakiza na kutoa motisha kwa watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, wenye jukumu la kuongeza thamani ya wanahisa kwa kutekeleza malengo ya kimkakati ya Kampuni.

Tunaendelea kupitia sera zetu za ujira na kuhakikisha tunatekeleza sheria na miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana ('CMSA') pamoja na kukidhi matakwa ya wanahisa.

Ukiangalia shughuli zetu kwa mwaka uliopita, kuna masuala mawili muhimu ninapenda kuyasisitiza:

- Inafurahisha sana kuona hatua tulizopiga katika kutekeleza wajibu wetu kuongeza wazawa katika safu ya uongozi wetu. Mwaka huu, wakurugenzi watatu wapya wameteuliwa, wote wakiwa ni Watanzania, na hivyo kuongeza uwakilishi wa wazawa katika kamati ya uongozi kufika 72.7% kutoka 30.8% miaka minne iliyopita, na wawili kati ya viongozi walioteuliwa ni wafanyakazi waliopandishwa vyeo. Tumefikia kiwango cha kuridhisha cha kuwabakiza wafanyakazi kazini na ukuaji wa ndani.
- Na pia, Vodacom Tanzania PLC imepata alama ya juu kabisa na ya kuridhisha katika Kundi la makampuni ya Vodacom kwenye matokeo ya utafiti wa ari ya wafanyakazi (Team Spirit Index). Hii imeonesha mabadiliko chanya ya utamaduni wa utendaji na mahusiano kazini .



Kamati imezingatia taratibu za utoaji wa taarifa kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya Soko la Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994, na imeridhika kuwa taarifa hii imekidhi miongozo ya uendeshaji wa kampuni za umma zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa nchini, sambamba na kuwa makini katika utoaji wa taarifa nyeti za kiushindani. Ninapenda kutoa shukrani kwa wajumbe wenzangu wa kamati kwa kuendelea kuniunga mkono, na ninatarajia kuendelea kufanya kazi nao mwaka ujao.

**Winifred Ouko**
Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira

Kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kuhusu taratibu za usimamzi wa makampuni ya umma yaliyoorodheshwa nchini Tanzania, taarifa hii inaeleza sera za Vodacom Tanzania za ujira kwa wakurugenzi watendaji na wakurugenzi wasio watendaji husan kiasi na aina za ujira kwa wakurugenzi ikiwa ni pamoja na wakurugenzi wasio watendaji kwa pamoja.

## Falsafa, sera na mfumo wetu wa ujira kwa mwaka huu kwa wakurugenzi watendaji.

Lengo letu ni kuwavutia, kuwawezesha kubaki na kuwapatia motisha watendaji wenye uwezo wa hali ya juu, sambamba na kulinganisha ujira wao na maslahi ya wanahisa na taratibu bora za utekelezaji. Utaratibu wetu wa stahiki za ajira ni mpana, wenye ulinganifu kwenye vipengele vifuatavyo:

- Ujira wa uhakika (GP);
- Motisha ya muda mfupi (STIP);
- Motisha ya muda mrefu (LTIP);
- Programu mbalimbali za utambuzi;
- Fursa mbalimbali za kujifunza na kujiendeleza;
- Mazingira ya kazi yanayovutia; na
- Programu nzuri ya ustawi wa wafanyakazi.

Viongozi watendji wanafuata falsafa ya 'Jumla ya gharama kwa kampuni', ambayo tunairejelea kama ujira uhakika (GP). Michango katika huduma za tiba, fedha za ustaafu na mafao ya bima yamejumuishwa katika GP.

Vipengele hivyo hapo juu vinaendana na kuimarishwa kwa utaratibu wetu wa kutathmini utendaji kazi na kuendeleza vipaji. Sera yetu ni kuwapa marupurupu viongozi wetu watendaji kutokana na michango yao katika ufanisi wetu kimkakati, kifedha na kiutendaji. Ili kuwa muajiri anayeheshimika katika sekta yetu tunahitaji kuvutia, kuendeleza na kubakiza vipaji bora na rasilimali ya wataalamu wa ndani na kimataifa.

Kila mwaka tunalinganisha viwango na kuongeza malipo katika GP kulingana na soko, ufanisi binafsi na uwezo. Tathmini ya ufanisi binafsi na uwezo wa kiutendaji hubainishwa kupitia utaratibu wetu wa kupima utendaji na uwezo wa kiutendaji wa wafanyakazi wetu. Matokeo ya utaratibu huu, huchangia katika uamuzi wa mabadiliko ya motisha ya muda mfupi na muda mrefu.

Motisha yetu ya muda mfupi inayolipwa kama bonasi ya fedha taslimu hutokana na kufikia malengo kwenye utendaji wa masuala ya fedha, mikakati, uendeshaji wa vitengo na malengo binafsi ambayo kila mtendaji amepewa. Kiasi kilichopo kwa ajili ya motisha ya muda mfupi kinatokana na utendaji kwenye masuala ya fedha kadiri ya malengo yaliyowekwa na kukubaliwa.

Viongozi watendaji ambao wametumwa kufanya kazi Vodacom Tanzania kutoka Vodacom Group Limited, hulipwa motisha ya muda mrefu kwa mujibu wa taratibu za kundi la makampuni la Vodacom Group, ambapo hupewa umiliki wa hisa na mwajiri wao. Hii huchochea utendaji unaoakisi umiliki na uaminifu, na huchangia katika lengo la Vodacom la kuwabakiza watendaji hodari. Mfumo huo ni mfumo kamili wa umiliki, na matokeo yake wahusika hupata gawio kutoka siku walipopewa hisa japokuwa thamani ya hisa inaweza tu kupatikana baada ya miaka mitatu na ni kwa kulingana na kiwango ambacho masharti ya kupewa hisa hizo yametimizwa.

## Utoaji taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji

### Ujira wa wakurugenzi watendaji – Malipo ya Uhakika

Ujira wa wakurugenzi watendaji ulifanyiwa mapitio kwa kuzingatia ulinganishi na ujira wa watendaji wengine katika soko, na pia athari za kushindwa kuwabakiza watendaji muhimu katika menejimenti.

Kwa kuzingatia utaratibu/sera ya ujira, taarifa iliyo kwenye toleo hili ni kwa wakurugenzi waliostahili, ambapo maamuzi yote yanayohusu ujira yamefanywa kwa kuzingatia utaratibu wa ujira kama ulivyopitishwa wakati uliopita na wanahisa. Kama ilivyo kwa mwaka uliotangulia, hakuna mabadiliko yaliyofanywa katika utekelezaji wa sera/utaratibu wa ujira katika mwaka huu.

Taarifa za ujira wa wakurugenzi watendaji na wasio watendaji zimetolewa kwa muhtasari katika jedwali hapo chini.

| Wakurugenzi | Bodi | Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | Ujira | Uteuzi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| TB Mihayo | 150 000 | | | | **150 000** |
| M Ikongo | 30 000 | 15 000 | | | **45 000** |
| W Ouko | 30 000 | 8 000 | 12 000 | 3 000 | **53 000** |
| T Semane | 30 000 | 8 000 | | | **38 000** |
| D Gutierrez | 30 000 | | 4 000 | | **34 000** |
| M Mbungela | 30 000 | | 4 000 | 3 000 | **37 000** |
| N Nyoka | 30 000 | | | | **30 000** |
| D Kastelic | 30 000 | | | | **30 000** |
| K Gomado | 30 000 | | | | **30 000** |
| R Morathi | 30 000 | | | | **30 000** |
| H Hendi | | | | | **0** |
| J Marais | | | | | **0** |
| | | | | | **477 000** |

Fedha hizi ni jumla ya ada kwa dola ya Marekani, ikijumuisha kodi zote pamoja na kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wakazi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka kwa mikutano ya kawaida isiyopungua minne kwa mwaka, mikutano maalum mitatu na Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa dharura kama itahitajika.


(NBAA)
The National Board of Accountants and Auditors - Tanzania
This Award is given to
Vodacom Tanzania Plc
as 1st Winner
in the
Trading and Distribution Category
for the Best Presented Financial Statements Award for the year 2019
Awarded on 5th December, 2020

# Maelezo ya hesabu za fedha za mwaka

Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021

## Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Taarifa ya wakurugenzi | 36 |
| Tamko la majukumu ya wakurugenzi | 43 |
| Tamko la mkuu wa kitengo cha fedha | 43 |

# Taarifa ya wakurugenzi

## Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021

Wakurugenzi wanawasilisha taarifa yao pamoja na taarifa ya pamoja iliyokaguliwa ya fedha ya Vodacom Tanzania PLC ('Kampuni'), na kampuni zake tanzu (kwa pamoja, 'Kundi la Kampuni') kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021..

### Aina ya biashara

Kundi la Kampuni huendesha biashara ya kutoa huduma ya mtandao wa mawasiliano ya simu na huduma za fedha kwa njia ya simu nchini. Pia linatoa huduma nyingine za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na huduma za mawasiliano ya kuunganishwa kwa waya.

### Tathmini ya masuala ya kiuendeshaji na kifedha

Matokeo kwa mwaka huu yamewekwa katika taarifa za pamoja na taarifa binafsi za faida au hasara na mapato mengine.

Mapato ya Kundi la Kampuni kwa mwaka yalipungua kwa 5.6% hadi shilingi milioni 974 391 (2020: shilingi milioni 1 032 667). Faida ya uendeshaji ya Kundi la Kampuni ilipungua kwa 48.4% hadi shilingi milioni 49 514 (2020: shilingi milioni 95 999). Kundi la Kampuni limepata hasara ikilinganishwa na faida iliyopatikana mwaka uliopita. Faida ilipungua kwa 165.8% hadi hasara halisi ya shilingi milioni 30 106 (2020: Faida halisi ya shilingi 45 762).

Mapato ya Kundi la Kampuni kabla ya riba; kodi; uchakavu; faida au hasara katika kuondosha mali, mitambo na mali zisizoshikika; na gharama zinazohusiana na hisa ('EBITDA') yalipungua kwa 13.4% hadi shilingi milioni 316 134 (2020: shilingi milioni 364 996) na kiwango cha EBITDA cha 32.4%, ikiwa ni upungufu wa alama 2.9 za asilimia mwaka hadi mwaka.

Kuanzia tarehe 1 Aprili 2020, biashara yetu ya fedha kwa simu ilianza kuendeshwa kupitia kampuni iliyosajiliwa kisheria ya M-Pesa Limited, ikimilikiwa kikamilifu na Vodacom Tanzania PLC, kwa mujibu wa sheria ya taifa ya mfumo wa malipo. Wakati M-Pesa Limited kama biashara inayojitegemea inazalisha faida, biashara ya GSM imepata hasara mwaka huu. Matokeo haya ya M-Pesa yalijumuishwa katika matokeo ya Kampuni ya mwaka. Utaratibu huu umeathiri msingi wa kukokotoa kodi ya mwaka, na kusababisha kodi kuongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Wateja wetu amilifu wa siku 90 wamepungua hadi kufikia 14 861 000 (2020: 15 513 000) ikiwa ni pungufu kwa 4.2% kwa mwaka.

### Gawio

Katika Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika tarehe 30 Oktoba 2020, wanahisa walipitisha gawio la mwisho kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2020 kulingana na sera, pamoja na gawio maalum. Wanahisa walilipwa gawio la mwisho la shilingi 12.26 (2020: shilingi 20.43) kwa kila hisa, sawa na shilingi milioni 27 462 (2020: shilingi milioni 38 819), na gawio maalum la shilingi 178.57 (2020: hakuna) kwa kila hisa, sawa na shilingi milioni 400 000 kutoka katika akiba ya mapato.

Gawio la mwisho lilikuwa ni sawa na 60% (2020: 60%) ya faida halisi baada ya kodi.

Malipo ya gawio la mwisho la shilingi milioni 27 462 sambamba na gawio maalum la shilingi milioni 400 000 yalifanyika tarehe 13 Novemba 2020 kwa wanahisa walioorodheshwa katika rejesta wakati wa kufunga biashara tarehe 19 Agosti 2020 na 16 Oktoba 2020.

Bodi ya wakurugenzi hupendekeza gawio kwa ajili ya kuidhinishwa na wanahisa katika mkutano mkuu wa mwaka kulingana na sera ifuatayo ya gawio:

Kampuni inakusudia kulipa sehemu kubwa iwezekanavyo ya faida yake baada ya kodi baada ya kutenga kiasi cha kulipa madeni ili kukidhi matakwa ya bajeti na mpango wa biashara, na kuzingatia mahitaji ya fedha kwa ajili ya uwekezaji. Hakuna tarehe maalum iliyopangwa ya kustahili kupata gawio ila tarehe ya malipo itapendekezwa na bodi na kupitishwa na wanahisa wakati wa kuidhinisha gawio, kwa kuzingatia matakwa ya taratibu za kuorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam ('DSE').

Kwa kuzingatia yaliyosemwa hapo juu, sera ya gawio ni kulipa angalau 50% ya faida baada ya kodi. Hivyo, Bodi ya Wakurugenzi haipendekezi gawio kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2021.

### Uwezo wa kulipa madeni na ukwasi wa Kampuni

Bodi inaona kuwa Kampuni ina uwezo wa kulipa madeni, kulingana na matakwa ya Sheria ya Makampuni, Na 12 ya mwaka 2002 ya Tanzania. Kampuni ilikuwa na mali za thamani ya shilingi milioni 43 897 kwa 31 Machi 2021, (2020: mali zilikuwa za thamani ya shilingi milioni 470 064) ambazo ni pamoja na shilingi milioni 244 257 fedha taslimu na uwekezaji wa hawala za serikali ya Tanzania (2020: Shilingi milioni 638 471).

## Muundo wa mtaji na umiliki wa hisa

Umiliki wa hisa zilizotolewa na kulipwa ni kama zinavyooneshwa hapo chini:

| | 2021 % | 2020 % |
|---|---|---|
| Vodacom Group Limited | **75.00** | 75.00 |
| Wanahisa wengine | **25.00** | 25.00 |
| | **100.00** | 100.00 |

Kufikia tarehe 31 Machi 2021, mtaji wa hisa ulioidhinishwa wa Kundi la Kampuni ulikuwa shilingi milioni 200 000 ikiwa ni hisa milioni 4 000 za kawaida zenye thamani ya shilingi 50 kwa kila hisa, wakati mtaji wa hisa uliolipwa ni shilingi milioni 112 000 unaotokana na hisa za kawaida 2 240 000 300 zenye thamani ya shilingi 50 kwa kila hisa. Hakukuwa na mabadiliko katika mtaji wa hisa ulioidhinishwa au mtaji uliotolewa mwaka huu.

## Gharama za uwekezaji

Katika kipindi cha mwaka, Kundi la Kampuni liliwekeza kiasi cha shilingi milioni 122 449 (2020: shilingi milioni 159 393) katika mitambo na mali zisizoshikika. Uwekezaji huu uligharimiwa kwa kutumia fedha zilizozalishwa ndani.

Maelezo zaidi kuhusu mali za kudumu, mitambo na mali zisizoshikika za Kundi la Kampuni yamewasilishwa katika Maelezo 17 na 18 kwenye taarifa za fedha za pamoja na taarifa binafsi za fedha za kampuni (nakala ya kiingereza).

Taarifa kuhusu majukumu ya Kampuni zimewasilishwa katika Maelezo 32 katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni (nakala ya kiingereza).

## Mipango ya biashara na maendeleo ya baadaye

Kampuni inalenga kuendeleza uwekezaji katika katika maeneo yake muhimu ya kimkakati ambayo ni data, M-Pesa na huduma kwa wateja wa matumizi ya biashara.

## Kampuni tanzu na taasisi zake

Taarifa za fedha za kampuni zinajumuisha taarifa za fedha za kampuni zake tanzu, yaani Vodacom Trust Limited ambayo ni kampuni yenye ukomo kwa udhamini na ina mtaji wa hisa; na M-Pesa Limited, Shared Networks Tanzania Limited ('SNT'), Vodacom Tanzania Limited (iliyosajiliwa huko Zanzibar), ambazo ni kampuni zenye dhima ya ukomo na mtaji wa hisa. Taarifa za pamoja za fedha pia zinajumuisha taasisi ya M-Pesa, The Registered Trustees of M-Pesa.

### Vodacom Trust Limited

Shughuli kuu ya Vodacom Trust Limited ni kuwa wadhamini wenye jukumu la kutunza na kulinda fedha zote zilizopatikana kutokana na/au zinazohusiana na huduma za fedha kwa simu kupitia M-Pesa kwa manufaa ya watumiaji wa huduma za M-Pesa. Tarehe 23 Oktoba 2018, jina la kampuni lilibadilishwa kutoka 'M-Pesa Limited' kuwa 'Vodacom Trust Limited' kufuatia kutolewa kwa hati ya kubadili jina iliyotolewa na Wakala wa Usajili na Leseni Tanzania ('BRELA'). Kubadili jina ilikuwa muhimu ili kutimiza masharti ya Sheria ya Mfumo wa Taifa wa Malipo, 2015. Akiba zilizomilikiwa kiudhamini na 'Vodacom Trust Limited' zilihamishiwa kwenye taasisi mpya ya Registereed Trustees of M-Pesa Trust Funds kwa mujibu wa kanuni za Mfumo wa Taifa wa Malipo. Mchakato wa kuifunga Vodacom Trust Limited unaenda.

### Shared Networks Tanzania Limited (SNT)

Tarehe 19 Julai 2016, Kundi la Kampuni lilinunua 100% ya hisa za SNT. SNT ilikuwa ikitoa huduma za mtandao kwa mauzo ya jumla ambayo ilikuwa na leseni ya kutumia masafa ya 900 MHz katika maeneo ya vijijini hapa Tanzania. Mwaka 2019, Vodacom ilipata kibali kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ('TCRA') kutumia masafa ambayo yalikuwa yakimilikiwa na SNT. Mwaka huu, wakurugenzi wameamua kuifunga SNT baada ya kuhamisha mali na madeni yake kwenda kwenye Kundi la Kampuni. Uhamishaji wa mali halisi ulikamilika na mfilisi ameshateuliwa.

### Vodacom Tanzania Limited (iliyosajiliwa Zanzibar)

Vodacom Tanzania Limited (iliyosajiliwa Zanzibar) ina mtaji wa hisa 100 ambazo hazijalipiwa ambapo hisa 99 zilitolewa kwa Kundi la Kampuni. Kampuni hii haijafanya kazi tangu ilipoandikishwa na sasa iko katika mchakato wa kufuta usajili wake.

### M-Pesa Limited

M-Pesa Limited iliandikishwa tarehe 26 Oktoba 2018. Kulingana na kanuni za Mifumo ya Taifa ya Malipo ambazo zilianza kutumika kuanzia Julai 2016, kampuni hii ilituma maombi ya leseni ya kutoa huduma za fedha kielektroniki ('EMI') ambayo ilitolewa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 13 Machi 2019. Kufuatia kupata leseni hiyo, shughuli kuu za kampuni hii ni kutoa huduma za fedha chini ya kanuni za kutoa huduma za fedha kielektroniki 'EMI' zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania. Kampuni hii imeanza kufanya kazi mwaka huu.

## **Kampuni tanzu na taasisi zake** inaendelea

### Registered Trustees of M-Pesa Trust Funds

Registered Trustees of M-Pesa Trust Funds ilisajiliwa chini ya sheria ya uandikishaji wa wadhamini, Sura ya 318 ya Tanzania tarehe 25 Septemba 2019 kwa namba ya usajili 5656. Akiba iliyowekwa kwa udhamini na Vodacom Trust Limited ilihamishiwa kwenye taasisi hii mpya. Mdhamini ni taasisi isiyozalisha faida ambayo ina mamlaka ya kutekeleza malengo yake kwa maslahi mapana ya walengwa wa fedha kwenye akaunti za Mdhamini. Shughuli za Mdhamini ni pamoja na kusimamia na kuangalia ipasavyo akaunti za mdhamini; kuhakikisha kunakuwa na usalama wa fedha za walengwa kwenye akaunti za mdhamini na kuzilinda dhidi ya hatari kwa kuchukua hatua sahihi za kuweka usalama; kuhakikisha fedha za akaunti ya mdhamini zinatengwa na hazichanganywi na fedha kwa ajili ya shughuli nyingine.

## Kukopa

Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2021 Kampuni haikuwa na mkopo (2020: Hakuna).

## Umiliki wa Kampuni

Kundi la Kampuni linamilikiwa na kampuni mama ya Vodacom Group Limited, iliyoandikishwa na yenye makao yake makuu katika Jamhuri ya Afrika Kusini ambayo inamiliki 75.0% (2020: 75.00%) ya hisa za Kampuni zilizotolewa. Pia, kampuni ya Vodacom Group inamilikiwa na kampuni mama ya Vodafone Group Plc, iliyoandikishwa na yenye makao yake makuu nchini Uingereza.

## Miamala na makampuni washirika

Miamala na makampuni washirika ilifanyika kwa mtiririko wa kawaida wa kibiashara. Maelezo ya miamala na salio la miamala hiyo yameelezwa katika Maelezo 35 ya taarifa za pamoja za fedha na taarifa za fedha za kampuni binafsi (nakala ya kiingereza).

## Usajili na makao ya kampuni

Kampuni na kampuni zake tanzu zimesajiliwa na makao yake makuu yako katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Wakurugenzi na Katibu wa Kampuni

Wakurugenzi wa Kampuni ambao wamefanya kazi mwaka huu hadi kufikia tarehe ya kutoa taarifa hii ni kama wafuatao:

| Cheo/Jina | Amekuwa kazini tarehe 1 Aprili 2020 | Tarehe ya Uteuzi | Tarehe ya Kustaafu | Anafanya kazi katika tarehe ya kuripoti |
|---|---|---|---|---|
| **Wakurugenzi** | | | | |
| Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo (Mwenyekiti) | X | 1 Novemba 2020 | – | ✓ |
| Andries Delport* | ✓ | – | 14 Mei 2020 | X |
| Margaret Ikongo (Mwenyekiti wa Muda) | ✓ | 1 December 2019 | – | ✓ |
| Till Streichert*** | ✓ | – | 30 Juni 2020 | X |
| Thembeka Semane* | ✓ | – | – | ✓ |
| Winifred Ouko^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Matimba Mbungela* | ✓ | – | – | ✓ |
| Diego Gutierrez^^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Kenneth Gomado^^^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Nkateko Nyoka* | ✓ | 1 Aprili 2020 | – | ✓ |
| Sitholizwe Mdlalose**** | X | 14 Julai 2020 | 31 Oktoba 2020 | X |
| Dejan Kastelic** | X | 17 August 2020 | – | ✓ |
| Raisibe Morathi* | X | 1 Novemba 2020 | – | ✓ |
| **Viongozi Watendaji** | | | | |
| Hisham Hendi^^^^ | ✓ | – | – | ✓ |
| Jacques Marais* | ✓ | – | – | ✓ |
| **Katibu wa Kampuni** | | | | |
| Caroline Mduma | ✓ | – | – | ✓ |

* Mwafrika Kusini ** Slovenia *** Mjerumani **** Mwingereza ^ Mkenya ^^ Mbolivia ^^^ Mghana ^^^^ Mmisri

Wakurugenzi wengine wote ni Raia wa Tanzania.

## Maslahi ya wakurugenzi

Wakurugenzi hawana maslahi yoyote ya moja kwa moja katika mtaji wa hisa zilizotolewa za Kampuni au kampuni tanzu yoyote.

## Uongozi wa Kampuni

Kampuni inahakikisha kuwa huduma za biashara zinatolewa kwa uaminifu, maadili na utaalamu wa hali ya juu. Kanuni za uongozi wa mashirika zinasisitiza kutunza nidhamu, uhuru, haki, uwajibikaji kwa jamii, uwazi na uwajibikaji wa wakurugenzi kwa wadau wote. Kanuni hizi zimeingizwa kwenye taratibu za usimamizi wa ndani na sera zinazoongoza utendaji wa Kampuni.

### Bodi ya Wakurugenzi

Bodi inawajibika kwa ujumla kuhakikisha mafanikio ya Kampuni. Kazi yake ni kuongoza na kufanya maamuzi sahihi katika kuelekeza Kampuni kufikia ukuaji endelevu na kuiendesha kwa maslahi ya wanahisa.

Wakurugenzi wasio watendaji wanachangia uzoefu na maarifa makubwa waliyo nayo kwenye kamati za Bodi. Kamati zote zinafanya kazi chini ya miongozo iliyopitishwa na Bodi, ambayo huboreshwa mara kwa mara ili kuendana na mabadaliko katika sheria ya mashirika na taratibu bora za uongozi. Bodi imekasimu baadhi ya majukumu yake katika kamati tatu kama inavyoelezwa hapo chini.

### Kamati ya Ujira

Kamati ya Ujira inafanya kazi ya kuwezesha na kusaidia Bodi iweze kutekeleza majukumu yake kwa:

- Kupanga na kukubaliana kuhusu ujira na utaratibu wote wa malipo kwa viongozi waandamizi, ukiacha waliotoka kampuni nyingine za Vodacom;
- Kupanga, kukubaliana na kuandaa sera ya ujira ya Kampuni na kuhakikisha inaendana na sera ya ujira ya 'Vodacom Group Limited';
- Kuhakikisha uwepo wa mikakati na programu zinazozingatia haki na ushindani ili kuwezesha kuajiri, kutoa motisha na kubakiza wafanyakazi wachapakazi katika ngazi zote ili kusaidia kufanikisha malengo ya Kampuni na kulinda maslahi ya wanahisa;
- Kupitia na kupendekeza kwenye Bodi vigezo muhimu vya kupima ufanisi wa viongozi waandamizi katika kutekeleza kazi na majukumu yao; na
- Kuandaa na kutekeleza falsafa ya sera ya ujira.

### Kamati ya Uteuzi

Kamati ya Uteuzi inafanya kazi ya kuwezesha na kusaidia Bodi kutekeleza majukumu yake kwa:

- Kuzingatia maslahi mengineyo au mipango yenye maslahi thabiti ya kifedha;
- Kuhakikisha kuwa ufanisi wa wajumbe wa Bodi unatathminiwa;
- Kupitia sera za kupandisha vyeo, kuhamisha na kusitisha ajira kwa niaba ya Kundi la makampuni;
- Kufuatilia ukubwa na muundo wa wajumbe wa Bodi;
- Kufanya tathmini ya kila mwaka ya uhuru wa wakurugenzi katika kutekeleza majukumu yao;
- Kupendekeza majina ya watu kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi na kamati zake;
- Kupitia mipango ya Bodi ya kuhakikisha kuna utaratibu wa uongozi endelevu;
- Kutathmini muundo na ufanisi wa bodi za kampuni tanzu;
- Kupitisha uteuzi kwenye bodi za kampuni tanzu; kuhakikisha kuwa wajumbe wa Bodi wana sifa stahiki kwa nafasi zao;
- Kupitia muundo wa Kampuni ili kuhakikisha kuwa unafaa kutekeleza mkakati na malengo ya muda mrefu ya kibiashara; na
- Kuhakikisha sheria na kanuni husika zinafuatwa.

### Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji (ARCC)

Kamati hii ina wajibu wa:

- Kupitia matokeo ya muda ya pamoja, matokeo ya awali, taarifa za mwaka na taarifa za pamoja za fedha za Kampuni na taarifa za fedha za kampuni tanzu;
- Kufuatilia utekelezaji wa sheria husika na Kanuni za Soko la Hisa la Dar es Salaam;
- Kuripoti kwenye Bodi kuhusu usahihi na ubora wa sera na taratibu za hesabu za Kampuni, ikijumuisha sera na taratibu muhimu za uhasibu;
- Kusimamia michakato ya kutoa taarifa za mwaka za fedha;
- Kutathmini uteuzi na/au kusitisha huduma ya wakaguzi wa nje, pamoja na ada zao za ukaguzi, uhuru na usahihi wa mchakato wa ukaguzi na kuamua aina za huduma nyingine zisizo za kikaguzi;
- Kupitisha mpango wa ukaguzi wa ndani wa mwaka;
- Kupokea na kushughulikia ipasavyo malalamiko, ya nje na ndani, yanayohusiana na taratibu za uhasibu na ukaguzi wa ndani au kuhusu maudhui au ukaguzi wa kampuni zote ambazo taarifa zake zipo ndani ya taarifa za pamoja za fedha na taarifa nyingine zinazowiana nazo za Kampuni;
- Kupitia na kufuatilia namna uongozi wa Kampuni unavyo shughulikia na kuripoti masuala yanayohusiana na kodi;
- Kufuatilia shughuli na michakato ya usimamizi wa dharura na kutathmini dharura muhimu zaidi za Kampuni; na
- Kufuatilia ufanisi wa michakato ya kujenga utayari na uelewa wa sheria na kanuni husika ili kuhakikisha kuwa menejimenti inazitekeleza.

## Michango ya Kisiasa na Kujitolea

Kampuni haikutoa michango yoyote ya kisiasa mwaka huu (2020: hakuna). Mwaka huu kampuni haikutoa mchango kwa Vodacom Tanzania Foundation (2020: shilingi milioni 315).

## Wajibu wa Kampuni kwa jamii

Vodacom Tanzania Foundation ('Vodacom Foundation') ni kampuni yenye dhima ya ukomo kwa dhamana iliyosajiliwa na yenye makao yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni, 2002 Sura ya 212 ya sheria za Tanzania.

Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Makampuni, 2002 na Sheria iliyofanyiwa Marekebisho Madogo, No. 3 ya 2019 ambayo imeanza kutumika tarehe 30 Juni 2019, mamlaka ya kusajili makampuni ambayo hayakusudii kuendesha biashara kwa faida, yalihamishwa kutoka BRELA kwenda kwa Msajili wa Asasi Zisizo za Kiserikali ('AZISE'). Hivyo, BRELA ilitoa tangazo kwa umma kuwa kuanzia tarehe 30 Agosti 2019, Msajili wa Makampuni hatatunza kumbukumbu za kampuni yoyote ambayo hayaruhusiwi kugawa faida kutokana na biashara, na wakashauri kampuni zilizoguswa na mabadiliko hayo kuwasiliana na Msajili wa AZISE ili wapatiwe mwongozo na maelekezo kuhusiana na usajili wa AZISE kulingana na Sheria ya Marekebisho Madogo, Na. 3 ya 2019.

Vodacom Foundation iliathiriwa na mabadiliko haya ya sheria kwa kuwa iliandikishwa kama kampuni yenye dhima ya ukomo kwa udhamini isiyokuwa na malengo ya kutengeneza faida. Hivyo ilifutwa kwenye Usajili wa Makampuni tarehe 30 Agosti 2019. Taasisi mbadala iitwayo Vodacom Tanzania Foundation, ilisajiliwa na Msajili wa AZISE katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mujibu wa Sheria ya Asasi Zisizokuwa za Kiserikali ya 2002 (iliyorekebiswa mwaka 2005) na Kanuni za Asasi Zisizokuwa za Kiserikali (Iliyorekebishwa) ya 2018 (kwa pamoja, Sheria na Kanuni za AZISE) za Tanzania.

Vodacom Foundation ni 'mkono' wa kampuni wa uwajibikaji kwa umma. Madhumuni yake ni kuleta manufaa kwa umma kupitia matumizi ya teknolojia ya simu za kiganjani ili kuboresha maisha ya jamii.

Vodacom Foundation inashirikiana na AZISE za ndani, asasi za kiraia, asasi za kijamii na mashirika yasiyozalisha faida kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha elimu, afya na ushirikishwaji kifedha kwa kulenga vikundi vya watu walio katika mazingira magumu.

Tangu kuzinduliwa hadi leo, Vodacom Foundation imewekeza shilingi milioni 16 150 (2020: shilingi milioni 16 150) katika kuboresha jamii ya Tanzania. Mwaka huu, Bodi imeamua kufunga asasi hii na badala yake shughuli zake zitaendeshwa na kampuni mama.

## Tahadhari ya Madeni

### Masuala ya kodi

Tozo ya kodi siku zijazo, kiwango cha kodi na faida kabla ya kodi ni mambo yanayoweza kuathiriwa na mambo mbalimbali ambayo ni pamoja na marekebisho ya mfumo wa kodi yanayofanyika nchini na utatuzi wa migogoro ya kodi iliyopo Mamlaka ya Kodi Tanzania ('TRA' au 'mamlaka ya kodi') na/au mahakama za kodi.

Kampuni imedhamiria kuendelea kushughulikia masuala yote ya kodi kwa uaminifu na uwazi ikiwa ni pamoja na sera ya uwazi kwa mamlaka ya kodi na ulipaji wa kodi zote zinazotakiwa kulipwa kwa mujibu wa sheria husika za kodi nchini.

Kampuni hufanyiwa ukaguzi mara kwa mara na kukadiriwa na mamlaka ya mapato kutokana na taarifa zake za kodi ya mapato na kodi nyinginezo.

Matokeo ya mapitio hayo ni kuwa katika baadhi ya matukio, migogoro inaweza kutokea na mamlaka ya mapato kuhusu tafsiri au matumizi ya kanuni fulani za kodi ambapo sheria hizi za kodi zina maana nyingi na zinaweza kuwa na mawanda mapana ya tafsiri.

Ili kushughulikia na kudhibiti hali ya uwezekano wa masuala ya kodi kuwa na tafsiri zinazotofautiana na hivyo kukosa uhakika wa usahihi, utawala bora ni muhimu kutumika ili kuwa na biashara endelevu. Hivyo, misimamo mikuu iliyochukuliwa kuhusu kodi hupitiwa na uongozi na kutolewa taarifa kwenye Bodi.

Kampuni hutumia msaada wa washauri wa nje wa kodi ili kuthibitisha usahihi wa msimamo uliochukuliwa kuhusiana na masuala muhimu ya kodi kuhusu matumizi na tafsiri za sheria ya kodi.

Kampuni imezingatia masuala yote ya migogoro na mamlaka ya kodi na kuripoti katika vitabu na taarifa za fedha uwezekano wowote wa madeni ya ziada kutokana na masuala ya kodi palipo na uwezekano wa hilo kutokea, wakati migogoro bado ikisuluhishwa. Kampuni haitoi kwa undani taarifa zote zinazohusu migogoro ya kodi iliyopo kwa sababu masuala hayo bado yapo katika mchakato wa usuluhishi.

Ifuatayo ni migogoro iliyopo ya kodi ambayo inaweza ikasababisha madeni ya kikodi iwapo Kampuni itashindwa katika mashauri yake. Athari za kifedha za migogoro hiyo hazijajumuishwa kama sehemu ya taarifa hii ya fedha.

- **Punguzo la kodi kutokana na uchakavu wa mitambo**
  Migogoro iliyopo ya kodi inayohusu uainishaji wa vifaa vya mawasiliano ya simu kwa ajili ya ukokotoaji wa kodi bado ipo mahakamani. TRA haikubaliani na namna Kampuni ilivyotafsiri uainishaji wa vifaa vya mawasiliano ya simu kulingana na Sheria ya Kodi ya Mapato. Hata hivyo, suala hili linahusu tofauti ya wakati wa kutambua punguzo la kodi, katika miaka ijayo makadirio haya yanaweza kuzidi iwapo Kampuni haitafanikiwa kupata usuluhishi wa shauri hilo, jambo ambalo pia litasababisha kupewa adhabu na tozo za ziada na TRA.

## **Tahadhari ya Madeni** inaendelea

- **Kodi ya zuio katika huduma za setilaiti, kuzuru kimataifa na mkongo uliopita chini ya bahari**
  Makadirio yaliyopokelewa na kampuni kuhusiana na kodi ya zuio katika huduma za setilaiti, kuzuru kimataifa na huduma za mkongo uliopita chini ya bahari zilizotolewa na watoa huduma wa kimataifa, pia yapo katika mchakato mahakamani.

  Kampuni haikukata kodi ya zuio kwenye malipo yaliyofanywa kwa watoa huduma wa kimataifa wa huduma hizi za mawasiliano ya simu kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa 'International Telecommunication Union' ('ITU') na imesaini makubaliano na ITU ambayo yameweka utaratibu unaozuia kukatwa kodi mara mbili kwa huduma za mawasiliano ya simu. Kampuni imetoa ushahidi (uthibitisho) wa makubaliano hayo baina ya ITU na Tanzania.

- **Usahihi wa Bei za huduma kutoka kwa kampuni washirika**
  Kampuni, ikiwa ni sehemu ya kampuni ya kimataifa, inatumia sana huduma zinazotolewa na kampuni washirika kwa namna ambayo inaongeza ufanisi, huku miamala ya huduma hizi ikifanyika kwa kanuni za soko. Miamala hii imeandikwa katika nyaraka za Kampuni zinazohusu bei za huduma kutoka kwa kampuni washirika kwa mujibu wa kanuni za ndani na miongozo ya OECD. TRA imefanya ukaguzi wa miamala hiyo kwa kipindi kati ya mwaka 2015 hadi 2017 ambapo baadhi ya vipengele vimekuwa na mgogoro kuhusu njia iliyotumika na namna vipengele vingine vya kanuni za kukubaliana bei ya huduma kwa kampuni washirika, vilivyotumika.

### Mashauri yaliyo mahakamani na madai mengine

Kwa sasa Kampuni ina mashauri mbalimbali ya kisheria yaliyo mahakamani na imetathmini matokeo ya mashauri hayo kwa kushauriana na mshauri wake wa kisheria. Kufuatia tathmini hii, menejimenti ya Kampuni imeridhika na hatua zilizochukuliwa ikiwemo tahadhari ya madeni kwenye vitabu vya fedha kuhusiana na mashauri haya.

Kampuni pia ina mashtaka ya madai kutokana na mikataba mbalimbali iliyoingia na wabia wake wa biashara. Migogoro inaweza ikaibuka kuhusiana na tafsiri au matumizi ya vifungu vya makubaliano ya mkataba. Migogoro hii inaweza ikaamuliwa kinyume na matarajio ya Kampuni na hivyo kuisababisha Kampuni kuwajibika. Menejimenti imetathmini kuwa hakuna uhakika wa kutosha katika madai yaliyopo, unaolazimu Kampuni kurekodi tahadhari ya madeni ambayo inaweza kulazimika kuyalipa. (2020: Hakuna).

## Masuala mengine

### Notisi za Dharura za Mamlaka ya Mapato Tanzania

Mnamo Julai na Agosti 2020, TRA ilitoa notisi mbili za dharura dhidi ya akaunti za benki za Kampuni za shilingi bilioni 2.9 na shilingi bilioni 17.5. Notisi hizo za dharura zilitaka benki kulipa fedha hizo haraka. Notisi hizo zilitekelezwa kikamilifu licha ya jitihada za Kampuni kujieleza na kuonyesha TRA kuwa kiasi cha fedha hizo katika notisi ya dharura hakikuwa sahihi na vilevile ukweli kuwa masuala yanayohusiana na fedha hizo bado yako mahakamani.

Kampuni inafuatilia michakato ya kisheria na vilevile kuishirikisha TRA na mamlaka nyingine za serikali kusuluhisha suala hili.

### Usajili wa wateja kwa alama za vidole

Mnamo tarehe 1 Mei 2019, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa miongozo mipya inayoagiza kuwa usajili halali wa wateja ni ule wa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN) kilichotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). TCRA iliagiza usajili kwa kutumia eKYC usitishwe. Kampuni kwa kushirikiana na wadau wengine katika sekta imeendelea kushirikiana na TCRA kuhakikisha inatekeleza maelekezo ya kanuni hizo mpya za usajili. Makampuni ya simu kwa kushirikiana na TCRA na NIDA yalizindua kampeni nchini kote kuielimisha jamii ili kuharakisha usajili kwa utaratibu huu mpya.

Mchakato wa usajili kwa alama za vidole ulianza mwezi Mei 2019, na kutakiwa kukamilika ifikapo Desemba 2019, hata hivyo muda uliongezwa hadi tarehe 20 Januari 2020. Idadi ndogo ya watu waliokuwa na Vitambulisho vya Taifa nchini kote uliathiri mchakato huo.

Kama ilivyoelezwa kwenye taarifa za pamoja za fedha za Kampuni zilizoishia tarehe 31 Machi 2021, hadi kufikia tarehe 20 Januari 2020, Kampuni haikuwa imekamilisha usajili kwa baadhi wateja. Baada ya muda ulioongezwa kuisha tarehe 20 Januari 2020, TCRA iliagiza kusitishwa kwa awamu, huduma za simu kwa wateja ambao hawajakamilisha usajili. Hii ilipelekea Kampuni kuwafungia huduma wateja milioni 2.9 kati ya tarehe 20 Januari na tarehe 31 Machi 2020. Inakadiriwa kuwa kati ya wateja hao takribani wateja 793 000 walisajiliwa kwa alama za vidole na laini zao kuunganishiwa tena huduma.

Zoezi hili liliathiri mapato ya Kampuni ya mwaka kwa ujumla. Jambo hili, pamoja na ongezeko la gharama zilizotumika katika mchakato wa kusajili upya laini za simu, vimeathiri matokeo ya kifedha ya Kampuni. Kampuni inaendelea na mchakato wa kusajili laini za simu kwa kushirikiana na TCRA na wenzetu katika sekta kuhakikisha laini zote za simu zinasajiliwa upya.

### Mabadiliko mengine katika kanuni za usajili wa laini za simu

Mnamo tarehe 1 Mei 2019, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa miongozo mipya inayoagiza kuwa usajili halali wa wateja ni ule wa kutumia Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN) kilichotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kama kitambulisho pekee kinachokubalika.

## **Masuala mengine** inaendelea

**Mabadiliko mengine katika kanuni za usajili wa laini za simu** inaendelea

Tarehe 7 Februari 2020, Serikali ilichapisha Kanuni mpya za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Usajili wa Laini za Simu) 2020. Kanuni hizo zimeeleza mchakato wa usajili kwa alama za vidole kwa kutumia kitambulisho cha Taifa, kama kitambulisho pekee kwa usajili wa laini za simu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kufikia tarehe 31 Machi 2021 jumla ya laini milioni 1.1 zinazozalisha mapato ya shilingi bilioni 2.9 kwa mwezi hazikuwa zimesajiliwa kwa alama za vidole. Tunaendelea kuwashirikisha NIDA kuhakikisha wateja hawa wanapatiwa vitambulisho vya taifa, na pia TCRA kwa madhumuni ya kuongeza muda wa usajili ili kuwapa nafasi wateja ambao hawajapata vitambulisho vya taifa.

Tarehe 1 Julai 2020, TCRA ilichapisha tangazo kwa umma linalowataka wateja ambao wamesajiliwa kwa alama za vidole na waliosajili zaidi ya laini moja katika kampuni moja ya simu, kuhakiki laini zao za simu kupitia simu zao za kiganjani. Baada ya hapo, TCRA na kampuni za simu ziliweka utaratibu wa kuthibitisha umiliki wa laini za ziada ambao unawawezesha wateja kupitia simu zao kuomba laini za simu za ziada kwa kutembelea maduka ya kampuni za simu au kupitia (USSD). Wateja wanaruhusiwa kumiliki hadi laini 5 za simu iwapo watafuata mchakato sahihi wa uthibitisho. Tunaendelea kuendesha kampeni za kujenga ufahamu kwa wateja kuhusu mchakato wa uhakiki wa laini za simu.

Mwaka huu, NIDA imeingia mkataba na kampuni zote za simu kutoza shilingi 500, kuanzia tarehe 1 Agosti 2020, kwa ajili ya kutumia taarifa za kanzidata ya NIDA kwa ajili ya kuhakiki wateja wao, kulingana na Kanuni za Usajili na Utambuzi wa Watu 2014. Vodacom Tanzania PLC pamoja na kampuni nyingine za simu zinashirikiana na Serikali kupitia TCRA, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia kwa madhumuni ya kupunguza tozo hii.

**Marekebisho ya bei ya data**

Tarehe 4 Machi 2021, TCRA ilitoa kanuni na maelekezo mapya ambayo yamepanga bei ya rejareja ya juu na chini kwa huduma za data kutumika kuanzia tarehe 2 Aprili 2021. Bei za chini za data zilipangwa kuwa shilingi 2.03 kwa Mb na bei ya juu shilingi 9.35 kwa Mb ikijumuisha kodi. Kanuni za bando pia zilitaka kampuni za simu kuwa na bando za ndani zisizozidi 50. Tarehe 2 Aprili 2021, Vodacom Tanzania PLC pamoja na kampuni nyingine za simu zilitekeleza maagizo kutoka TCRA. Baada ya kutekeleza, TCRA ikaagiza kampuni za simu kurudisha viwango vya bando vilivyokuwa hapo awali. Tunaendelea kuwasiliana na TCRA, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia na Taasisi zingine za Serikali kuhusu umuhimu wa mageuzi ya sekta. Tunaamini kuwa, mageuzi haya yataendeleza uwekezaji wa mtaji nchini ambao utachochea ujumuishaji kidigitali na kifedha.

**Maagizo ya utekelezaji na adhabu**

Tarehe 5 Mei 2020, TCRA ilitoa agizo la utekelezaji dhidi ya Kampuni na kampuni zingine za simu. Kufuatia Kampuni kujitetea tarehe 12 Juni 2020, TCRA iliitoza Kampuni adhabu ya shilingi milioni 400 kwa msingi kwamba Kampuni ilishindwa kuonesha kwa uwazi vigezo na masharti na kutekeleza matumizi ya bando mpya kabla ya kuisha bando iliyokuwepo. Kampuni imelipa faini na itahakikisha inafuata maelekezo ya TCRA.

Mnamo Agosti 2020, TCRA iliiandikia Kampuni barua kuhusu ukiukwaji wa taratibu kwa kueleza kuwa kati ya Mei 2020 na Juni 2020, Kampuni ilitoza viwango vya huduma ya kuunganishwa simu kimataifa chini ya kiwango cha kisheria US$ 0.25 kinyume na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (mawasiliano ya simu) 2018. Kampuni iliwasilisha maelezo ya ufafanuzi TCRA kuonyesha utekelezaji wake wa kanuni.

Kufuatilia tathmini ya ubora wa huduma iliyofanywa na TCRA kwa kipindi cha Septemba hadi Desemba 2020, kampuni zote za simu zilitozwa faini ya shilingi bilioni 38 kutokana na kushindwa kufikia viwango vya ubora wa huduma. Kwa upande wake, Kampuni ilipigwa faini ya shilingi bilioni 7.8 kwa kushindwa kufikia viwango 3 kati ya 102 vilivyopimwa. Hata hivyo, badala ya kulipa faini, Kampuni iliingia makubaliano na TCRA kuwekeza thamani sawa na faini hiyo kwenye kuboresha mtandao wake ili kuongeza ubora wa huduma.

## Matukio baada ya muda wa ripoti hii

Matukio baada ya muda wa ripoti hii yameelezwa katika Maelezo 43 (nakala ya kiingereza) katika taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za Kampuni. Bodi haina taarifa ya suala au mazingira mengine yoyote yaliyoibuka tangu mwisho wa muda wa kuripoti ambayo yalipaswa kuripotiwa katika taarifa hii, na kuhitaji kufanyiwa marekebisho au kufafanuliwa kwenye taarifa za pamoja au binafsi za fedha.

## Mkaguzi wa hesabu

Ernst & Young, mkaguzi wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2021, ameonyesha utayari wa kuendelea kufanya kazi nasi na ana sifa za kuteuliwa tena. Azimio la kupendekeza kuteuliwa tena kwa Ernst & Young kama mkaguzi wa hesabu za Kampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2022 litapelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka.

## Taarifa za pamoja za fedha na taarifa binafsi za fedha za kampuni

Taarifa za fedha za Kampuni na kampuni tanzu kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 zilipitishwa na kuidhinishwa na Bodi kwa ajili ya kuchapishwa tarehe 31 Mei 2021.

Kwa agizo la Bodi

| | |
|---|---|
| **Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo** | **Hisham Hendi** |
| Mwenyekiti | Mkurugenzi |

# Tamko la majukumu ya wakurugenzi

## Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021

Sheria ya Makampuni, 2002 Na.12 ya Tanzania inawataka wakurugenzi kuandaa taarifa za pamoja za fedha na taarifa za fedha za kampuni moja moja kwa kila mwaka wa fedha ambazo zinaonyesha ipasavyo hali ya kifedha na matokeo ya Kampuni tanzu na Kampuni. Wakurugenzi pia wanatakiwa kuhakikisha kuwa Kampuni na kampuni tanzu zinatunza kumbukumbu sahihi za hesabu za fedha ambazo zinaeleza kwa usahihi wa kutosha, hali ya kifedha na matokeo kwa Kampuni na kampuni tanzu. Wakurugenzi pia wana jukumu la kulinda mali za Kampuni na kampuni tanzu na kuchukua hatua madhubuti za kugundua na kuzuia ulaghai, makosa yasiyo kusudiwa na mambo mengine yasiyo sawa.

Wakurugenzi wanakubali wajibu wa kuandaa taarifa za fedha za Kampuni na kampuni tanzu, ambazo zimeandaliwa kwa kuzingatia sera sahihi za uhasibu zikichangiwa na maamuzi na makadirio ya kimantiki, kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Kuripoti Masuala ya Kifedha ('IFRS") na masharti ya Sheria ya Makampuni Na 12, ya mwaka 2002. Wakurugenzi wanaamini kuwa taarifa za fedha za Kampuni na kampuni tanzu zinawasilisha kwa usahihi, katika hali zote, hali ya kifedha na matokeo ya kifedha ya kampuni hizo kulingana na kanuni za IFRS na masharti ya Sheria ya Makampuni, Na 12, ya mwaka 2002. Wakurugenzi pia wanakubali wajibu wa kutunza kumbukumbu za fedha ambazo zinaweza kutegemewa katika maandalizi ya taarifa za fedha za Kampuni na kampuni tanzu na vilevile kuandaa, kutekeleza na kusimamia uwepo wa mazingira ya usimamizi wa ndani unaowezesha kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha ambazo hazina upotoshaji utokanao na udanganyifu au makosa yasiyokusudiwa.

Hakuna dalili yoyote ambayo wakurugenzi wameiona inayoashiria kuwa Kampuni na kampuni tanzu hazitaweza kuendelea na shughuli zake za biashara ndani ya kipindi cha walau miezi kumi na miwili ijayo kutoka tarehe ya tamko hili.

Taarifa ya fedha ya Kampuni na kampuni tanzu kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 zilithibitishwa na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 31 Mei 2021.

**Jaji (Mstaafu) Thomas B Mihayo**
Mwenyekiti

**Hisham Hendi**
Mkurugenzi Mtendaji

# Tamko la mkuu wa kitengo cha fedha

## Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) kulingana na mamlaka ya sheria ya Wakaguzi na Wahasibu (Usajili) Na. 33 ya 1972, kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 2 ya 1995, inataka tamko la Mkuu wa Kitengo cha Fedha anayehusika na kuandaa taarifa za fedha za kampuni husika liambatanishwe na taarifa za fedha.

Ni wajibu wa mtaalamu wa uhasibu kuisaidia Bodi ya Wakurugenzi kutekeleza wajibu wa kuandaa taarifa za fedha za kampuni zikionesha muonekano sahihi wa hali ya kifedha na ufanisi kwa mujibu wa matakwa ya IFRS na masharti ya sheria ya Makampuni, 2002 Na.12.

Kulingana na sheria, jukumu la kuandaa taarifa za fedha lipo kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoelezwa katika tamko la majukumu ya Wakurugenzi katika ukurasa uliotangulia.

Mimi, **Robin Kimambo**, nikiwa **Mkuu wa Kitengo cha Fedha** wa Vodacom Tanzania Public Limited Company ninatambua jukumu langu la kuhakikisha kuwa taarifa za fedha za kampuni na kampuni tanzu kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 zimeandaliwa kwa mujibu wa matakwa ya IFRS na masharti ya sheria ya Makampuni, 2002 Na.12 ya Tanzania.

Hivyo ninathibitisha kuwa taarifa za fedha za Kampuni na kampuni tanzu zinaonesha kwa usahihi hali ya kifedha ya Vodacom Tanzania Public Limited Company kwa tarehe hiyo na kuwa zimeandaliwa kwa kutumia kumbukumbu za fedha zilizotunzwa kwa usahihi.

**Robin Kimambo**
Namba ya Uanachama wa NBAA: GA4810
Mkuu wa kitengo cha fedha

31 Mei 2021

# Taarifa ya Mkutano Mkuu

**Vodacom Tanzania Public Limited Company**
(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

**Taarifa inatolewa kuwa, mkutano mkuu wa tano wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba 2021 kuanzia saa tano asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:**

## 1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa nne uliofanyika tarehe 30 Oktoba 2020.

**Azimio la kawaida namba 1**

'ILIRIDHIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa nne uliofanyika tarehe 30 Oktoba 2020 zimethibitishwa.'

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni **https://vodacom.co.tz/investors**

## 2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za jumla na binafsi zilizokaguliwa za fedha za Kampuni, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021.

**Azimio la kawaida namba 2**

'ILIRIDHIWA KUWA taarifa za jumla na binafsi zilizokaguliwa za fedha za Kampuni, pamoja na ripoti ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021, zimepokelewa na kupitishwa.'

Taarifa ya mwaka inapatikana katika tovuti ya Kampuni **https://vodacom.co.tz/investors**

## 3. Uchaguzi wa wakurugenzi

Kwa kupitia maazimio tofauti:

3.1 Ndg. Raisibe Morathi aliteuliwa kuwa mkurugenzi kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi hadi mkutano wa kawaida unaofuata. Wasifu wa Ndg. Morathi upo katika ukurasa wa 46.

3.2 Ndg. Sitholizwe Mdlalose aliteuliwa kuwa mkurugenzi kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi hadi mkutano wa kawaida unaofuata. Wasifu wa Ndg. Mdlalose upo katika ukurasa wa 46.

**Azimio la kawaida namba 3**

'ILIRIDHIWA KUWA Bi Raisibe Morathi amechaguliwa kuwa mkurugenzi wa Kampuni.'

**Azimio la kawaida namba 4**

'ILIRIDHIWA KUWA Bw Sitholizwe Mdlalose amechaguliwa kuwa mkurugenzi wa Kampuni.'

3.3 Ndg. Diego Guiterrez, Ndg. Jacques Marais, Ndg. Kenneth Gomado na Ndg. Matimba Mbungela wanapaswa kustaafu katika mkutano huu kwa mujibu wa ibara 104 na 105 za Katiba ya Kampuni. Ibara hizo zinabainisha kuwa licha ya kustaafu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi. Wasifu wao upo katika ukurasa wa 46 na 47.

**Azimio la kawaida namba 5**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Diego Gutierrez amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi wa Kampuni.'

**Azimio la kawaida namba 6**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Jacques Marais amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi wa Kampuni.'

**Azimio la kawaida namba 7**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Kenneth Gomado amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi wa Kampuni.'

**Azimio la kawaida namba 8**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Matimba Mbungela amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi wa Kampuni.'

## 4. Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakaguzi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka.

**Azimio la kawaida namba 9**

'ILIRIDHIWA KUWA Ernst & Young Inc. wameteuliwa kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka.'

## 5. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa kifungu cha 32(f) cha Katiba ya Kampuni, Ndg. Margaret Ikongo, Ndg. Thembeka Semane na Ndg. Winifred Ouko wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, wachaguliwe kuendelea kuwa wajumbe wa kamati tajwa. Wasifu wao upo katika ukurasa wa 47.

**Azimio la kawaida namba 10**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Winifred Ouko amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji.'

**Azimio la kawaida namba 11**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Thembeka Semane amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji.'

**Azimio la kawaida namba 12**

'ILIRIDHIWA KUWA Ndg. Margaret Ikongo amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji.'

## 6. Gawio

Kuthibitisha kuwa hakutakuwa na malipo ya gawio kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2021.

**Azimio la kawaida namba 13**

"ILIRIDHIWA KUWA hakutakuwa na malipo ya gawio kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2021.

## 7. Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 481 000 kuanzia tarehe 1 Novemba 2021 hadi hitimisho la mkutano mkuu ujao wa mwaka, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni. Hakuna mapendekezo ya mabadiliko ya ada.

**Azimio la kawaida namba 14**

'ILIRIDHIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 481 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:

| | Pendekezo la ada Dola ya Marekani[1] | Ada ya sasa Dola ya Marekani |
|---|---|---|
| Mwenyekiti wa Bodi | 150 000 | 150 000 |
| Mjumbe wa Bodi | 30 000 | 30 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | 15 000 | 15 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | 8 000 | 8 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira | 12 000 | 12 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ujira | 4 000 | 4 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi | 3 000 | 3 000 |

[1] Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi zote pamoja na kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wakazi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka kwa mikutano ya kawaida isiyopungua minne kwa mwaka, mikutano maalum motets na Mkutano Mkuu wa Mwaka na wa dharura kama itahitajika.

# Wasifu wa Wajumbe wa Bodi



## Raisibe Morathi (51)

**Mkurugenzi asiye mtendaji**
**Afisa Mkuu wa Fedha – Vodacom Group Limited**
**Mjumbe wa kamati ya Uongozi ya Vodacom Group**

*Shahada ya Uzamili ya Filosofia, Stashahada ya juu ya masuala ya kodi kutoka Chuo Kikuu cha Wits, Mhitimu wa programu ya menejimenti ya INSEAD (Ufaransa), Cheti cha Taaluma ya Uhasibu ya Afrika Kusini (CA, SA).*

Raisibe aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa Vodacom Group Limited kuanzia tarehe 1 Novemba 2020. Alijiunga na Vodacom akitokea Nedbank Group ambapo alikuwa Afisa Mkuu wa Fedha tangu Septemba 2009. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 27 katika huduma za fedha katika mashirika mbalimbali makubwa huko Afrika Kusini, ikiwa ni pamoja na Nedbank Group, Sanlam Group na Industrial Development Corporation. Raisibe pia ni mkurugenzi asiye mtendaji wa bodi za Vodacom Afrika Kusini na Safaricom PLC.



## Sitholizwe Mdlalose (41)

**Mkurugenzi Mtendaji - Vodacom Tanzania PLC**
**Mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Vodacom Tanzania PLC**

*Shahada ya Uhasibu (BCompt), Chuo Kikuu cha Afrika Kusini*
*Mwanachama wa Shirikisho la Wanataaluma ya Uhasibu, Uingereza (ACCA).*
*Mhitimu wa Programu ya Uongozi, Shule ya Biashara Harvard.*

Sitholizwe aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc mwezi Agosti 2021. Amejiunga na Vodacom Tanzania akitokea Vodacom South Africa (VSA) ambapo alikuwa mkurugenzi wa fedha tangu mwaka 2017. Sitholizwe ameshika nafasi mbalimbali za juu za uongozi ndani ya Vodacom Group zikiwemo Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha pamoja na Afisa Mkuu wa Fedha wa Vodacom International Business. Kabla ya hapo, Sitholizwe alikuwa Vodafone Group kwa zaidi ya miaka 6 akishikilia nafasi mbalimbali za uongozi wa juu. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 19 katika fani ya usimamizi na ushauri wa fedha; ambayo miaka 13 akiwa katika sekta ya mawasiliano ya simu ya masoko yaliyokua pamoja na yale yanayoibukia.



## Diego Gutierrez (45)

**Mkurugenzi asiye mtendaji**
**Afisa Mkuu wa Uendeshaji: Vodacom International Business**
**Mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Vodacom Group**

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na Masoko, Chuo Kikuu cha Católica, Bolivia.*

Diego Gutierrez aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa Vodacom International Business kuanzia tarehe 1 Agosti 2017. Diego ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika shughuli za kimataifa katika sekta ya mawasiliano ya simu hususan kwenye masoko yanayoibukia huko Latini Amerika, Afrika na visiwa vya Karibi. Ana uzoefu uliothibitika wa kufanya mageuzi ya kibiashara na kuwezesha ongezeko la ufanisi wa uendeshaji, kupitisha makampuni katika vipindi vigumu vya mabadiliko na kutafsiri mikakati ya mashirika kuwa matokeo ya uendeshaji yanayoonekana.



## Jacques Marais (55)

**Mkurugenzi wa Fedha – Vodacom Tanzania**
**Mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Vodacom Tanzania PLC**

*Shahada ya Biashara katika Uhasibu (Hons), Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini.*
*Cheti cha Taaluma ya Uhasibu ya Afrika Kusini (CA, SA).*

Jacques aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania mwezi Julai 2016. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika masuala ya fedha na amekuwa mhimili muhimu katika kuyaongoza makampuni katika changamoto mbalimbali za masuala ya kodi, uchumi na ushindani wa kibiashara. Uzoefu wake umethibitika katika kufikia malengo ya ongezeko la faida katika masoko yanayokua kwa kufanya uwekezaji sahihi wa mtaji na kushusha gharama za uendeshaji.



## Kenneth Kwame Gomado (43)

**Mkurugenzi wa Bodi asiye mtendaji Afisa Mkuu wa Fedha – Vodacom International Business**

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Cape Town, Afrika Kusini.*
*Mwanachama wa Shirikisho la Wanataaluma ya Uhasibu, Uingereza (ACCA).*

Kenneth ni Afisa Mkuu wa Fedha wa Vodacom International Business mwaka 2018. Kabla ya kujiunga na Vodacom International Business, alikuwa Afisa Mkuu Fedha wa Vodafone Ghana tangu 2014. Alijiunga na Kundi la Kampuni za Vodafone mwaka 2011, baada ya kupata uzoefu mpana katika huduma za ushauri wa ukaguzi na bidhaa za walaji zinazouzika haraka. Kenneth ana uzoefu wa uendeshaji katika mazingira yenye changamoto za kiudhibiti na kodi, kuleta mafanikio ya kibiashara, kupunguza gharama na kutoa maamuzi makini katika uwekezaji wa mtaji.



## Matimba Mbungela (49)

**Mkurugenzi wa Bodi asiye mtendaji**
**Afisa Mkuu Rasilimali Watu wa Vodacom Group Limited**
**Mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Vodacom Group Limited**
**Mkurugenzi wa Vodacom (Pty) Limited**

*Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Kwazulu Natal, Shahada ya Utawala, Chuo Kikuu cha Venda, Stashahada ya Juu ya Rasilimaliwatu, Chuo Kikuu cha Cape Town, Mhitimu wa Programu ya Vodafone kwenye ubora wa masuala ya rasilimaliwatu.*

Matimba ni Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Vodacom Group. Kabla ya kushika nafasi hii, alikuwa Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Vodacom South Africa hadi Aprili 2014. Matimba amefanya kazi ndani ya Vodacom/Vodafone Group tangu 2003 akishikilia nafasi mbalimbali katika Kitengo cha Rasilimaliwatu. Kwa miaka mitatu alifanya kazi Vodafone kama Mkuu wa Kanda ya Afrika, Mashariki ya Kati na Asia Pasifiki "AMAP" akihusika na Ufanisi na Mabadiliko na pia kama Mkuu wa Vipaji wa Kanda. Kabla ya hapo alikuwa anashughulikia Usimamizi wa Vipaji katika Vodacom kwa miaka sita ambapo alitekeleza kwa mafanikio kujumuishwa kwa mkakati wa vipaji katika mkakati wa dunia wa Vodafone. Uzoefu wake wa siku za nyuma ni pamoja na kufanya kazi za Afisa Rasilimaliwatu katika kampuni za BMW Afrika Kusini na Unilever. Matimba anawakilisha Vodacom Employee Trust ('Siyanda') katika Bodi ya YeboYethu, pia ni Mkurugenzi Asiye Mtendaji wa Vodacom Msumbiji na Vodacom Lesotho. Matimba aliteuliwa katika Bodi ya Ushauri ya Unisa GSBL tarehe 1 Juni 2020.



## Margaret Ikongo (63)

**Mkurugenzi huru**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii**

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na masuala ya Fedha, Chuo Kikuu Huria Tanzania.*
*Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa ViashiriaHatarishi, Uingereza.*
*Diploma ya Kimataifa ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Mjumbe Mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa ViashiriaHatarishi, Uingereza.*
*Mjumbe katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza.*

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya AAR Insurance Tanzania. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Bodi ya NMB Bank PLC. Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika sekta ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.



## Thembeka Semane (45)

**Mkurugenzi huru**
**Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii**

*Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon, Afrika Kusini*
*Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini.*

Thembeka aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeka ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuatiliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeka ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Udhibiti ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini na pia ni mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeka anafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimaliwatu na Ujira. Pia ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Dharura na Kamati ya Ujira ya Mbuga za Wanyama za Afrika Kusini. Vilevile, Thembeka ni mjumbe wa South African Heritage Resource Agency na Kamati ya Uthibiti na Usimamizi wa Utendaji wa Manispaa ya Sol Platje.



## Winifred Ouko (51)

**Mkurugenzi huru**
**Mjumbe wa Kamati ya Ujira**
**Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi**
**Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha katika kamati hii.**

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Cornell, Marekani.*
*Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Uhasibu, Kenya.*

Winnie aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Winnie ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha katika makampuni na miradi. Winnie ni Mkurugenzi Mtendaji wa Lattice Consulting, akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 wa kutoa huduma za ushauri katika masuala ya fedha, pamoja na mikakati na mafunzo kwa wateja ndani ya Afrika na Amerika Kaskazini. Winnie ni mjumbe wa bodi ya Kenya Water Pool Fund pia ni mkurugenzi asiye mtendaji wa Safaricom.

## Tarehe ya kufunga rejesta

Tarehe ya kufungwa rejesta ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhudhuria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Jumatano tarehe 6 Oktoba 2021.

## Kushiriki kwa njia ya kielektroniki

Mkutano mkuu utafanyika kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye kifungu 29 na 63 cha Katiba ya Kampuni.

Wanahisa waliopo kwenye rejesta itakayofungwa tarehe 6 Oktoba 2021 watapokea ujumbe mfupi wenye mwongozo wa namna ya kushiriki. Mkutano mkuu utaoneshwa mubashara kupitia kiunga cha wavuti kwenye simu janja. Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea tovuti ya Kampuni **https://vodacom.co.tz/investors**.

Wanahisa watagharamia matumizi ya data na mtandao. Kampuni haitawajibika na upotevu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya kimtandao/kuishiwa muda wa hewani/kukatika kwa umeme/na matatizo ya kiufundi yanayoweza kuathiri ushiriki wa kielektroniki kwenye mkutano mkuu.

Wanahisa wanahimizwa kutuma maswali yatokanayo na maazimio yaliyopo kwenye taarifa hii kabla ya mkutano mkuu kwenda kwenye barua pepe **investorrelations@vodacom.co.tz** kabla ya Ijumaa ya tarehe 8 Oktoba 2021 saa 4:00 asubuhi. Majibu ya maswali hayo yatatolewa katika mkutano mkuu. Uwasilishaji wa maswali haumzuii mwanahisa kuuliza maswali siku ya mkutano mkuu.

## Mahudhurio

Wanaostahili kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.


Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Fomu ya uwakilishi iliyojazwa, inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni **https://vodacom.co.tz/investors** pamoja na nakala ya hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, kitambulisho cha taifa/kura/leseni ya udereva na taarifa za mawasiliano vitumwe kwa barua pepe kwenda **investorrelations@vodacom.co.tz** au viwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni, Vodacom Tower, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Ijumaa ya tarehe 8 Oktoba 2021. Uwasilishaji wa fomu ya uwakilishi haumzuii mwanahisa kuhudhuria mkutano.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapaswa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenye hisa zisizokuwa katika majina yao lazima wawapatie watunzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoyatoa kwake.

Wanahisa wanahimizwa kutembelea tovuti ya Kampuni kwa taarifa zaidi.

Imeidhinishwa na Bodi



**Caroline M Mduma**
Katibu wa Kampuni

20 Septemba 2021

# Fomu ya Mwakilishi

**Vodacom Tanzania PLC**
(Imesajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya Usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
("Vodacom" au "Kampuni")

**Kifungu A**
**Ijazwe na wanahisa wote**

Jina Kamili

Namba ya hati ya hisa (CDS A/c No)

Idadi ya hisa mwanahisa anazomiliki

**Kifungu B**
**Ijazwe na wanahisa watakaoteuwa wawakilishi (na si Mwenyekiti) kuhudhuria mkutano kwa niaba yao**

Mimi(Sisi), mwenye/wenye hati ya hisa zenye idadi ya hisa za kampuni kwa mujibu wa kifungu A, namteua/tunamteua (angalia maelekezo namba 1 & 2)

au akishindwa yeye

au akishindwa yeye

**Mwenyekiti** wa mkutano mkuu wa mwaka kuwa mwakilishi wangu/wetu kuhudhuria, kushiriki mijadala na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika mkutano mkuu wa tano wa mwaka utakaofanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Ijumaa, tarehe 15 Oktoba 2021 kwa lengo la kutoa maamuzi na kupitisha maazimio ya kawaida na maalum, kupiga kura ya kuafiki au kutokuafiki au kutoshiriki kwenye upigaji kura kulingana na hisa zilizoandikishwa kwa jina langu/letu.

**Kifungu C**
**Ijazwe na wanahisa wote**

Weka alama x kwenye kisanduku kulingana na matakwa yako.
**Vinginevyo mwakilishi wako atapiga kura atakavyoona inafaa.**

| | Naafiki | Siafiki | Sishiriki |
|---|---|---|---|
| 1. **Azimio ka kawaida namba 1**<br>Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa nne wa mwaka uliofanyika tarehe 30 Oktoba 2020 | | | |
| 2. **Azimio la kawaida namba 2**<br>Kupitisha taarifa za jumla na binafsi zilizokaguliwa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 | | | |
| 3. **Azimio la kawaida namba 3**<br>Kumchagua Raisibe Morathi kuwa mkurugenzi wa Kampuni | | | |
| 4. **Azimio la kawaida namba 4**<br>Kumchagua Sitholizwe Mdlalose kuwa mkurugenzi wa Kampuni | | | |
| 5. **Azimio la kawaida namba 5**<br>Kumchagua tena Diego Gutierrez kuwa mkurugenzi wa Kampuni | | | |
| 6. **Azimio la kawaida namba 6**<br>Kumchagua tena Jacques Marais kuwa mkurugenzi wa Kampuni | | | |
| 7. **Azimio la kawaida namba 7**<br>Kumchagua tena Kenneth Gomado kuwa mkurugenzi wa Kampuni | | | |
| 8. **Azimio la kawaida namba 8**<br>Kumchagua tena Matimba Mbungela kuwa mkurugenzi wa Kampuni | | | |
| 9. **Azimio la kawaida namba 9**<br>Kuchagua Ernst & Young Inc. kuwa wakaguzi wa Kampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2022 | | | |
| 10. **Azimio la kawaida namba 10**<br>Kumchagua tena Margaret Ikongo kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 11. **Azimio la kawaida namba 11**<br>Kumchagua tena Thembeka Semane kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 12. **Azimio la kawaida namba 12**<br>Kumchagua tena Winifred Ouko kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | | | |
| 13. **Azimio la kawaida namba 13**<br>Kuthibitisha kuwa hakutakuwa na malipo ya gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2021 | | | |
| 14. **Azimio la kawaida namba 14**<br>Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 481 000 kwa mwaka | | | |

Imetiwa sahihi tarehe mwezi Oktoba 2021

Sahihi: Sahihi:

Fomu ya mwakilishi iliyojazwa iwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC kabla saa 4 asubuhi, Ijumaa tarehe 8 Oktoba 2021.

# Maelekezo ya fomu ya mwakilishi

1. Mwanahisa anayepaswa kuhudhuria katika mkutano mkuu anaweza kuteua mwakilishi wake kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yake. Mwakilishi sio lazima awe mwanahisa wa kampuni. Kwa makampuni, fomu ya mwakilishi ijazwe na afisa mwenye mamlaka na iwekwe muhuri wa Kampuni husika.
2. Weka alama 'X' kwenye eneo la kujaza kwenye fomu kulingana na kura unayotaka kupiga katika agenda husika. Iwapo utapenda kupiga kura kwa hisa pungufu ya hisa unazomiliki, onesha idadi ya hisa pungufu ambazo ungependa zipige kura. Iwapo maelekezo haya hayatazingatiwa, mwakilishi atapiga kura atakavyoona inafaa.
3. Mwanahisa anaweza kuweka jina la mwakilishi/wawakilishi wake kwenye sehemu iliyooneshwa kwenye hii fomu bila kufuta kipengele cha kuwakilishwa na "Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka" kilichopo chini ya sehemu ya kuandika majina ya wawakilishi. Mwanahisa atapaswa kuweka sahihi yake iwapo atafuta kipengele hicho. Mwakilishi ambaye jina lake limejazwa likiwa la kwanza kwenye fomu ya uwakilishi akihudhuria mkutano mkuu ndiye atahusika kufanya maamuzi.
4. Fomu za mwakilishi zilizojazwa pamoja na hati ya hisa au risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, ziwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 8 Oktoba 2021. Aidha, fomu zinaweza kusainiwa kisha kuzituma kwa barua pepe ya i**nvestorrelations@vodacom.co.tz.**
5. Mwanahisa akifanya masahihisho/mabadiliko yoyote kwenye fomu ya mwakilishi, atapaswa kuwekwa sahihi yake pembeni ya masahihisho/mabadiliko hayo.
6. Wenye hisa wenye umri mdogo kisheria wanapaswa kusimamiwa na wazazi/walezi wao ambao watapaswa kuwa na nyaraka za kisheria za kuwathibitisha.
7. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa mwaka atakubali fomu ya mwakilishi itakavyokuwa imejazwa tofauti na matakwa haya iwapo ataridhika na namna ambavyo mwanahisa atapenda kupiga kura.
8. Kwa wale wenye hisa za pamoja/vikundi:
   - Yeyote kati yao anaweza kutia sahihi kwenye fomu hii
   - Kura ya mwanahisa mkubwa (ukubwa wa hisa utajulikana kulingana na majina yaliorodheshwa kwenye rejista ya wanahisa wa Kampuni) itakayopigwa na yeye binafsi au kutumia mwakilishi, ndio itakayoruhusiwa kwa niaba ya wanahisa wenzake kwenye kikundi.

**Ms. Caroline Mduma**
Katibu wa Kampuni
Vodacom Tower, Ursino Estate
Kiwanja na 23, Barabara ya Bagamoyo
P.O. Box 2369
Dar es Salaam
Barua pepe: **investorrelations@vodacom.co.tz**

# Taarifa kuhusu umiliki

| Jumla ya hisa | # ya hisa | % ya hisa |
|---|---|---|
| Vodacom Group Limited | 1 680 000 200 | 75.0% |
| Mfuko wa Pensheni wa Wafanyakazi wa Serikali (Uwekezaji wa Shirika la Umma SOC Limited, Jamhuri ya Afrika Kusini) | 164 503 540 | 7.3% |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (Afrika Mashariki) | 250 355 792 | 11.2% |
| Wawekezaji wa Kitaasisi (sehemu nyingine za duniani) | 50 062 653 | 2.2% |
| Wawekezaji wengine[1] | 95 078 115 | 4.3% |
| | **2 240 000 300** | **100.0%** |

[1] Hisa hizi zinaweza kuhusisha uwekezaji kutoka kwenye taasisi au watu binafsi ambazo ziko chini ya kiwango cha uchanganuzi.

| Umiliki wa hisa kitaasisi | Machi 2021 % Umiliki kitaasisi |
|---|---|
| Tanzania | **47.9%** |
| PIC | **35.4%** |
| Uganda | **6.0%** |
| Wanahisa wengine wa kimataifa | **10.7%** |
| | **100.0%** |

# Taarifa za Kampuni

## Vodacom Tanzania Public Limited Company

(imeandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Usajili namba: 38501
(ISIN: TZ1996102715 Share Code: VODA)

## Directors

- TB Mihayo[1] (Mwenyekiti)
- H Hendi (Mkurugenzi Mtendaji)[2]
- JJ Marais (Mkurugenzi wa Fedha)[3]
- D Gutierrez[4]
- D Kastelic[5]
- K Gomado[6]
- M Mbungela[3]
- M Ikongo[1]
- N Nyoka[3]
- R Morathi[3]
- T Semane[3]
- W Ouko[7]

1 Mtanzania
2 Mmisri
3 Mwafrika Kusini
4 Mbolivia
5 Mslovenia
6 Mghana
7 Mkenya

## Katibu wa Kampuni

Caroline Mduma

## Ofisi iliyosajiliwa

Ghorofa ya 15, Vodacom Tower,
Eneo la Ursino, Kiwanja namba 23,
Barabar ya Bagamoyo,
S.L.P 2369, Dar es Salaam, Tanzania

## Msajili Masuala ya Hisa

CSD & Registry Company Limited (CSDR)
Kambarage House,
Ghorofa ya 2 , Mtaa wa 6 Ufukoni
S.L.P 70081, Dar es Salaam, Tanzania

## Mshauri Mkuu aliyesajiliwa wa

Orbit Securities Company Limited
Golden Jubilee Tower
Ghorofa ya 4, (Jengo la PSPF), Mtaa wa Ohio
S.L.P 70254, Dar es Salaam, Tanzania

## Mawasiliano ya Nje

Rosalynn Mworia

## Mahusiano na Wawekezaji

Hilda Bujiku, Albert Maneno
investorrelations@vodacom.co.tz
**https://vodacom.co.tz/investors**

## Mkaguzi wa Hesabu za Fedha

**Ernst&Young**
Ghorofa ya 4, Tanhouse Tower
Kiwanja namba 34/1, Ursino Kusini
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2475, Dar es Salaam, Tanzania

## Watoa huduma za Kibenki

**Citibank Tanzania Limited**
Citibank House
Kiwanja namba 1962, Barabara ya Toure,
Oysterbay
S.L.P 71625, Dar es Salaam, Tanzania

**National Bank of Commerce Limited**
Barabara ya Sokoine & Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1863
Dar es Salaam, Tanzania

**NMB Bank PLC**
Mtaa wa Ohio /Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 9213
Dar es Salaam, Tanzania

**CRDB Bank Plc.**
Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 268
Dar es Salaam, Tanzania

**Standard Chartered Bank Tanzania**
Jengo la International House
Mtaa wa Shaaban Robert/Garden Avenue
S.L.P 9011
Dar es Salaam, Tanzania

## Washauri wa Mambo ya Kisheria

**IIMMMA (Advocates)**
Kiwanja namba 357, IMMMA House
Barabara ya Umoja wa Mataifa, Upanga
S.L.P 72484, Dar es salaam, Tanzania

**Lawhill**
14112 Regent Estate Mikocheni
Mtaa wa Historia, Kiwanja namba 311, Nyumba namba 96
S.L.P 105646, Dar es salaam, Tanzania

# Dai la haki

## Taarifa zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ('IFRS')

Taarifa hii ina baadhi ya hatua zisizofuata Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha ambazo hazijapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi la Kampuni za Vodacom ('Kundi'). Menejimenti ya Kundi inaamini hatua hizi zinatoa taarifa muhimu za ziada kwa kuelewa ufanisi wa Kundi la Vodacom au biashara za Kundi la Vodacom kwa sababu zinaeleza hatua zilizotumiwa na Kundi la Vodacom kutathimini ufanisi. Hata hivyo, taarifa hizi za ziada zilizowasilishwa hazikufasiliwa kwa njia inayofanana na kampuni zote, ikiwa ni pamoja na zile zilizo katika tasnia ya Kundi la Vodacom. Hivyo, inawezekana haiwezi kulinganishwa na hatua zinazofanana na kutolewa taarifa na kampuni nyingine. Kwa kuongezea, ingawa hatua hizi ni muhimu katika usimamizi wa biashara, hazipaswi kuangaliwa kipwekepweke au kama mbadala, badala yake ziwe kama kijalizo, katika hatua za Kanuni za Kimataifa za Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha. Rejea katika sehemu ya 'Ufanisi wetu' ya taarifa hii kwa maelezo yanayohusiana na mapato ya huduma, EBIT na mapato kwa kila hisa.

## Alama za Biashara

Vodafone, logo ya Vodafone, M-Pesa, Vodacom, Wakulima Waliounganishwa na Vodafone Supernet ni alama za biashara za Vodafone Group Plc (au ina program zinazosubiria). M-Fundi, M-Shamba, M-Pawa na Vodacom Faraja ni alama za biashara za Vodacom Tanzania Public Limited Company (au ina program zinazosubiria). Bidhaa zingine na majina ya kampuni yaliyotajwa hapa yanaweza kuwa alama za biashara za wamiliki wao husika.

## Matamko ya Matarajio

Taarifa hii, ambayo inajumuisha matokeo ya Kundi la makampuni kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2021, ina 'matamko ya matumaini', ambayo hayajapitiwa au kuripotiwa na wakaguzi wa Kundi, kuhusiana na hali ya kifedha ya Kundi, matokeo ya uendeshaji na biashara na taarifa zinazohusiana na mipango na malengo ya Kundi la Vodacom. Hasa, matamko hayo ya kuangalia mbele yanajumuisha matamko yanayohusiana na: ufanisi wa baadaye wa Kundi la Vodacom; matumizi ya mtaji siku zijazo, ununuzi, kujitoa, gharama, mapato, masharti ya kifedha, sera ya gawio na maendeleo ya baadaye; mikakati ya biashara na uwekezaji inayohusiana na upanuzi na ukuaji wa Kundi la Vodacom; athari za udhibiti wa biashara za Kundi la Vodacom unaofanywa na serikali katika nchi inapofanya shughuli zake; matarajio ya Kundi la Vodacom kuhusiana na tarehe za uzinduzi na kuanza uuzaji wa bidhaa, huduma au teknolojia; matarajio kuhusu mazingira ya uendeshaji na hali ya soko; ongezeko la wateja na matumizi; na kiwango cha ongezeko la gawio kwa Kundi.

Matamko ya kuangalia mbele wakati mwingine, lakini si wakati wote, hubainishwa kwa matumizi yao ya tarehe katika wakati ujao au Maneno kama 'nita', 'tarajia', 'kusudia', 'ninge', 'weza', 'paswa', 'amini', 'panga' au 'lenga' (pamoja na miundo yao ya ukanushi).

Kwa hali yao, matamko ya kuangalia mbele kwa asili yanatabirika, yanaweza kukisiwa na yanajumuisha hatari na mashaka kwa sababu yanahusiana na matumio na yanategemea mazingira ambayo yanaweza kutokea au yasitokee siku za baadaye. Kuna sababu mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha matokeo halisi na maendeleo kutofautiana kabisa kuanzia yale yaliyoelezwa au kumaanishwa na matamko haya ya kuangalia mbele. Sababu hizi ni pamoja na, ingawa haziishii hapo, zifuatazo: mabadiliko katika hali ya kiuchumi au kisiasa katika masoko yanayohudumiwa kwa shughuli za Kundi la Vodacom; ushindani mkubwa kuliko ilivyotarajiwa; gharama kubwa kuliko ilivyotarajiwa au matumizi ya mtaji; ongezeko dogo la wateja kuliko ilivyotarajiwa na kupungua kwa wateja wa kudumu; mabadiliko katika hali ya matumizi ya wateja wapya na waliopo; uwezo wa Kundi kupanua nafasi yake kimawanda au kuongeza muda au kuchukua leseni mpya; uwezo wa Kundi kufanikisha kuokoa gharama; uwezo wa Kundi kutekeleza mkakati wake wa kutumia mkongo; kuanza kutoa bidhaa na huduma mpya; huduma za data (mobile data), upanuzi wa Biashara na mtandao wa 4G, mabadiliko katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile katika viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, na vilevile viwango vya riba; uwezo wa Kundi kupata faida kutokana na kuingia katika ubia au kufanya biashara pamoja na kuingia katika kufanya biashara ya huduma na utoaji wa leseni ya chapa; matokeo yasiyofaa kwa Kundi ya kufanya na kuchanganya ununuzi na utupaji; mabadiliko katika mfumo wa kisheria ambapo Kundi huendesha shughuli zake; athari za mashauri ya kisheria na mengineyo; kupoteza wasambazaji au kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji; maendeleo katika hali ya fedha ya Kundi, mapato na fedha zinazosambazwa na mambo mengine ambayo Bodi imezingatia wakati wa kuamua viwango vya magawio; uwezo wa Kundi kuwa na mtaji wa kufanyia kazi na mahitaji mengine; mabadiliko katika viwango vya kodi kisheria au mchanganyiko wa faida; na/au mabadiliko katika sharia ya kodi. Matamko mengine yote yaliyofuata ya kuangalia mbele yawe kwa maandishi au mdomo ambayo ni ya Kampuni, kwa mhusika yeyote wa Kundi au kwa watu wowote wanaofanya kwa niaba yao wanastahili katika wingi wao kwa sababu zinarejelewa hapo juu. Uhakika hauwezi kutolewa kuwa matamko ya kuangalia mbele katika waraka huu yatafikiwa. Kutegemea kufuata sharia na kanuni zinazotumika, Kampuni haikusudii kuboresha matamko haya ya kuangalia mbele na haichukui wajibu wowote wa kufanya hivyo.

vodacom